**15 SEPTEMBA, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 15 Septemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAJI:**

Maelezo ya Waziri wa Maji kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *[The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022]*.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *(The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022)*.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

Na. 39

### Hitaji la Nyumba za Watumishi Wa Halmashauri – Geita

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU K.n.y. MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi waliohamishiwa Halmashauri mpya Nzera?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku Mbunge wa Jimbo la Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi Milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, ambapo ujenzi wa nyumba hiyo unaendelea na upo katika hatua ya upauaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetengewa kiasi cha Shilingi Milioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili (2) za Wakuu wa Idara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Halmashauri nyingine kote nchini zenye upungufu wa nyumba za watumishi kuendelea kutenga bajeti za mapato ya ndani kila mwaka ili kutatua changamoto za upungufu wa nyumba za watumishi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ni moja ya Halmashauri mpya ambazo zilianzishwa miaka michache iliyopita. Ambazo watumishi wake wengi bado wanaishi kwenye Halmashauri za

zamani. Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na *NHC*, imekuwa ikijenga nyumba na kukopesha watumishi na Halmashauri hiyo ina viwanja tayari vimepimwa. Ni kwa nini TAMISEMI, wasiingie mkataba na Wizara ya Ardhi, kujenga nyumba na kuirahisishia Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Miji mingi Tanzania imekuwa ikikua lakini kwa ujenzi holela. Kwa nini Serikali kwa sababu ni sharti moja la Miji hiyo kupanda hadhi na kuwa Manispaa au Miji mikubwa isiingie utaratibu na Wizara ya Ardhi kuipima Miji yote ili kuzuia ujenzi holela ambao unaendelea?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, Mheshimiwa Constantine Kanyasu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala la Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kuingia makubaliana na Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya kuitumia *NHC* kujenga nyumba za watumishi, Serikali imekuwa ikifanya hivyo katika Halmashauri mbalimbali. *NHC* wamejenga nyumba na watumishi wameuziwa au wanapangishwa na wanaendelea huduma katika maeneo hayo. Kwa hiyo, tumepokea wazo la Mheshimiwa Kanyasu tutafanya utaratibu huo ili kuona uwezekano wa kujenga nyumba hizo katika Halmashauri ya Geita Vijijini lakini pia Geita Mjini baada ya kuongea na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusiana na upimaji wa Miji, Serikali ilishaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza jukumu lao la kupima ardhi katika maeneo yao. Kwa hiyo, suala hili ni suala la msingi na jukumu la msingi la Halmashauri kazi zinaendelea, ni kweli kwamba kasi ya upimaji imekuwa ndogo na ujenzi holela umeendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote kote nchini, kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao wa kupima maeneo ya ardhi katika Miji ili kuzuia ujenzi holela.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kabla sijatoa nafasi ya maswali ya nyongeza niwakumbushe maswali ya nyongeza ni mafupi na yaende moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Yustina Rahhi swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imekamilisha jengo la utawala na wamehamia katika makao mapya yaliyoko Dongobeshi, lakini kuna changamoto kubwa ya nyumba za watumishi.

Je, Serikali itawejengea lini nyumba za watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu limekamilika lakini kuna changamoto ya nyumba za watumishi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka mpango baada ya kukamilisha jengo la watumishi sasa tutakwenda kufanya utaratibu wa kujenga nyumba za watumishi ili watumishi waishi karibu na Makao Makuu ya Halmashauri na kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Halmashauri ya Mji ya Bunda ni mpya tayari imejenga jengo la ofisi ya Halmashauri, lakini kuna changamoto kubwa sana ya nyumba za watumishi wakiwemo Walimu, Madaktari na watumishi wa halmashauri. Ni lini sasa Serikali itajenga na hasa ukisema utegemee Halmashauri ya Bunda mapato yake ni madogo?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Mji wa Bunda, imejengewa jengo la halmashauri kwa maana ya jengo la utawala, lakini changamoto ya nyumba za watumishi ipo na Serikali inatambua changamoto hiyo. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Bunge Mjini kwamba wewe pamoja na Mheshimiwa Mbunge Maboto mnashirikiana vizuri kuhakikisha nyumba za watumishi zinajengwa pale na

Serikali itaendelea kufanya utaratibu kuona uwezekano wa kujenga nyumba za watumishi pale.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu katika shule za msingi na sekondari Mkoa wa Simiyu.

Je, ni lini Serikali itajenga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba Mkoa wa Simiyu lakini pia Mikoa yote kote nchini bado kuna changamoto ya upungufu wa nyumba za watumishi wa sekta ya afya, sekta ya elimu pia sekta na idara nyingine. Mpango wa Serikali tumeendelea kujenga nyumba za watumishi lakini safari ni hatua tunakwenda kwa awamu. Tumeendelea kujenga, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri hizo, Serikali imeelekeza kuhakikisha wanaanza kutenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba hizo, pia Serikali Kuu itaendelea kujenga kwa awamu. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi.

Na. 40

**Kuboresha Wodi za Wazazi Nchini**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI K.n.y. MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Wodi za Wazazi nchini pamoja na kuongeza huduma hizo kwa Wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2018/2019 mpaka sasa, Serikali imejenga Hospitali mpya za Halmashauri 127 kati ya hizo Hospitali 70 zimeshasajiliwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo huduma za dharura, upasuaji na wodi za Wazazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Vituo vya Afya 822 vimekarabatiwa na kujengwa ambapo kati ya hivyo 476 vinatoa huduma za dharura, upasuaji na wodi za wazazi. Wodi za Wazazi zimeboreshwa kwa kuweka maeneo yote muhimu kwa huduma za uzazi salama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 12.5 kwa ajili ya kujenga hospitali 25 zitakazokuwa na Wodi za Wazazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani umekaa na nawakumbusha kila siku. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Morogoro.

Je, ni lini Serikali itahakikisha dawa zote zinazohitajika kwenye wodi za kinamama na vipimo vyote zinapatikana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Kituo cha Afya cha Mkoani Ruvuma, Wilaya ya Songea, Kata ya Ruvuma, kumekuwa na tatizo la Madaktari na Matabibu ambao ni wachache sana hawakidhi kutoa huduma ya afya ipasavyo.

Je, ni lini Serikali itaongeza Madaktari na Matabibu kwenye kituo cha afya hiki ili huduma sahihi ziendelee kutolewa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuboresha upatikanaji wa dawa lakini pia vitendanishi na vifaa tiba katika vituo vyetu. Katika kipindi cha

mwaka huu fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa tiba, Bilioni 69.95 kwa ajili ya kununua vifaatiba katika Vituo vya Afya 530 nchini kote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, bajeti ya dawa imeongezeka na mwaka huu wa fedha bajeti ya dawa imeongezeka. Kwa hiyo, nimhakiksishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imedhamiria kuhakikisha inaondoa changamoto ya upungufu wa baadhi ya dawa kwenye Wodi za Wazazi lakini kwenye vituo kwa ujumla lakini kuboresha huduma za vipimo vya maabara.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na Kituo cha Afya katika Kata ya Ruvuma juu ya uchache wa Madaktari na Matabibu, Serikali imeendelea kuajiri watumishi, mtakumbuka mwisho mwa mwaka uliopita watumishi wa afya zaidi ya 7,000 wameajiriwa na kupelekwa nchini kote, zoezi hili ni endelevu tutaendelea kuajiri kwa kadri ya upatikanaji wa fedha ili watumishi hawa watoe huduma bora za afya katika vituo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Christine Ishengoma swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaanzisha huduma za upasuaji katika Kituo cha Afya cha Mafiga, Mkoani Morogoro Manispaa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, vituo vya afya vikijengwa vinajengwa na majengo ya upasuaji na dhamira ya Serikali ni mara tu majengo ya upasuaji yakikamilika huduma za upasuaji zianze. Kwa hiyo, kama Kituo hiki cha Afya, Mafiga, jengo la upasuaji limekwishakamilika, naelekeza Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro waanze huduma za upasuaji haraka iwezekanavyo, lakini kama kituo hakijakamilika wakamilishe na baada ya hapo wasajili ili huduma za upasuaji ziweze kuanza. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itarekebisha au kupunguza bei ya huduma ya upasuaji hasa ya uzazi katika hospitali za rufaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha inatoa huduma ambazo zinaendana na gharama kwa maana ya kupunguza gharama za matibabu na hasa eneo la upasuaji. Katika hospitali za Rufaa za Mikoa, bado gharama za upasuaji ni changamoto na tumekubaliana na Wizara ya Afya, pia katika maeneo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Vituo vya Afya na hospitali za Halmashauri, bado gharama za upasuaji ni kubwa. Kwa hiyo, tunapitia lakini baada ya muda tutatoa gharama ambazo zitakuwa zinafikika kirahisi kwa wananchi wetu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kuiuliza Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa jengo la *x-ray* katika Kituo cha Afya Inyecha, kwa sababu Serikali imeshaleta mashine ya *x-ray* na wananchi kwa nguvu zao wamejenga hadi hatua za boma.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha jengo hilo la *x-ray*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Chikota, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imekwishapeleka mashine ya *x-ray* katika Kituo hiki cha Afya cha Inyecha, lakini jengo lile halijakamilika tumekubaliana na Halmashauri, kwanza watenge fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo, pia Serikali itaona namna ya kuongeza nguvu ili kukamilisha jengo hilo na kuanza kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Je, ni lini Serikali italeta mashine ya *ultra sound* kwa ajili ya wanawake wajawazito katika Hospitali ya Rufaa ya Ligula? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara, maarufu kwa jina la Ligula, iko chini ya Wizara ya Afya nasi kama Serikali tunachukua hoja hiyo kuona uwezekano wa kupeleka mashine ya *ultra sound* mapema iwezekanavyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa Spika, nauliza ni lini Zahanati ya Mdunduwaro – Songea Vijijini itamalizika ili wananchi wale wapate huduma, toka 2014.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ntara, amekuwa akifuatilia sana suala la Zahanati ya Mdunduwaro nami nimekwisha wasiliana na Watendaji mara kadhaa tukiwa nae na ujenzi unaendelea vizuri hatua za ukamlisha. Tulishakubaliana, ifikapo Septemba, mwisho mwaka huu Zahanati ya Mdunduwaro itaanza kutoa huduma. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, kuhakikisha kwamba zahanati hii inakamilika mwisho mwa mwezi Septemba, ianze kutoa huduma kwa wananchi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Hitaji la Kituo cha Afya Kagera/Nkanda – Kasulu**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Kagera/Nkanda Wilayani Kasulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilipeleka Shilingi Bilioni 1.4 kwenye Halmashauri ya Wilaya Kasulu kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kitanga, Nyenge na Rungwe Mpya. Ujenzi wa vituo hivi upo hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 itatenga fedha Shilingi Milioni 500 kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Kagera/Nkanda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JASEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu yake nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Kagera/Nkanda iko kilomita 70 kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Kutoka Kagera/Nkanda mpaka Mgonde mara nyingi hutokea uhalifu wa utekaji wa magari, ikitokea dharura usiku wanawake wanashindwa kufikishwa katika hospitali ya Wilaya kutokana na kuogopa kutekwa magari usiku.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka gari la kubebea wagonjwa katika Kata ya Kagera/Nkanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Kata hii ya Kagera Nkanda iko mbali sana kutoka Makao Makuu na ndiyo maana katika mwaka ujao wa fedha Serikali itatenga Milioni 500 kuhakikisha tunajenga kituo cha afya katika Kata hii na kuondolea wananchi changamoto ya kusafiri umbali mrefu kwenda kupata huduma za afya katika hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba katika mwaka huu wa fedha, Serikali itapeleka magari ya wagonjwa, Halmashauri hii pia itapata

gari moja la wagonjwa. Kwa hiyo, sasa Halmashauri inaweza kuona namna ya kulipeleka katika eneo hili ili litoe huduma bora kwa wananchi wa Kata hiyo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kata ya Kalembo, Isongole pamoja na Malangali katika Wilaya ya Ileje ni miongoni mwa Kata ambazo hazina kituo cha afya. Naomba kufahamu, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata hizo? Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shonza, amekuwa mara kwa mara akiulizia kuhusiana na Kata hizi na amekuwa akiwasemea kwa dhati wananchi wa Mkoa wa Songwe. Nimhakikishie kwamba Serikali itaendelea kuhakikisha inakwenda kwa awamu na kimkakati kujenga vituo vya afya katika Kata ambazo amezitaja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Kizazi ambacho kimejengwa kwa nguvu za wananchi katika Jimbo la Muhambwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mbunge wa Jimbo la Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Kata aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge wametoa nguvu zao, wameanza ujenzi wa kituo cha Afya na Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia. Tumekubaliana kwamba tukipata fedha tutakwenda kuchangia nguvu za wananchi pale, kituo cha afya kikamilike tuanze kutoa huduma za afya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunakwenda kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hiyo. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, Vituo Vya Afya cha Chihangu pamoja na Mkwedu muda mrefu havina wodi za kulaza wagonjwa.

Je, ni lini Serikali itaenda kujenga wodi katika Vituo hiyo vya Afya vilivyoko Jimbo la Newala Vijijini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais -TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini kama ifutavyo: -

Mheshimiwa Spika, vituo vyetu vya afya vingi havina wodi za wazazi pamoja pia na wodi za wagonjwa wengine, kama vituo hivi ambavyo Mheshimiwa Maimuna Mtanda amevitaja. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuna mpango wa kuhakikisha vituo vyote ambavyo havina majengo toshelezi tunakwenda kujenga majengo hayo kwa awamu ili yaweze kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga Japhet, swali la nyongeza**.**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Kituo cha Afya cha Kata ya Msiha na Kata ya Hiyanda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais -TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga Mbunge wa Jimbo la Vwawa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatoa maelekezo kwa Halmashauri zetu zote kuweka vipaumbele vyao vya ujenzi wa vituo vya afya katika tarafa na kata za kimkakati. Kwa hivyo kama hizi ni kata za kimkakati, nimhakikishie Mheshimiwa Hasunga, kwamba Serikali kupitia mapato ya ndani lakini kupitia fedha ya Serikali Kuu tutaendelea kuweka hatua za ujenzi ili vituo viweze kukamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita Kisau, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa tulishasema tumalize vituo vya afya kwenye tarafa ambazo hazina;

Je, ni lini Serikali itajenga Vituo kwa Tarafa za Makame, Dosudosi na Kibaya ambazo bado hazina? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais -TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Wakili Olelekaita Mbunge wa Jimbo la Kiteto kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli, Jimbo la Kiteto lina Tarafa ambazo bado hazina Vituo Vya Afya, na Mheshimiwa Mbunge amekuwa mara kwa mara akifuatilia hili. Nimhakikishie, kwamba mpango wa Serikali ni kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika tarafa ambazo hazina vituo vya afya, na tutakwenda pia kutoa kipaumbele katika Tarafa za Jimbo la Kiteto ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza**.**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, je lini Serikali itajenga Vituo Vya Afya katika Kata za Nyamigogo, Kabindi, Kaniha, na Nyatakala Wilayani Biharamulo? Kwasababu tuna uhitaji mkubwa wa Vituo Vya Afya katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais -TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge na uhitaji wa vituo vya afya tutakwenda kufanya tathmini na kuona uwezekano wa mapato ya ndani kujenga vituo hivyo, lakini pia kutafuta fedha Serikali Kuu kwa ajili ya kujenga vituo hivyo kama vitakidhi vigezo vile vya kujenga vituo vya afya katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Naomba kujua, je, gari la wagonjwa lililoahidiwa kwenye Kituo Cha Afya Mgeta litaenda lini kwenye kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais -TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Boniphace Mwita Getere Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kata aliyoitaja na uhitaji wa kituo cha afya hicho tutakwenda kuona uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho kama kitakidhi vigezo tulivyoweka kwa ajili ya vituo vya afya vya Kimkakati ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Je lini Serikali itajenga Vituo Vya Afya katika Kata za Igundu, Muhura na Kitengule katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais -TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kajege Mbunge Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge zinahitaji vituo vya afya, na amekwisha leta kama vipaumbele vya jimbo lake. Nimhakikishie, kwamba tumekubaliana na halmashauri, kwamba kwanza waanze kutenga fedha kwa awamu kupitia asilimia arobaini ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya hivyo; lakini pia Serikali itakwenda kuunga mkono nguvu hizo kwa ajili ya kukamilisha vituo vya afya katika maeneo hayo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaenda Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Uwiano wa Jinsia kwa Nafasi za Uteuzi na Nafasi za Ajira Nchini**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, nini Sababu ya kukosekana uwiano wa jinsia ya kike kwenye nafasi za uteuzi na ajira nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kunakuwepo na uwiano sawa wa kijinsia kwenye nafasi za uteuzi na ajira nchini kwa kuweka mazingatio ya usawa wa kijinsia katika nyaraka zinazosimamia Utumishi wa Umma, ikiwemo Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2008 inayotaka kila mamlaka ya ajira kuhakikisha uwiano wa kijinsia katika uteuzi na ajira zote. Pia Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2019, Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2009 pamoja na Kanuni za Uendeshaji wa Shughuli za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimeiwezesha Serikali kuwa kwenye nafasi nzuri ya kufikia uwiano sawa wa kijinsia katika nafasi za Uteuzi na ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa suala hili ni kipaumbele cha Dunia kupitia ajenda 2020/2030 kuhusu Maendeleo Endelevu, Lengo Na. 5 Usawa wa Kijinsia, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameazimia kuhakikisha uwepo wa uwiano sawa wa kijinsia katika nafasi mbalimbali za uteuzi katika kipindi chake cha uongozi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iko katika hatua za mwisho za kutoa Mwongozo wa Ujumuishwaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma. Mwongozo huu unatoa maelekezo kwa mamlaka za ajira katika utumishi wa umma kote nchini kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wanakuwa na fursa sawa kuanzia katika mchakato wa ajira, upandishaji madaraja, uteuzi, mafunzo, ubadilishanaji pamoja na urithishaji madaraka. Lengo likiwa ni kuondoa vikwazo kwa kujenga uwezo wa ushindani kwa jinsia zote ili kupata sifa stahiki za kushika madaraka na fursa mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma Murtazar Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, na nimpongeze sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kulipa kipaumbele suala la jinsia katika ajira katika kipindi chake.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 22 na 23 ya katibu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haki ya usawa wa ajira na ujira ni ya raia wote wa nchi yetu kwa shughuli yoyote inayosimamiwa na mamlaka yetu ya nchi.

Sasa, je, Mheshimiwa Waziri kwa nini hamuoni jambo la busara kwenda kumshauri Mheshimiwa Rais ili sasa Serikali ije ilete sheria ili hizo kanuni zenu na miongozo iingie humo iwe sheria, ili yoyote yule ambaye atakiuka sheria hiyo aweze kuadhibiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA.** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wote humu ni mashahidi, Mheshimiwa Rais wetu wa awamu ya sita Mama yetu Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya dhati ya kuweza kuleta uwiano sawa katika nafasi za uteuzi. Lakini vilevile sisi kama Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kama nilivyosema awali kwenye majibu yangu ya msingi, tumeanza kuweka miongozo, tunaandaa namna ya kuweza kupata usawa katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, miongozo ya Sekretarieti ya Ajira inasema wazi pale endapo *candidate* wawili watagongana maksi na mmoja ni mwanamke, basi atachuliwa yule mwanamke katika kuingia katika ajira ya Utumishi wa Umma. Miongozo hii ipo na tutaendelea kuisimamia na kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini niwatoe mashaka, Mheshimiwa Rais ameweza kutafuta fedha kutoka *European Union,* Serikali ya *Finland* na Serikali yetu ya Tanzania vilevile imewekeza fedha katika Chuo kile cha Uongozi *Institute;* ambapo sasa tunaenda kutoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake zaidi ya 500. Na hivi ninavyozungumza tayari kuna wanawake 50 ambao wapo katika mafunzo ya uongozi kwenye Taasisi yetu ya Uongozi *Institute*. Watakapo maliza wao wanakuja tena wanawake mia 100 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuweza kupata mafunzo ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imejipanga vyema katika kuhakikisha wanawake wanapata fursa sawa katika uteuzi na ajira nchini. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani maswali yenu yote ya msingi ameshamaliza kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunakushuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Emmanuel Lekisho Shangai Mbunge wa Ngorongoro sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Hitaji la Vitambulisho vya Taifa na Vyeti vya Kuzaliwa**

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Vitambulisho vya Taifa na vyeti vya kuzaliwa wananchi wa Kata za Ololosokwan, Soitsambu na Enguserosambu Ngorongoro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhandisi Masauni majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Shangai Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika**,** hadi kufikia mwezi Agosti 2022 jumla ya wananchi 84,637 katika Wilaya ya Ngorongoro wametambuliwa na kusajiliwa. Namba za Utambulisho 61,237 ambayo ni sawa na asilimia 72.3 ya wananchi wote waliotambuliwa na kusajiliwa zimezalishwa na kugawiwa kwa wananchi. Aidha, jumla ya vitambulisho 46,997 ambayo ni sawa na asilimia 76.7 ya namba za utambulisho tajwa vimezalishwa pamoja na kugawiwa kwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, usajili na utambuzi wa wananchi na uzalishaji na ugawaji Vitambulisho vya Taifa ni kazi endelevu. Hivyo, Mamlaka itaendelea na usajili wa wananchi wanaokidhi vigezo kupitia ofisi za usajili wa wilaya pamoja na kuzalisha na kugawa Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi kupitia katika kata zote.

Mheshimiwa Spika, usajili na utoaji wa vyeti vya kuzaliwa bila malipo unaendelea katika vituo vyote vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto pamoja na vituo vya kata.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Lekisho Shangai, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwenye Kata nilizotaja za Oldonyosambu, Ololosokwan, Solosambu pamoja na Soitsambu ni kwamba kuna wananchi wengi ambao fomu zao zimezuiliwa kwenye Ofisi ya Uhamiaji.

Je, ni lini Serikali itamaliza uhakiki kwa haraka ili wananchi wapate Vitambulisho vya Taifa pamoja na vyeti vya kuzaliwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuna wananchi wengi Wilaya ya Ngorongoro hasa Kata ya Orgosorok Loliondo; wengi wao wazazi wao walizaliwa Tanganyika wamefanya kazi walikuwa watumishi na wengine wamestaafu lakini bado wanasumbuliwa hata kupata vitambulisho vya Taifa pamoja na vitambulisho vya kuzaliwa.

Je, Waziri yuko tayari kuongozana nami kwa ajili ya kutatua matatizo ya wananchi hao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mbunge wa Ngorongoro kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nikianza na ombi lake la kutaka tuambatane pamoja kwenye jimbo lake kutatua changamoto hizi mbili; nimhakikishie Mheshimiwa Lekisho Shangai tutafanya hivyo. Naamini tutakapokuwa tumekwenda kwenye hiyo ziara jimboni kwake tutaweza kujua na kupata undani wa changamoto alizozungumza ili tuweze hatua stahiki ili wananchi hawa wanaostahiki haki yao ya msingi ya kupata vitambulisho waweze kupata; ikiwemo wale ambao amezungumza mara ya kwanza ambao fomu zao Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba zimezuiwa uhamiaji. Vile vile hata wale ambao amesema ni raia lakini bado wameshindwa kutambuliwa

Mheshimiwa Spikam, changamoto zote hizi mbili tutazishughulikia mimi na yeye kwa pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar, swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa vitambulisho vya Taifa, kwa mfano *NIDA*, ni kazi kubwa kuvipata au ni janga kubwa kwa wananchi kuweza kuvipata.

Je! Mheshimiwa Waziri ataliambia Taifa au atawaambia wananchi watu ili kuweza kuvipata kwa wepesi waweze kupita njia gani ikiwa ni haki yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu**.**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fakharia kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna changamoto kidogo ya upatikanaji wa vitambulisho na changamoto hii inatokana na ukweli kwamba, tulikuwa na changamoto ya kimikataba kati ya mkandarasi ambaye alikuwa anapaswa kutoa huduma hiyo. Changamoto nyingine ilitokana na upungufu wa kadi ghafi ambazo ndizo zinatumika kuzalisha vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, ikiwemo na changamoto ya tatu vilevile ambayo ni changamoto ya upatikanaji wa kadi ghafi zenyewe katika soko la dunia zilizosababishwa na athari za UVIKO-19. Kwa hiyo changamoto hizo ndizo zilizosababisha tukajikuta kwamba hatuna kadi za kutosha za kuzalisha vitambulisho hivi.

Mheshimiwa Spika lakini nataka nimkikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali imefanya jitihada kuhakikisha changamoto zote hizi tatu zinatatuliwa. Nimani yangu kwamba changamoto za upatikanaji vitambulisho zitapungua hatua kwa hatua. Hata hivyo, nitoe wito kwa wananchi ama Waheshimiwa Wabunge kuwajulisha wananchi katika maeneo ambayo wanayasimamia na kuyaongoza, kwamba upatikanaji wa namba ya utambulisho bila kuwa na kadi unawezesha vilevile kuwafanya waweze kupata huduma mbalimbali za kijamii. Hivyo, kwa wale ambao bado wanasuburi kupata kadi zao waendelee kutumia namba za utambulisho wakati Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kwamba watanzania wote waliosajiliwa na kutambuliwa wanapata vitambulisho vya Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, swali langu limeshaulizwa, nilitaka kujua ni kwa nini watu wanachelewa kupata vitambulisho, ameshajibu Mheshimiwa.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ndani ya Jimbo la Momba wapo baadhi ya wananchi wengi kadhaa ambao wamekosa kunufaika na Mfuko wa *TASAF* na zoezi la

kuandikishwa kwenye mbolea kwa sababu wamekosa vitambulisha vya Taifa.

Je, ni lini Serikali itachukuwa jambo hili kwa haraka na kwa dharula ili wananchi hawa waweze kupata haki yao ya msingi kwenye mahitaji hayo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe Mbunge wa Momba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wananchi kukosa huduma mbalimbali, nilieleza katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Fakharia kwamba namba za utambulisho zinaweza kutumika katika kupata huduma mbalimbali. Lakini kama kuna changamoto katika maeneo mahususi ambayo ameyagusia Mheshimiwa Mbunge, kwa mfano eneo hili la *TASAF* na sensa kama nilivyosikia sawa sawa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, na mbolea.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, na mbolea! Basi nilichukuwe pamoja na kukaa na Mawaziri wa sekta husika hili tuweze kulifanyia kazi kama Serikali. Lakini suluhisho la kudumu ni kuhakikisha kwamba watanzania wote wanapata vitambulisho vyao, na ndicho kipaumbele cha Serikali na tunachukuwa jitihada ili kuhakikisha hili linatekelezeka. Na kwa bahati njema katika bajeti hii ya mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 42.5 kwa ajili ya ununuzi wa kadi ghafi milioni nane laki tano.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa kadi ghafi hizo utasaidia sana kuepukana na changamoto mbalimbali ikiwemo changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge amezungumza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tulipokuwa tunafanya elimu ya sensa katika Mkoa wetu wa Iringa kuna baadhi ya vijiji wana vijiji kabisa hawajui kabisa kama wanapataje namba za utambulisho, na kuna baadhi wana namba za utambulisho muda mrefu sana hawajapatiwa *NIDA*.

Je, ni lini sasa waliopata namba watapata na wale ambao hawajasajiliwa watapata angalau elimu wajue wanasajiliwaje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kuongeza jitihada za kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na huduma hii ya vitambulisho na katika kufanya hivyo kuna njia kadhaa. Njia moja ni kuhakikisha kwamba huduma hizi zinasogea karibu na wananchi. Katika kufanya jitihada hizo, Serikali imefanya kazi kubwa sana kuhakikisha inaimarisha Ofisi za *NIDA* katika ngazi za chini kwa maana ya Wilayani ili Maafisa hawa wa *NIDA* waweze kuwa karibu na wananchi na waweze kutoa huduma ikiwemo hii huduma ya Elimu kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo, katika bajeti ya mwaka huu tunatarajia kuongeza ujenzi wa vituo zaidi 31 katika wilaya 31 nchini. Lengo ni kuhakikisha kwamba Wilaya zote katika nchi hii zinapata huduma ya *NIDA* ili kuwa karibu na wananchi waweze kupata huduma mbalimbali ikiwemo elimu itakayowezesha kuwasaidia kujua haki zao za msingi katika kupata kadi na vitambulisho vya *NIDA* kwa ujumla wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwenye taasisi nyingi za Serikali na zisizo za Serikali kuna mkanganyiko mkubwa kwamba wananchi wengi wenye namba za *NIDA* hawapati huduma. Naomba kauli ya Serikali leo kuhusiana na wananchi wenye Namba za *NIDA* ambao hawana vitambulisho na wanakosa huduma hasa kwenye mikopo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kauli ya Serikali ni kwamba huduma za Serikali popote zilipo zinatakiwa zitolewe kwa kutambua uhalali wa namba za vitambulisho. Kwa sababu hatuwezi kumhukumu mwananchi kutokupata huduma kwa kosa ambalo siyo lake. Kama amechukua hatua zote za kisheria kuweza kujisajili, amepatiwa namba ya kitambulisho na kadi hatujampa kwa kosa ambalo siyo lake, lazima huduma yake ya msingi apate.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kauli ya Serikali ni kwamba taasisi zote zinazohusika za Serikali, kama kuna changamoto basi tutakaa tuzungumze ndani tuone, inawezekana pengine kuna baadhi ya Taasisi kulingana na masuala ya kisheria au masuala ya kimiundombinu zinashindwa kutekeleza hayo. Tutalichukua kama Serikali kwa pamoja tuzungumze tuone tunalitatua vipi maeneo ambayo bado kuna tatizo katika kukibali ama kuzipokea namba hizo za utambulisho wa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdulrahman Mwinyi Mohamed, Mbunge wa Chambani, sasa aulize swali lake.

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nilirebishe jina langu jina langu ni Mohamed Abdulrahman Mwinyi.

Na. 44

**Wananchi wa Wilaya ya Mkoani kupatiwa Vitambulisho vya Taifa Zanzibar**

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI** aliuliza:-

Je, ni lini Wananchi wa Wilaya ya Mkoani waliosajiliwa kwa muda mrefu watapewa Vitambulisho vya *NIDA*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge wa Jimbo la Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeandikisha jumla ya wananchi 47,557 ambayo ni sawa na asilimia 94 ya waliokadiriwa kuandikishwa katika Wilaya ya Mkoani. Aidha, Namba za Utambulisho 45,785 zilizalishwa sawa na asilimia 96 ya wananchi wote walioandikishwa.

Mheshimiwa Spika, jumla ya vitambulisho 41,494 ambayo ni sawa na asilimia 91 ya Namba za Utambulisho vimegawiwa kwa wananchi wa Wilaya ya Mkoani. Aidha, mwezi Septemba, 2022 jumla ya vitambulisho 1,000 vimepelekwa Wilaya ya Mkoani ili vigawiwe kwa wananchi. Serikali itaendelea kuzalisha vitambulisho na kuvigawa kwa wananchi walioandikishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohammed Abdulrahman Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi ambao wamejisajili mwaka 2018, 2019 na 2020 na baadhi yao mpaka leo hawajapata vitambulisho hivyo: Nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati najibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, kuhusu changamoto hii ya upatikanaji wa vitambulisho nilizungumza kwa ujumla wake na majibu yale yale yanaweza kusaidia kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Mwinyi kuhusu changamoto hii ya upatikanaji wa vitambulisho kwa nchi nzima ambayo inakumba majimbo yote likiwemo jimbo la Chambani.

Mheshimiwa Spika, nilieleza hatua gani Serikali imechukua ili kukabiliana na jitihada hizo. Hivyo basi, namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie na majibu yale yale ambayo nimeyajibu ambayo yaliainisha hatua ambazo Serikali inachukua kukabiliana na changamoto ya upungufu wa upatikanaji wa kadi kwa wananchi wa nchi nzima wakiwemo wananchi wake wa Jimbo la Chambani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi swali lingine bado lipo katika Wizara yako. Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Welezo, sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Kuzuia Hati za Kusafiria za Wakandarasi**

**MHE. MAULID SALEH ALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia Hati za kusafiria kwa Wakandarasi wanaoingia nchini kutekeleza miradi mbalimbali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Spika, Serikali haina mkakati wa kuzuia hati za kusafiria kwa Wakandarasi wanaoingia nchini kutekeleza miradi mbalimbali isipokuwa inafanya hivyo kwa mujibu wa sheria pale inapohitajika. Serikali kupitia Sheria ya Uhamiaji Sura Na. 54 rejeo la mwaka 2016, imeipa mamlaka Idara ya Uhamiaji kuweza kushikilia au kuzuia kitu chochote ikiwa ni pamoja na nyaraka yoyote ambayo inaweza kuonyesha au kuthibitisha uvunjifu wa sheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, swali la nyongeza.

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kumekuwa na miradi mingi inayotekelezwa na Wakandarasi wa nje ya nchi na kupelekea miradi hiyo kutofanya vizuri na kupelekea Wakandarasi hao kukimbia nchini:-

Je, Serikali haioni haja sasa ya kuzuia hati zao za kusafiria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, samahani niliona ameshangiliwa sana, sikupata swali, naomba arudie tena.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, uliza tena swali lako Mheshimiwa Waziri hajasikia vizuri hapa mbele.

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa kumekuwa na wakandarasi wengi kutoka nje ambao wanatekeleza miradi yao nchini bila kutekeleza miradi hiyo kwa wakati; je, Serikali haioni haja sasa ya kuweza kudhibiti *passport* za Wakandarasi hao mpaka watakapomaliza miradi hiyo kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa maulid Saleh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la Wakandarasi kutokutekeleza miradi ni la kimikataba na pia linahusisha mamlaka nje zaidi ya Uhamiaji. Kwa hiyo, hatua za kudhibiti zinaweza kuwa nyingi kulingana na mkataba husika. Hata hivyo, kama nilivyoeleza katika jibu langu katika swali la msingi, kwamba pale ambapo Jeshi la Uhamiaji linahitajika kutumia sheria hii ambayo nimeiorodhesha hapa ambayo inaipa mamlaka kufanya hivyo kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa, kwa misingi ya sheria hii ambayo nimeizungumza, ikihitajika kufanyiwa hivyo; na imeshafanya hivyo mara kadhaa, lakini haiwezi ikatoka ikasema kila mradi ambao haujakamilika, basi twende tukakamate *passport* bila kufuata utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Matumizi ya TEHAMA Katika Kufundisha**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kueneza matumizi ya TEHAMA katika kufundisha ili kuwaokoa walimu na matatizo ya mgongo na shingo?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kuanzia mwaka 2019/2020, Serikali kupitia Programu ya Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu *(TESP)* imeendelea kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka 2021/2022 Serikali kupitia Programu ya Mafunzo Endelevu kwa Walimu Kazini (MEWAKA) imewezesha mafunzo kwa walimu wa Shule za Msingi 30,400 yanayohusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kugawa vishikwambi vilivyotumika katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi mwezi Agosti, 2022 kwa walimu wote nchini kwa lengo la kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA H. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nimwambie tu Mheshimiwa Waziri kwamba hivyo vishikwambi

ambavyo vimetumika kwenye sensa havitaweza kutosha kwa walimu wa nchi nzima kwa sababu waliokuwa wanahesabu sensa na idadi ya walimu ni tofauti kabisa. Sasa: Je, mna mpango gani wa kuhakikisha mnaongeza vifaa na kuweka *projector* kwenye kila shule ili kuondokana na suala la magonjwa na shingo na mgongo kwa walimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Mmetoa mafunzo kwa walimu ambao watakwenda kufundisha wanafunzi: Je, mmewaandaa namna gani hawa wanafunzi wanaokwenda kufundishwa kwa sababu somo hili litakuwa ni jipya kwao hasa kwenye maeneo ya vijijini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Subira Mwaifunga Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika majibu yangu ya msingi kwamba vishikwambi vilivyotumika katika zoezi la sensa ni zaidi ya 205,000 lakini sisi kama Wizara tumeongeza vishikwambi vingine zaidi ya 100,000. Kwa hiyo, nimwondoe hofu kwanza. Idadi ya vishikwambi ambavyo wizara imeweza kuratibu na kununua vitatosheleza kwa walimu wote.

Mheshimiwa Spika, niongezee hapo katika swali lake lingine ambalo anazungumzia habari ya kuwaandaa wanafunzi na vilevile kuandaa walimu. Serikali inaendelea na mchakato wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na vifaa toshelezi katika maeneo yote na hata katika bajeti yetu ya mwaka huu 2022/2023 tumeweka fungu kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, lakini tutaanza kwanza na kuimarisha vituo vile vya kufundishia walimu, zile *TRC* zetu.

Mheshimiwa Spika, vituo vile vyote 162 tayari tumevikarabati, tumenunua vifaa pamoja na *projector* katika vituo hivyo kwa kuhakikisha kwanza walimu tunaweza kwenda kuwafundisha wakiwa kule kule makazini pamoja na uwepo huu wa vishikwambi, itakuwa ni rahisi kuwafundisha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hiyo, Serikali ipo katika mpango wa kuandaa maktaba mtandao ambapo tunaamini maktaba hii itakapokamilika vitabu vyote vya kiada na ziada vitakuwepo kwenye maktaba hiyo na itakuwa ni rahisi kwa wanafunzi pamoja na walimu kupata mafunzo na mada mbalimbali kutoka kwenye maabara hizo. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kubwa kama ambavyo umeeleza za kuhakikisha inanunua vifaa vya TEHAMA nchini pamoja na kuwafundisha Walimu: Je, ni vipi jitihada hizi zinaunganishwa kuhakikisha kwamba tunaitumia TEHAMA kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa…

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, amekatika kidogo hapo katikati sikumpata vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ulenge moja kwa moja kwenye swali, Mheshimiwa hajasikia vizuri.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya jitihada kubwa za kununua vifaa vya TEHAMA nchini; je, ni vipi jitihada hizo zita…

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, subiri kwanza. Mwulize swali. Yale maelezo ameyasikia, yeye amesema hajasikia swali. Ukianza tena na maelezo, swali atakuwa hasikii tena.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni vipi jitihada hizo zinaunganishwa ili kuweza kutatua changamoto ya upungufu wa Walimu wa Masomo ya Sayansi nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali lake la msingi, Serikali bado inaendelea na jitihada ya kuzalisha walimu katika masomo ya sayansi nchini. Sambamba na hilo, kama nilivyozungumza ni kwamba tunaendelea na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na mahali tutakapoanzia ni kwenye vituo vyetu vya *TRC* na lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba vifaa vile tunaweza kwenda kuwafundisha walimu wetu.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la kuanzisha vituo hivi ni kuhakikisha kwamba tuna-*absorb* walimu wengi zaidi kuweza kuwafundisha katika maeneo hayo ili watakaporudi kule shuleni waweze kufundisha, kwa sababu siyo lazima walimu wa TEHAMA watokane na wale walimu wa sayansi tu.

Tukishawafundisha walimu wetu, hata wale walimu wa masomo ya kawaida bado wanaweza kutumika katika kufundisha somo hili la TEHAMA.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa swali la nyongeza. Tunaipongeza Wizara kwa jitihada yake inayofanya kwa ajili ya TEHAMA. Kwa wale wanafunzi wanaoona watapewa vishikwambi: Je, kwa wale wanafunzi wenye uono hafifu Serikali itawasaidiaje? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Mwinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada zake za kuhakikisha kwamba watoto wote wakiwemo na wale wenye uono hafifu na wenye ulemavu wa aina mbalimbali wanaweza kupata vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina takwimu sahihi za wanafunzi hawa na tutahakikisha nao vilevile katika eneo hili tunakwenda kuwapatia vifaa vya kuwasaidia na wao kuweza kujifunza somo hili muhimu la TEHAMA. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Majibu ya Waziri yameonesha Serikali ina mpango wa kuanzisha Maktaba Mtandao lakini kiuhalisia maeneo mengi nchini hakuna mtandao na umeme. Tunataka kujua ni nini mkakati wa Serikali kushirikiana na Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia kuhakikisha kwamba *program* hii inafika kwa wakati katika shule zetu zote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna changamoto ya mtandao maeneo mengi, lakini nimwondoe hofu kwamba Serikali yetu inaendelea na uimarishaji wa mtandao kwa kujenga mkongo wa Taifa. Nasi kama Wizara tayari tuna mradi mkubwa sana

ambao utahakikisha tunakwenda kuziunganisha shule zetu na mkongo huu na vilevile kuziunganisha kwenye mtandao wa *internet*.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utaanza na mikoa 10 katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 na tunaamini mpaka kufika mwaka 2025 basi utakuwa umefikia mikoa yote, lakini shule zote zitakuwa zimeunganishwa na mtandao wa *internet* kuhakikisha kwamba masomo haya ya TEHAMA yanakwenda kufanyika mpaka kule vijijini. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Ujenzi wa Barabara ya Zege Mlima Magara Mbulu Mjini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya zege ya kilometa tatu kwenye Mlima Magara katika Jimbo la Mbulu Mjini.

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo korofi na hatarishi katika Mlima Magara lina urefu wa kilometa saba. Kati ya hizo kilometa saba, Serikali imekamisha ujenzi kwa kiwango cha zege kilometa nne. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali itaendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege kwa kiasi cha kilometa moja. Kilometa mbili zilizobaki zitaendelea kujengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza; kwa kuwa tunaelekea robo ya pili ya mwaka wa fedha sasa na jiografia ya Mlima Magara ni ngumu sana utekelezaji wake wakati wa mvua; je, Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa hiyo kilometa moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Barabara ya Magara – Mbulu ina jiografia ngumu kuliko sehemu yoyote nchini na hizo kilometa 44 zilizobaki zimefanyiwa usanifu tayari kwa miaka mitatu. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mpango wake wa lami wa kilometa 44 katika barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuanzia Novemba mwaka huu barabara hii itakuwa imeanza kujengwa kwa kiwango cha zege kwa sababu taratibu zote za zabuni zimeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanza kujenga barabara yote, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kilichokuwa kimefanyika ulikuwa ni usanifu wa awali na atakubaliana nami kwamba wakati Makamu wa Rais anafungua Daraja la Magara mwezi Machi mwaka huu aliagiza barabara ile ikamilike na Juni mwaka huu ndiyo usanifu wa kina umekamilika. Kwa hiyo Serikali inaendelea kutafuta fedha ili ijenge kilometa hizi 44 kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kumekuwa na ucheleweshwaji mkubwa wa utoaji wa *tax exemption* kwa wakandarasi, sasa ni lini Wizara ya Ujenzi watakaa chini na Wizara ya Fedha ili waweke mfumo mzuri utakaorahisisha wakandarasi hawa kupewa *tax exemption* mapema ili waweze kujenga barabara mapema ikiwemo Barabara ya Bulyanhulu mpaka Kahama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maboresho mengi ya kuhakikisha kwamba malipo ya wakandarasi yanalipwa haraka na sasa hivi *TRA* hata mikoani wana uwezo wa kuchakata na kuharakisha malipo ya hawa wakandarasi. Hata hivyo, bado Serikali inaendelea kuboresha ili kuona

namna bora zaidi ya kukamilisha malipo haya ya wakandarasi kwa muda. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale, swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nauliza Serikali, je, ni lini itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Bigwa – Kisaki ya kilometa 78?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamisi Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Bigwa – Kisaki (kilometa 78) ilishapata kibali na taratibu za kukamilisha zabuni hizo ilitangazwa, lakini itatangazwa tena kwa ajili ya kupata mkandarasi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa kibali kilishatolewa, kwa hiyo ni taratibu tu za manunuzi ambazo zinaendelea ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali ina mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya kutoka Nangurukuru mpaka Liwale inayopitia katika Majimbo ya Kilwa Kusini, Kilwa Kaskazini pamoja na Jimbo la Liwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nangurukuru – Liwale ipo kwenye mpango kuijenga kwa kiwango cha lami na tayari usanifu ulishakamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo kwa kuwa usanifu umeshakamilika, Serikali ipewe nafasi na fedha ikipatikana barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Dongobesh – Dareda, ni lini itajengwa kwa kwiango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii imeshapata kibali kuanza kujengwa kwa awamu kwa kiwango cha lami kuanzia Dareda kwa kilometa zisizopungua nane. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tunaishukuru Serikali kwa kuendelea na ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Kidatu na hasa tunaishukuru Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* kwa usimamizi wa barabara hii. Je, Serikali ina mpango gani wa uwekaji wa taa za barabarani katika Barabara hii ya Ifakara – Kidatu kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoelekeza kwa zile barabara zinazopita katika vijiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru na kumpongeza kwa kutambua jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inaendelea kujengwa sasa hivi kwa kasi tofauti na ilivyokuwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa barabara zote zinazojengwa na hasa kwa kiwango cha lami, pale ambapo kuna miji mikubwa na midogo taa za barabarani zinatakiwa ziwekwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu huo upo na itakapokamilika basi awamu itakayofuata itakuwa ni kuweka taa za barabarani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza; ni lini Serikali itaanza upembuzi yakinifu wa Barabara kutoka Mfumbi – Matamba – Kitulo (kilometa 51) ili iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ni ahadi ya Serikali na ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni kama barabara ya uchumi ambako tunajua kunalimwa viazi vingi sana na mazao ya mbao. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina mpango wa kuanza kuifanyia usanifu barabara hii ili kupata thamani ama gharama ya hiyo barabara na baadaye Serikali itafute fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Imekuwepo Barabara ya Makondeko – Kwembe – Kisokwa ambayo imekuwa ndani ya bajeti katika kipindi cha miaka miwili mfululizo, 2021/2022 na 2022/2023. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mtemvu na atakubaliana nami kwamba tumefika kwenye jimbo lake. Barabara hii ni kati ya zile barabara ambazo zinapunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam na ipo katika mpango wa kuanza kuijenga kwa awamu hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Hoja ya Dharura.

**SPIKA:** Nani kasema Hoja ya Dharura?

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Bahati na Mheshimiwa Bonnah, naomba mkae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali yanayotoka kwenu kuelekea upande wa Serikali na Serikali kutoa majibu na sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele.

Ninalo tangazo la wageni ambao wapo Bungeni siku ya leo. Kwanza tunao wageni waliopo Jukwaa la Spika, hawa ni wageni 12 wa Bunge ambao ni Mabalozi wa *EU*. *(Makofi)*

Tutaanza na Mheshimiwa Manfredo Fanti ambaye ni – sasa hili tangazo limeandikwa Kiingereza, nafikiri walikuwa wanaogopa asije mtu asiyejua. Subiri nitakutangaza vizuri kwa sababu naona tangazo limemtaja cheo chake kwa Kiingereza kwa hiyo mniruhusu niendelee kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Manfredo Fanti, *Ambassador of EU Delegation to Tanzania;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Emilio Rossetti ambaye ni *Deputy Ambassador EU Delegation;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Mary O'Neill ambaye ni *Ambassador of Ireland;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Charlotte Ozaki Macias ambaye ni *Ambassador of Sweden;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Mette Norgaard Dissing Spandet ambaye ni *Ambassador of Denmark;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Marco Lombardi ambaye ni *Ambassador of Italy;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Wiebe De Boer ambaye ni *Ambassador of Netherlands;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Krzysztof Buzalski ambaye ni *Ambassador of Poland;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Nabil Hajlaoui ambaye ni *Ambassador of France;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Sari Uusi Rauva ambaye ni *Deputy Ambassador, Finland;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Petra Heylen ambaye ni *Deputy Ambassador, Belgium;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Kathrin Steinbrenner ambaye ni *Deputy Ambassador, Germany;* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Mariam Kilongo ambaye ni Afisa Mambo ya Nje, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; karibu sana. Yeye ameongozana na wageni wetu. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge ambao wako hapa Bungeni, wote wasimame kwa pamoja. Wageni wote wa Waheshimiwa wa Bunge wasimame kwa pamoja; karibu sana wageni wetu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao Walimu nane wa kidato cha sita kutoka Shule ya Sekondari Ziba waliofanikisha shule hiyo kuingia kumi bora Tanzania kwa mwaka 2022 kutoka Mkoa wa Tabora, Jimbo la Manonga; Walimu karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa ninyi muendelee kusimama kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, hii ni shule ya kata na imeingia kwenye kumi bora kwenye yale matokeo ya kidato cha sita. Kwa hiyo tunawapongeza sana Walimu wetu kwa kazi nzuri mliyoifanya na tunaamini mtaendelea kufanya hivyo kwa shule hii na kuzisaidia shule nyingine zilizo mkoani kwenu ili nao wafanye vizuri zaidi. Tunatamani watoto wetu wote wafanye vizuri na tunawatakia kila la heri katika majukumu yenu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 100 kutoka *Tanzania Red Cross* ambao ni wakufunzi wa huduma ya kwanza kutoka mikoa yote ya Tanzania wakiwa pamoja na viongozi na *volunteers* wa *Red Cross;* karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mnafahamu kwamba safari hii Rais wa *Red Cross Tanzania* yuko humu Bungeni, Mheshimiwa David Kihenzile; karibu sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa tangazo lingine. Mnatangaziwa kuwa Siku ya Jumamosi, tarehe 17, Septemba, 2022, kutakuwa na Bonanza la Michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *NMB* litakalofanyika katika Viwanja vya *Chinangali Park* ambapo michezo itakayoshindaniwa ni kama ifuatavyo: -

Kwanza ni mpira wa kikapu wanaume na wanawake, mpira wa pete, mpira wa wavu wanaume na wanawake, mchezo wa kuvuta kamba wanaume na wanawake, mchezo wa kukimbiza kuku wanaume na wanawake na mpira wa miguu. *(Makofi)*

Michezo hiyo itatanguliwa na matembezi yatakayoanzia maeneo ya Bunge saa 12 asubuhi na kuishia katika viwanja vya *Chinagali Park* ambapo michezo mingi itafanyika muda wa asubuhi na mchezo wa mpira wa miguu utafanyika kuanzia saa tisa alasiri katika viwanja vya Kilimani *Club*.

Aidha, mara baada ya michezo hiyo Wabunge wote mnakaribishwa kwenye mchapalo utakaofanyika katika Viwanja vya Chinangali kuanzia saa moja jioni, na mgeni rasmi katika Bonanza hilo na wakati wa mchapalo atakuwa Spika wa Bunge. Karibu sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Pia Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote mnakaribishwa kushiriki kikamilifu. Kama mlivyoambiwa kuna michezo mingine itaongezeka hapa, kwa hiyo wewe Mbunge mchezo unaoumudu utatuambia ni upi, *NMB* hawana neno. Tutawaambia Mbunge huyo anamudu huu kwa hiyo ninyi leteni wa kwenu ili ashindane naye. Kwa hiyo karibu sana.

Mwaka jana tulipata fursa ya kushiriki hili bonanza na wale walioshiriki waliona, hakuna masharti ya matumizi ya vinavyokuwepo pale kuhusu michezo. Kwa hiyo karibu sana kwenye hili Bonanza la *NMB* tuje tutoe ushirikiano.

Waheshimiwa Wabunge, wakati nikisimama hapa walisimama Wabunge wawili ikiashiria kwamba wana mambo, mmoja alisema mwongozo, mwingine alisema jambo la dharura, sasa jambo la dharura; Mheshimiwa Bahati Ndingo.

## JAMBO LA DHARURA

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimesimama kuomba Bunge lako Tukufu liahirishwe kwa muda tujadili jambo la dharura kwa Kanuni namba 54, ni suala zima la usalama wa raia wetu.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kupata taarifa na kuona taarifa mbalimbali, jana Mkoa wa Dar es Salaam kuhusiana na panya *road*. Wanaendelea na uvamizi kwenye makazi ya watu na barabarani, lakini jana wamesababisha mauti ya raia huko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, vikundi kama hivi vimeendelea kuenea nchini, kikundi kama hicho Mkoani Mara wanajiita Watukazi na kwenyewe kunaendelea na matukio hayo. Jimboni kwa Mheshimiwa Chaya pia Mheshimiwa Diwani amevamiwa. Kwa hiyo ni matukio ambayo yanaendelea kwa kasi. Hata hapa Dodoma baadhi ya Waheshimiwa Wabunge tayari wameshavamiwa na vikundi mbalimbali vya vijana hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la dharura. Naomba kwa unyeti wake Bunge liahirishwe kwa muda tuweze kulijadili hapa Bungeni kuishauri Serikali, naomba kutoa hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kaeni kwanza. Kanuni zinataka nikishajiridhisha ndiyo nimpe fursa atoe maelezo yake halafu ndiyo nijue kama hiyo hoja inaingia kwenye dharura au hapana, lazima nijiridhishe. Kwa hiyo haya ni maelezo yake ya awali, hoja atatoa baadaye ambayo ndiyo itabidi muunge mkono. Nadhani imeeleweka siyo?

Haya, kabla sijatoa uamuzi kuhusu hili, nimsikilize Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 54(1). Naomba ridhaa yako kuahirishwa kwa Bunge ili tuweze kujadili suala ambalo linaendelea katika mikoa mbalimbali ambalo linahusiana na mambo ya usalama na vikundi maarufu kwa jina la panya *road* ambalo linaendelea sana sana Mkoa wa Dar es Salaam ili tuweze kulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ridhaa yako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wamesimama Wabunge wawili hapa, kwanza alisimama Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo kwa Mujibu wa Kanuni ya 54 akitaka Bunge liahirishwe kwa muda ili tuweze kujadili jambo ambalo yeye ameona ni la dharura na ametoa maelezo yake hapa kwa kirefu, ameeleza kuhusu jambo hilo linasimama kwenye hoja ya usalama wa raia. Ameeleza sasa sehemu ya pili kwamba inasimama pia kwenye usalama wa raia lakini la pili ni usalama wa mali zao.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 54 inatoa fursa kwa Mbunge kusimama na kueleza yale maelezo ya awali halafu iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo linatimiza masharti yaliyowekwa katika Kanuni ya 55 basi Spika atampa fursa huyo mwenye hoja ili atoe maelezo kwa kirefu halafu atatoa hoja hiyo ili Bunge liendelee kujadili.

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili kwa masharti ya Kanuni ya 55 ni jambo ambalo sisi kama Bunge ni dhahiri tungeweza kulijadili lakini kwa namna lilivyo na kwa namna Kanuni yetu ya 55 ilivyoweka masharti, hili ni moja ya mambo ambayo linaangukia katika Kifungu Kidogo cha (3) cha Kanuni ya 55 na kwa hivyo, ukisoma pia masharti hayo hayo ya Kanuni ya 55 Fasili ya (1) na (2), hili ni jambo ambalo linapaswa kushughulikiwa na Serikali katika utaratibu wa kawaida. Maana yake kwa ujumla kuhusu hoja hiyo ni kwamba sintaitoa ijadiliwe na Bunge kwa sababu ya masharti ambayo tumeyaweka sisi wenyewe kwenye Kanuni ya 55. Kwa hivyo, litashughulikiwa na Serikali kwa utaratibu wa kawaida. Lakini kwa sababu Mheshimiwa Bahati

namna alivyolieleza jambo hili, namna ambavyo limeshaathiri maisha ya mtu ama watu, limeshaathiri mali za watu na jana tulizungumza pia hapa athari zinakwenda mbali zaidi ya hapo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa pamoja na kwamba Kanuni inasema Serikali itashughulikia katika utaratibu wa kawaida, utaratibu huu wa kawaida siyo kwamba utachukua kama yale mambo mengine yote inavyokuwa Hapana! Ni kwamba tunaipa fursa Serikali ilishughulikie jambo hili kwa haraka. Kanuni inavyosema utaratibu wa kawaida ni kwamba utaratibu wa kawaida kwa maana ya Sheria ile ambayo inashughulika na mambo haya inatoa fursa ya Serikali kuchukua hatua. Serikali inayo huo uwezo wa kuchukua hatua, tulishapata hizo changamoto nchi hii na Serikali ilifanyakazi na hayo mambo yakaisha kabisa. Tunaamini hata hili mnao uwezo wa kulimaliza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo nimesema kwa mazingira ya Kanuni ya 55 na jambo lenyewe namna lilivyoletwa masharti haya yanataka nielekeze Serikali kuchukua utaratibu wa kawaida mlifanyie kazi jambo hili kwa haraka. Kwa sababu zile athari siyo tu kwa sababu na Wabunge wameathirika, maana Wabunge wameathirika mali zao lakini hata na siyo kwa maana ya maisha lakini kimsingi hata maisha yangeweza kuchukuliwa kwa sababu wapo walioumizwa na matukio haya. Lakini siyo kwa sababu ni ya Wabunge, ni kwa sababu hata huko nje wananchi wanapata athari. Kwa hiyo, Serikali ichukue hatua za haraka kushughulikia jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, nimezungumza hivyo kwa jumla kwa sababu Mheshimiwa Bahati alisema jambo hili na Mheshimiwa Bonnah Kamoli pia amesimama kwa jambo hili, kwa hiyo siyo mambo mawili tofauti na kwa hivyo yote hayajakidhi masharti ya Kanuni yetu ya 55 na kwa hivyo Serikali naiagiza ichukukue utaratibu wake wa kawaida, kwa sababu bado tupo hapa tunaamini kwamba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu yupo hapa mtalichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili na kuchukua hatua zile ambazo tunazitarajia kutoka kwenu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nimpishe Mwenyekiti aendelee na ratiba nami nikaendelee na ratiba nyingine ya kuonana na hao wageni wetu wazito hapo juu. Ahsante sana. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

## (Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *(The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022)*

*(Kusoma Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninamuita sasa Waziri wa Maji kuwasilisha Muswada kwa dakika 30, karibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *(The Water Resources Management (Amendment) Act, 2022)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa Mara ya Pili na ya Tatu na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimae lipitishe Muswada huu kuwa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema hivyo kuweza kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wa Tanzania. Pia nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani kidogo, Waheshimiwa naomba tutulie tumsikilize Mheshimiwa Waziri wa Maji. Naomba sana tutulie.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema hivyo kuweza kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wa Tanzania. Pia, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutoa fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji hapa nchini. Sote tunambua ukweli kuwa "Maji ni Uhai" na vilevile ni kichocheo kikubwa katika shughuli za kijamii na maendeleo. Hivyo, nimepewa dhamana kubwa ambayo sina budi kuisimamia kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usaidizi wake uliotukuka kwa Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha utekelezaji wa Ilani ya CCM ambayo ni nyenzo muhimu sana katika kuweka mikakati ya kuhakikisha utunzaji wa rasilimali za maji na upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo stahiki ambayo amekuwa akinipatia katika uketelezaji wa majukumu yangu kama Waziri wa Maji, hivyo kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Dkt. Christine Ishengoma (Mbunge)na Mwenyekiti wa Kamati yetu pamoja wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuchambua na kupitia kwa kina Muswada huu. Maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao ya kuboresha muswada huu. Wadau hao ni pamoja na Wizara za Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali, watumiaji wa maji, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa hatua zote za maandalizi na hatimaye kukamilisha muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la muswada ni kuufanyia marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331 kwa lengo la kuondoa upungufu uliodhihirika wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maelezo kuhusu mpangilio wa muswada, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu Sheria za Maji zinazotumika sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kuwa hutumika majumbani, kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji umeme, utalii na mazingira. Ni kutokana na umuhimu huo mfumo na muundo wa usimamizi umetungiwa Sheria mahususi ambayo leo nawasilisha ili kuomba mabadiliko katika baadhi ya maeneo kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maji imegawanyika katika maeneo makuu muhimu ambayo ni usimamizi wa rasilimali za maji, utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira na udhibiti wa utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira. Kwa upande wa usimamizi wa rasilimali za maji, sheria inayoongoza utekelezaji wa majukumu hayo ni Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya 2009, kwa upande utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira ni Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Namba 5 ya mwaka 2019.

Vilevile, utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira, unadhibitiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Namba 11 ya mwaka 2001. Katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa

Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009, zipo changamoto zilizojitokeza katika masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331. Marekebisho hayo yanalenga kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi katika kusimamia Rasilimali za Maji ili kuendana na mabadiliko yaliyofanyika katika sekta ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba sasa kutoa muhtasari wa masuala yaliyomo katika Muswada huu ambao umegawanyika katika sehemu Mbili. Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi. Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho ya ujumla kwa kufuta maneno "*Basin Water Officer*" popote yatapojitokeza katika Sheria na badala yake kuweka maneno "*Basin Water Director*". Madhumuni ya marekebisho haya ni kuakisi cheo sahihi cha Wakuu na Maafisa Masuuli wa Bodi za Mabonde ya Maji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 3 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya neno "Mahakama" inayojumuisha Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Mahakama Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuweka bayana katika Sheria Mahakama zitakazokuwa na mamlaka ya kushughulikia makosa yanayotendwa chini ya sheria hii. Hatua hii itasaidia kuondoa utata wa kimamlaka na kusogeza huduma ya Mahakama maeneo yote kwa kujumuisha Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho yanayopendekezwa katika Kifungu cha 8 yanalenga kuzingatia masharti ya Kifungu cha 104 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 kinachoelekeza kuwa tathmini ya mazingira kimkakati ifanyike kuhusu Miswada, Kanuni, Sera, Mikakati, Programu na Mipango. Hivyo, inapendekezwa kufuta maneno "*a major water project is planned*" na badala yake kuweka maneno "*water programmes and development plans are prepared*". Lengo la Marekebisho haya ni kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa katika kipengele (b) kwa lengo la kuondoa maneno yanayoainisha jukumu la Bodi ya Maji ya Taifa la kuishauri kuhusu vipaumbele vya uwekezaji na upatikanaji wa fedha ambayo yapo pia kwenye kipengele (f). Hivyo, marekebisho yanafanyika ili kutengeneza majukumu yaliyoelekezwa kwenye kipengele (b) na (f) na kuondoa marudio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 23 kinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuzipa Bodi za Mabonde ya Maji jukumu la kutoa elimu kwa wadau kuhusu hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa katika usimamizi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 24 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza Kifungu Kidogo cha (2) ili kuainisha sifa za uteuzi wa Mkurugenzi wa Bonde la Maji. Kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongezwa Kifungu Kidogo cha (4) ili kubainisha kosa la kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ambayo yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu *(protected zones)* ya vyanzo vya maji. Marekebisho hayo yanalenga kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji dhidi ya uchafuzi, mmomonyoko wa udongo na athari hasi zinazoweza kutokea kutokana na uvamizi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 43(1) kinapendekezwa kurekebishwa ili kujumuishwa suala la kuzuia maji "*impoundment of Water*" kwenye mkondo kama moja ya suala ambalo linahitaji kuombewa kibali. Marekebisho hayo yanalenga kudhibiti vitendo vya kuzuia maji kwenye mkondo bila kuwa na kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 44 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kwa madhumuni ya kutenganisha kosa la matumizi ya maji kinyume na kibali na kosa la matumizi ya maji bila kibali. Kifungu cha 44A kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha kosa la matumizi ya maji bila kuwa na kibali. Lengo la marekebisho haya ni kutenganisha kosa la matumizi ya maji kinyume na kibali na kosa la matumizi ya maji bila kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 56 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza mwishoni mwa Kifungu Kidogo cha (2) maneno "*in a particular aquifer*" ili kuweka takwa la kuzingatia hali ya mwamba "*geological formation*" katika kuainisha umbali kati ya kisima na kisima. Kifungu cha 65 kinapendekezwa kurekebishwa ili kumpa mamlaka Waziri ya kuunda maabara za ubora za maji zitakazo kuwa na jukumu la kusimamia uchunguzi na uhakiki wa ubora wa maji kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191. Lengo la marekebisho haya ni kutambua maabara hizo kisheria na kuzipa ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 75 kinapendekezwa kurekebishwa katika Kifungu Kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "*right*" na badala yake kuweka maneno "*permit*". Marekebisho haya yanalenga kuweka bayana kuwa vibali vinavyotolewa na Bodi ya Bonde la Maji ni "*water permit*" na siyo "*water right*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 79 kinapendekezwa kuongeza Kifungu Kidogo cha (2) kwa kufuta maneno "*National Water Board*" na badala yake kuweka maneno "*Director of Water Resources*" lengo la marekebisho haya ni kubainisha kuwa jukumu la kupokea taarifa za daftari la maji kutoka Bodi za Mabonde ya Maji ni la Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 88 kinapendekezwa kuongeza Kifungu Kidogo cha (7) ili kuweka masharti kwa wamiliki wa mabwawa kulipa gharama za uhakiki wa eneo na mapitio ya ripoti ya usanifu wa mabwawa kama itakavyoainishwa katika Kanuni. Kifungu cha 97A kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha utaratibu wa "*summary procedure*" ambao Bodi za Mabonde ya Maji zitatumia katika kudai au kufuatilia maduhuli kwa wadaiwa. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka gharama kubwa za kugharamia kesi za madai kwa kufuata utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendekezwa kuongezwa Kifungu kipya cha 105A ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu zake hazijawekwa bayana katika vifungu husika. Lengo la marekebisho haya ni kuepuka uwezekano wa kutotoa adhabu kwa mtu ambaye amethibitishwa kutenda kosa chini ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 107 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza maneno "*without prejudice to provisions of section 105*" mwanzoni mwa Kifungu kwa lengo la kuepuka utata wa fidia zilizotajwa kwenye Kifungu cha 105 kutokana na vitendo vya kijinai na fidia zilizotajwa kwenye Kifungu cha 107 kutokana na utekelezaji wa majukumu ya Bodi za Mabonde ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 111 kinapendekezwa kurekebishwa katika Kifungu Kidogo cha (2) kwa kuongeza aya mpya ya (k) ili kumpa mamlaka Waziri kutengeneza Kanuni zitakazo bainisha utaratibu wa kuhamisha maji kutoka bonde moja kwenda bonde lingine. Lengo ni kuweka utaratibu wa kuhamisha maji kutoka bonde moja kwenda bonde lingine ili kukabiliana na upungufu wa maji katika baadhi ya mabonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali la Tatu linapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuipa mamlaka Bodi ya Bonde la Maji jukumu la kuteua wajumbe wa Kamati za Vidaka Maji *(Catchment Water Committee*) kwa mujibu wa Sheria. Vilevile, Jedwali hilo linapendekezwa kurekebishwa ili kufuta maneno "*Minister*" na badala yake kuweka maneno "*Basin Water Board*". Marekebisho haya yanalenga kuipa Bodi ya Bonde la Maji mamlaka ya nidhamu kwa Kamati za Vidaka Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jedwali la Nne linapendekezwa kurekebishwa ili kuongeza maneno "*and at least two members shall be women*". Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa kuna uwiano wa

kijinsia katika uwakilishi kwenye usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya Jumuiya za Watumiaji Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufikia hatua hii, mchakato umehusisha wadau wengi ikiwa ni pamoja na Wizara za Serikali, Bodi ya Taifa ya Maji, Bodi za Mabonde ya Maji, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, jumuiya za watumiaji wa maji, asasi zisizo za serikali na washirika wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nichukue fursa hii tena kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kupitia kwa undani Muswada ulio mbele ya Bunge lako Tukufu. Matokeo ya uchambuzi wao wa kina ni Jedwali la Marekebisho kama lilivyosambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge. Aidha, ushauri na maelekezo ya Kamati yatazingatiwa kikamilifu katika utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, kwa heshima kubwa naomba Waheshimiwa Wabunge wajadili Muswada huu na kuridhia na hatimaye kuupitisha kuwa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2022 *(The Water Resources Management (Amendment) Act, 2022)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA.** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwa Heshimu abnaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Waziri wa Maji na hoja yako imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ili aweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria wa Usimamizi wa Rasilimali ya Maji wa Mwaka 2022. Mheshimiwa Christine Ishengoma, karibu.

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji *(The Water Resources Management Amendment)*, *Bill*, 2022. Muswada huu wenye jumla ya Ibara 22 ulisomwa mara ya Kwanza tarehe 23 Juni, 2022 katika Kikao cha Hamsini cha Mkutano wa Saba wa Bunge. Baada ya hatua hiyo, Muswada huo ulipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hiyo inaitaka Kamati inayohusika kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo. Kwa kuthamini imani yako kwa Kamati hii na kwa kutambua masharti hayo ya Kanuni za Bunge, mapema wakati wa vikao vya Kamati za Bunge vilivyoanza tarehe 29 Agosti, 2022, Kamati ilianza kuufanyia kazi Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maelezo ya jumla. Taarifa hii inalijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu pamoja na matokeo ya uchambuzi. Taarifa inajumuisha Maoni na Ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kama inavyoonekana katika Taarifa iliyowekwa mezani mapema leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia/mbinu zilizotumika. Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020 imeweka msingi unaotaka taarifa ya Kamati ioneshe namna jambo linaloripotiwa lilivyofanyiwa kazi. Aidha, ili kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti na ustahiki naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu. Njia zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu zimechangia kufanikisha uchambuzi na hatimaye maandalizi ya taarifa hii. Kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 naomba kuzitaja njia zilizotumika na madhumuni ya kila moja kama ifuatavyo: -

(a) Kupokea maelezo ya mtoa hoja kuhusu mapendekezo yake ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji lengo ni kupata mantiki ya marekebisho yanayopendekezwa,

(b) Kufanya mapitio ya maudhui ya Muswada na kubaini mambo yanayopendekezwa kurekebishwa katika mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji,

(c) Kuoanisha mapendekezo ya Muswada wa sheria inayojadiliwa na miongozo mingine katika shughuli za umma chini ya sekta hii,

(d) Kujadili dhana kuu ya sekta ya maji inayoguswa na mapendekezo ya kurekebisha sheria ya usimamizi wa rasilimali za maji,

(e) Kupokea na kusikiliza maoni ya wadau kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 97(2) pamoja na masharti ya Kanuni ya 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali kuuelewa Muswada huu. Naomba kubainisha mbinu hizo kwa kutaja zifuatazo: -

(a) Kubaini nia ya mapendekezo kwa kusoma Jina Refu la Muswada na Sheria inayopendekezwa kurekebishwa, pamoja na kupitia maelezo ya sababu na madhumuni ya Muswada huu,

(b) Kupambanua mambo makuu yanayorekebishwa katika mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi wa rasilimali za maji,

(c) Kuoanisha nia, mambo yanayopendekezwa kurekebishwa, Sera na Sheria zilizopo pamoja na ahadi iliyotolewa kwa wananchi katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, na

(d) Kupima mapendekezo ya marekebisho ya usimamizi wa rasilimali za maji katika muono mpana wa Afrika na dunia kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitumia njia na mbinu zilizobainishwa, ambazo uwezo wake umetoa manufaa ya uchambuzi unaoliwezesha Bunge kukidhi matarajio ya wananchi. Nikiri kuwa njia na mbinu hizo zimeiwezesha Kamati kupata undani wa marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Muswada. Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, ulifanyiwa uchambuzi kwa kuhakiki na kupembua maudhui, masharti, mpangilio na dhamira kwa ujumla. Uchambuzi huo ulijumuisha mapitio ya jumla ya maudhui na baadaye upembuzi wa Ibara za Muswada huo ili

kupata picha halisi ya maudhui na msingi wa masharti ya Sheria inayopendekezwa. Lengo ni kujiridhisha na masuala makuu manne ya kiuchambuzi, ambayo ni: -

(a) Iwapo kuna mahitaji ya sheria inayopendekezwa;

(b) Iwapo pendekezo katika Muswada huu linaendana na ahadi na mwelekeo wa jumla wa nchi, kanda na dunia;

(c) Iwapo pendekezo linakidhi haja ya sheria inayobainishwa; na

(d) Iwapo misingi ya utungaji wa sheria imezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo hayo, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika sehemu mbili. Sehemu hizo ni: Upembuzi wa Maudhui ya Muswada wa Sheria na Uchambuzi wa Ibara za Muswada ikilinganishwa na vifungu vya Sheria inayorekebishwa kwenye madhumuni ya kupembua maudhui ya Muswada huu ni kubaini uthabiti wa marekebisho yanayopendekezwa ili kuishauri Bunge inavyostahili. Kwa ujumla utaratibu wa Kibunge wa hoja huwasilishwa, huungwa mkono, hujadiliwa na kuamuliwa unahitaji misingi inayofanikisha uhakiki na upembuzi wa kina wa hoja inayojadiliwa. Kwa sababu hiyo, Kamati imefanya mapitio ya kimaudhui ya Muswada huu ili kulibainishia Bunge mambo yatakayoisaidia kuamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya jumla yanaonesha kuwa dhana kuu katika sheria inayopendekezwa kurekebishwa ni usimamizi wa rasilimali za maji. Usimamizi wa rasilimali za maji ni mchakato wa kupanga, kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji. Dhana hii inajumuisha taasisi, miundombinu, taratibu na michakato ya utumiaji, uhifadhi na udhibiti wa matumizi ya rasilimali za maji. Kwa maana hiyo, Muswada huu unahusu marekebisho ya Sheria inayohusu utaratibu, mamlaka, wajibu, majukumu, haki na masharti mbalimbali kuhusu uhifadhi, usimamizi, na udhibiti wa matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la dhana hii katika suala la rasilimali za maji ni hali halisi ilivyo duniani, Afrika na Tanzania. Ni dhahiri kwamba idadi ya watu, maendeleo ya shughuli za binadamu, mahitaji ya maji na ulazima wa kuzingatia uendelevu wa mazingira ya vyanzo vya maji ni miongoni mwa mambo yanayosukuma dhana ya usimamizi wa rasilimali za maji. Kwa msingi huo, mapendekezo yoyote ya sheria katika sekta ya maji yanapaswa kuzingatiwa kwa muono wa dhana ya usimamizi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa huo uliisukuma Kamati kuchanganua mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Matokeo ya kufanya hivyo, yamebainisha mambo mbalimbali yanayoguswa na Muswada huu. Naomba kulibainishia Bunge kwa kutaja baadhi ya mambo hayo na kuyaeleza kwa kifupi kama ifuatavyo: -

(a) Cheo cha Ofisa Bonde la Maji (*Water Basin Officer*) kinabadilishwa kuwa Mkurugenzi wa Bonde la Maji. Itambulike kuwa kwa sasa uendeshaji wa sekta ya maji unahitaji maofisa hao waendelee kuwa na mamlaka na madaraka yanayoendana na cheo kinachopendekezwa kwenye Sheria;

(b) Tafsiri ya neno mahakama *(court)* inaongezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Bila kufanya hivyo, sheria itaendelea kuacha utata ambao si jambo la kuendelea nalo. Utata huo katika kushughulikia makosa yanayohusu ukiukaji wa masharti ya usimamizi wa rasilimali za maji unahitaji kutatuliwa na mfumo wa kisheria;

(c) Wigo wa masharti ya miradi ya maji kufanyiwa tathmini ya kimkakati ya athari ya mazingira unaongezwa. Ongezeko hilo ni jambo linalopaswa kuzingatiwa inavyostahili;

(d) Ufafanuzi wa majukumu ya Bodi ya kushauri kuhusu uratibu wa uainishaji wa vipaumbele katika uwekezaji wa fedha kwenye masuala ya rasilimali za maji unawekwa bayana zaidi. Jambo hilo linahitaji kupimwa inavyostahili;

(e) Wadau wanawezeshwa zaidi kupata taarifa kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika usimamizi wa rasilimali za maji. Lengo la kuwashirikisha wadau katika uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za maji linapaswa kuangaliwa kama limewekewa masharti stahiki;

(f) Adhabu kwa kosa la ufanyaji wa shughuli za kibinadamu kwenye maeneo tengefu inabainishiwa msingi katika Sheria.

(g) Uzuiaji wa maji kwenye mkondo wake unawekewa masharti ili kusimamia na kudhibiti jambo hilo.

(h) Usimamizi wa uchunguzi na uhakiki wa ubora wa maji kwa kumruhusu Waziri anayehusika kuunda maabara za ubora unawekewa masharti katika Sheria.

(i) Changamoto ya gharama za usajili wa mabwawa na haja ya kuongeza kazi ya usajili wa mabwawa yenye usalama inawekewa misingi ya kutatuliwa. Dhamana ya Bunge kwa mahitaji ya wananchi kuhusu usajili wa mabwawa ya maji inapaswa kuwa kigezo cha uchambuzi; na

(j) Masharti yanayohakikisha kuwa kuna uwiano stahiki wa kijinsia katika usimamizi wa rasilimali za maji yanaongezwa na kuimarishwa

katika Sheria. Bunge linapaswa kujiridhisha na masharti hayo muhimu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo yanayopendekezwa katika mfumo wa kitaasisi na kisheria wa usimamizi wa rasilimali za maji, yanaweza kuhakikiwa kwa kufanya mapitio ya machapisho na miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za umma nchini. Lengo ni kuzingatia mtazamo mpana kuhusu marekebisho yanayopendekezwa pamoja na kuoanisha mambo hayo na mwelekeo wa nchi kwa muktadha wa matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo wa Kamati wakati wa uchambuzi ulilengwa kwenye Sera ya Maji ya Mwaka 2002, ahadi waliyopewa wananchi katika Ilani ya CCM ya mwaka 2020, bila kuacha mwelekeo uliobainishwa katika Dira ya Taifa ya 2025. Kwa faida ya mjadala kuhusu hoja iliyo mbele ya Bunge naomba kutoa muhtasari wa matokeo ya mapitio kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mtazamo wa jumla kuhusu usimamizi wa Rasilimali za Maji unajengeka kwa mapitio ya machapisho mbalimbali ikiwemo taarifa za Kimataifa na Kikanda. Kamati ilijiridhisha kwa kuzingatia Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo ya Sekta ya Maji na Dira ya Afrika kuhusu Maji. Ripoti hii inatambulisha dunia haja ya kuboresha usimamizi wa rasilimali za maji na pia imesisitiza mambo matatu kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji. Mambo hayo yaliyosisitizwa ni kutambua, kupima na kuendeleza rasilimali za maji pamoja na kufungamanisha mambo hayo katika michakato mbalimbali ya uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti hiyo, kufanya hivyo ni muhimu ili kufanikisha ufuatiliaji wa usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na kufanikisha malengo endelevu. Mtazamo huo ulizingatiwa katika uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Kwa mfano, katika uchambuzi wa Ibara kwa Ibara, Kamati ilibaini kwamba, Ibara ya 8 inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kidogo cha (4) katika Kifungu cha 37 cha Sheria Mama kwa lengo la kubainisha kosa la kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ambayo yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Kamati ilizingatia Dira ya Maji Afrika kwa mwaka 2025 ambayo inajenga msingi wa mipango ya muda mrefu kuhusu maji katika Kanda ya Afrika na Jumuiya ya Kikanda ndani ya Afrika. Kwa ujumla Dira hiyo inahimiza utawala bora katika usimamizi wa Rasilimali za Maji na kujenga uwezo wa kukusanya na kutoa taarifa kuhusu rasilimali za maji. Dira ya Maji ya Afrika inatambua kwamba Bara hili limebeba vyanzo vingi vya maji na kwamba linakabiliwa na upotevu mkubwa wa maji ya mvua. Dira hiyo imefafanua zaidi kuwa uhaba wa maji katika baadhi ya nchi

unatokana na kutolinganishwa kwa suala la rasilimali za maji zilizopo na mahitaji ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali za maji zinahitaji kulindwa na kuhifadhiwa ili ziwe za kudumu na endelevu, lakini pia zinapaswa kutumika ili kukidhi mahitaji ya maji yanayoongezeka. Uhusiano huo umelinganisha suala la usimamizi wa rasilimali za maji katika dhana ya usalama wa maji wa Taifa. Dhana ya Usalama wa Maji imetafsiriwa na Kikosi cha Usalama wa Maji cha Umoja wa Matiafa. Fasiri hiyo ilielezwa kama ifuatavyo: -

> "*Water Security is the Capacity of a population of safeguard sustainable access to adequate quantities of and acceptable qualities of water for sustaining livelihoods, human well - beings, and socio-economic development for ensuring protection against waterborne pollution and water related disasters and for preserving ecosystems in a climate of peace and political sustainability*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji unaokidhi mahitaji ya umma ni ule unaotengenezwa kwa sheria zinazosaidia usalama wa maji. Suala kubwa kutokana na ukweli huo ni kuona iwapo marekebisho ya Sheria yanayopendekezwa yatasaidia kuboresha usalama wa maji. Miongoni mwa viashiria muhimu vya kuzingatiwa kwa dhana ya usalama wa maji, ni masharti ya sheria inayopendekezwa kuongeza uhakika endelevu wa maji kwa kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maji. Aidha, uzingatiaji wa ruhusa ya matumizi ya maji kwa uhai wa binadamu ni suala lingine lililopewa uzito wakati wa uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Ibara ya 4 ya Muswada huu ya kufuta maneno "*a major water Project is planned*" na kuweka maneno "*Water Programmes and development plans are prepared*", yanaendana na dhana ya usalama wa maji. Mwendano huo unatokana na mambo makubwa mawili ambayo ni: -

(a) Kutaka uendelevu wa kuzingatia tathmini ya mazingira kwenye miradi yote ya maji; na

(b) Kuweka dhana zinazoogofya ili kuendelea kuzilinda rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Miongozo. Kamati ilichambua Muswada huu kwa muktadha wa ahadi walizopewa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Sababu ya kufanya hivyo ni kupima kama matarajio ya wananchi yanazingatiwa katika Muswada huu. Kamati ilibaini kwamba, Chama Cha Mapinduzi kinachoongoza Serikali, kiliwaahidi

wananchi kuwa Serikali itasimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali, Kamati iliona umuhimu wa kuoanisha mapendekezo yanayotolewa kwa upande mmoja na mtazamo wa nchi kisera kwa upande mwingine. Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 yalisaidia kuhakiki maudhui ya Muswada wa Sheria unaojadiliwa na Bunge lako Tukufu leo. Ili kuweka mtazamo wa Kamati kuhusu Muswada huu, katika muktadha stahiki, naomba kulibainishia Bunge kuhusu sera inayorejewa. Sera hiyo imegawanyika katika sehemu kuu tatu:-

(a) Menejimenti ya rasilimali za maji;
(b) Utoaji wa huduma za maji vijijini; na
(c) Utoaji wa huduma za maji safi na maji taka mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya hoja hii inayojadiliwa na Bunge kwa sasa, Kamati ilijielekeza kwenye sehemu ya sera inayohusu Menejimenti ya Rasilimali za Maji kwa kuwa ndiyo inayohusika katika marekebisho ya sheria inayopendekezwa. Lengo kuu la Sera hii ni kuendeleza mifumo kamilifu kwa ajili ya maendeleo na Menejimenti ya Rasilimali za Maji. Mifumo hiyo inakusudiwa kuwa endelevu na shirikishi kwa wanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa azma ya Sera hii inatiliwa nguvu za kisheria katika mapendekezo ya Serikali. Jambo hili linadhihiri katika maudhui ya Muswada ikilinganishwa na sheria inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Muswada ibara kwa ibara ulifanyika kwa kusoma kila sentensi na kila neno katika Muswada. Utaratibu huo unazingatia ushauri aliowahi kuutoa Mwandishi Mtaalamu wa Sheria, John Aneurin Grey wa Chuo Kikuu cha Wales kwa kusema:- *"The function of a committee on a bill, says Erskine May, is to go through the text of the Bill clause by clause and, if necessary, to making such amendments in it as may seem generally acceptable"*. Kwa tafsiri ya Kiswaili kisicho rasmi tunaweza kusema: "Kazi ya Kamati inayoshughulikia Muswada, anasema Erskine May, ni kupitia matini *(text)* ya Muswada ibara kwa ibara na, ikilazimika neno kwa neno kwa mtazamo wa kufanya marekebisho ambayo yanaweza kuwa ya kukubalika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo, Kamati ilipitia Muswada wote kuanzia namba ya utambuzi wa chapisho la Muswada, namba ya Muswada, namba ya toleo la Gazeti la Serikali lililoutangaza Muswada, tarehe, mpangilio, sababu na madhumuni hadi jina na saini ya mdhamini wa

hoja. Lengo la kufanya hivyo ni kujiridhisha na masharti yote ya utungaji wa sheria na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kulishauri Bunge inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi Kamati, ilitambua kazi kuu ya kuzingatia mapendekezo kwa kutathmini maelezo ya mtoa hoja, mapendekezo ya wadau na maoni yaliyokuwa yakitolewa kwa kila ibara wakati wa kuujadili Muswada huu. Vigezo vilivyotumika kufikia makubaliano katika Kamati vilijumuisha kujiridhisha:-

(a) Iwapo kuna mahitaji ya marekebisho ya Sheria yaliyopendekezwa;

(b) Iwapo marekebisho yanayopendekezwa yanaendana na ahadi zilizotolewa kwa wananchi; na

(c) Iwapo marekebisho ya Sheria yapo ndani ya misingi ya Uandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwa ili Bunge likidhi mahitaji ya hali ya sasa:-

(a) Jumla ya ibara 12 katika Muswada huu zinastahili kupitishwa na Bunge kama zilivyo;

(b) Jumla ya Ibara saba zinahitaji kurekebishwa kidogo kwa kurekebisha uandishi, maneno au sehemu yake;

(c) Aya moja ya Ibara inahitaji kutokuwepo kabisa katika Muswada huu; na

(d) Aya moja inahitaji kuongezewa sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matokeo hayo, mtoa hoja, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Juma Aweso, Mbunge, aliafikiana na Kamati na kuja na Jedwali la marekebisho. Kamati inapongeza hatua hiyo ambayo iliwezesha kufikiwa mwafaka katika mambo yanayohusu maslahi ya wananchi katika shughuli za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iweke juhudi katika kutoa elimu mara kwa mara kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza, kulinda na kuhifadhi raslimali za maji. Wananchi wakielewa umuhimu huo, ulinzi, utunzaji,

na uhifadhi wa raslimali za maji utakuwa wa kiwango cha kuridhisha; na

(ii) Kwa kuzingatia kwamba, Sera ya Maji ya Taifa ya Mwaka 2002 ni nyenzo muhimu inayoweka dira ya usimamizi wa raslimali za maji nchini, hivyo ni vyema ikahuishwa ili iendane na hali halisi iliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa uamuzi wako wa kuuleta Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwenye Kamati ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji. Kwa kweli uzoefu wa Wajumbe katika Sekta ya Maji umekuwa na mchango wa kutosha wakati wa uchambuzi. Aidha, utayari wa Wajumbe kupokea na kusikiliza maoni ya wadau umesaidia kupata mawazo yenye tija katika uzingatiaji wa maslahi ya Umma wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua hii, nawashukuru tena wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Wadau hao ni:-

(i) Mtandao wa Maji na Usafi wa Mazingira Tanzania *(Tanzania Water and Sanitation Network - TAWASANET)* ambao unajumuisha Mashirika yasiyo ya Kiserikali sita ambao ni Shahidi wa Maji; *TAFEs, IECA, SNV,* MAMADO na SAWA TANZANIA; pamoja na

(ii) *Africa Rural Development Support Initiative*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Weledi walionao na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi umesaidia kufanikisha ukamilifu wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa taarifa hii, Bunge litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi ya Umma, Taifa na uhai endelevu wa Tanzania. Aidha, kwa kutambua mchango wa Wajumbe, naomba waingie kwenye *Hansard* kama orodha yao ilivyo na inavyoonekana kwenye vitabu vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa baadhi ya Wabunge ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji wakati wa uchambuzi wa Muswada huu, sasa ni Wajumbe wa Kamati nyingine, sina budi kuwashukuru sana kwa mchango wao ambao ni sehemu ya Taarifa hii. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua fursa hii kuwakaribisha Wabunge walioteuliwa hivi karibuni kuwa Wajumbe wapya wa Kamati hii ambao ni Mheshimiwa Asya Sharifu Omary na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumshukuru Waziri wa Maji na Wataalamu mbalimbali kutoka Serikalini kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada. Maelezo yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc;* na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc* kwa kuongoza kikamilifu shughuli za Sekretarieti katika kuratibu uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, namshukuru Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kukushukuru wewe kwa jinsi ulivyoongoza kipindi hiki wakati nawasilisha wasilisho hili la Muswada huu. Napenda pia kuwashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Eunike Shirima na Chacha Nyakega, pamoja na Ndugu Waziri Kizingiti, Msaidizi wa Shughuli za Uratibu kwa kufanikisha kazi za Kamati kama ilivyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA MAJI WA MWAKA 2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimal za Maji (The Water Resources Management Amendment), Bill, 2022.

Muswada huu wenye jumla ya Ibara 22 ulisomwa mara ya Kwanza tarehe 23 Juni, 2022 katika Kikao cha Hamsini cha Mkutano wa Saba wa Bunge. Baada ya hatua hiyo, Muswada huo ulipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu

ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni hiyo inaitaka Kamati inayohusika kuujadili Muswada huo mapema iwezekanavyo. Kwa kuthamini imani yako kwa Kamati hii na kwa kutambua masharti hayo ya Kanuni za Bunge, mapema wakati wa vikao vya Kamati za Bunge vilivyoanza tarehe 29 Agosti, 2020, Kamati ilianza kuufanyia kazi Muswada huo. Lengo la kazi hiyo ni kuhakiki mapendekezo yanayotolewa na kubani kama kuna maslahi yoyote kwa Bunge kutunga Sheria inayopendekezwa. Maslahi mahususi katika Muswada huu ni manufaa yanayoweza kupatikana katika uendeshaji wa shughuli za Umma chini ya Sekta ya Maji, Sekta Ndogo ya Rasilimali za Maji nchini.

## 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya Uchambuzi wa Muswada huu kwenye Kamati ni kuliwezesha Bunge kuzingatia ahadi za Serikali kwa wananchi na misingi ya uendeshaji wa Sekta ya Maji nchini kwa namna inayozingatia maendeleo ya uchumi - jamii pamoja na ustawi wa watu na taifa. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linatarajiwa kupitia Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Rasiliali za Maji kwa namna inayozingatia maslahi ya Umma na uhai endelevu wa taifa letu.

Taarifa hii inalijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu pamoja na matokeo ya Uchambuzi. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kuamua, Taarifa inajumuisha Maoni na Ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekeibisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kama inavyoonekana katika Taarifa iliyowekwa mezani mapema leo hii.

## 1.2 Njia na Mbinu zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, imeweka msingi unaotaka Taaifa ya Kamati ioneshe namna jambo linaloripotiwa lilivyofanyiwa kazi. Aidha, ili kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti (reliability) na ustahiki (validity), naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu.

### 1.2.1 Njia zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, njia zilizotumika kufanyia kazi Muswada huu zimechangia kufanikisha uchambuzi na hatimaye maandalizi ya Taarifa hii. Kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142, naomba kuzitaja njia zilizotumika na madhumuni ya kila moja kama ifuatavyo:-

(a) Kupokea maelezo ya mtoa hoja kuhusu mapendekezo yake ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Lengo ni kupata mantiki ya marekebisho yanayopendekezwa;

(b) Kufanya mapitio ya Maudhui ya Muswada na kubaini mambo yanayopendekezwa kurekebishwa katika mfumo wa usimamizi wa Rasilimali za Maji. Madhumuni ni kutathmini kufaa au kutokufaa kwa marekebisho yanayopendekezwa;

(c) Kuoanisha mapendekezo ya Muswada wa Sheria inayojadiliwa na miongozo mingine katika shughuli za Umma chini ya sekta hii. Kusudio ni kuzingatia hali halisi katika kutathmini mapendekezo yaliyotolewa na mtoa hoja.

(d) Kujadili dhana kuu (key concept) ya Sekta ya Maji inayoguswa na mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Lengo ni kujenga mtazamo mpana unaosaidia kuhakiki maudhui ya Muswada kwa kulinganisha na matarajio ya wananchi; na

(e) Kupokea na kusikiliza Maoni ya Wadau kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 97(2) pamoja na masharti ya Kanuni ya 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Nia ni kuwa na maoni jumuifu kutoka katika umma na kuliwezesha Bunge kuendelea kuzingatia mtazamo wao katika utungaji wa Sheria.

**1.2.2 Mbinu zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kulisaidia Bunge lako tukufu kutunga Sheria yenye manufaa na inayozingatia maslahi ya sekta hii, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali kuuelewa Muswada huu. Naomba kubainisha mbinu hizo kwa kutaja zifuatazo:-

(e) Kubaini nia ya mapendekezo kwa kusoma Jina Refu la Muswada na Sheria inayopendekezwa kurekebishwa, pamoja na kupitia maelezo ya sababu na madhumuni ya Muswada huu;

(f) Kupambanua mambo makuu yanayorekebishwa katika mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi wa rasilimali za maji;

(g) Kuoanisha nia, mambo yanayopendekezwa kurekebishwa na Sera na Sheria zilizopo pamoja na ahadi iliyotolewa kwa wananchi katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020; na

(h) Kupima mapendekezo ya marekebisho ya usimamizi wa rasilimali za maji katika muono mpana wa Afrika na dunia kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitumia njia na mbinu zilizobainishwa, ambazo uwezo wake umetoa manufaa ya uchambuzi unaoliwezesha Bunge kukidhi

matarajio ya wananchi. Nikiri kuwa njia na mbinu hizo zimeiwezesha Kamati kupata undani wa marekebisho yanayopendekezwa kufanyika katika mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi wa rasilimali za maji.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, ulifanyiwa uchambuzi kwa kuhakiki na kupembua maudhui, masharti, mpangilio na dhamira kwa ujumla. Uchambuzi huo ulijumuisha mapitio ya jumla ya maudhui na baadaye upembuzi wa Ibara za Muswada huo ili kupata picha halisi ya maudhui na msingi wa masharti ya Sheria yanayopendekezwa. Lengo ni kujiridhisha na masuala makuu manne ya kiuchambuzi, ambayo ni:

(e) Iwapo kuna mahitaji ya sheria inayopendekezwa;

(f) Iwapo pendekezo katika Muswada huu linaendana na ahadi na mwelekeo wa jumla wa nchi, kanda na dunia;

(g) Iwapo pendekezo linakidhi haja ya sheria iliyobainishwa; na

(h) Iwapo misingi ya utungaji wa sheria imezingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo hayo, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika sehemu mbili. Sehemu hizo ni: Upembuzi wa Maudhui ya Muswada wa Sheria na Uchambuzi wa Ibara za Muswada ikilinganishwa na vifungu vya Sheria inayorekebishwa. Mtiririko huo unaweza kulisaidia Bunge kufanya uamuzi unaotokana na tatizo au ombwe la sheria inayorekebishwa, unaotatua au kuziba ombwe ipasavyo na unaozingatia misingi ya utungaji wa sheria.

### 2.1 Upembuzi wa Maudhui ya Muswada (*thematic review*)

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya kupembua maudhui ya Muswada huu ni kubaini uthabiti wa marekebisho yanayopendekezwa ili kulishauri Bunge inavyostahili. Kwa ujumla utaratibu wa kibunge wa hoja kuwasilishwa, kuungwa mkono, kujadiliwa na kuamuliwa, unahitaji misingi inayofanikisha uhakiki na upembuzi wa kina wa hoja inayojadiliwa. Kwa sababu hiyo, Kamati imefanya mapitio ya kimaudhui ya Muswada huu ili kulibainishia Bunge mambo yatakayolisaidia kuamua.

Mapitio ya jumla yanaonesha kuwa dhana kuu katika sheria inayopendekezwa kurekebishwa ni Usimamizi wa Rasilimali za Maji *(Water Resources Management*). Kimaana, usimamizi (menejimenti) ya rasilimali za maji ni mchakato wa kupanga, kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji. Dhana hii inajumuisha taasisi, miundombinu, taratibu na michakato ya utumiaji, uhifadhi na udhibiti wa matumizi ya rasilimali za maji. Kwa maana

hiyo, Muswada huu unahusu marekebisho ya Sheria inayohusu utaratibu, mamlaka, wajibu, majukumu, haki na masharti mbalimbali kuhusu uhifadhi, usimamizi, na udhibiti wa matumizi ya maji.

Chimbuko la dhana hii katika suala la rasilimali za maji ni hali halisi ilivyo duniani, Afrika na Tanzania. Ni dhahiri kwamba idadi ya watu, maendeleo ya shughuli za kibinaadamu, mahitaji ya maji na ulazima wa kuzingatia uendelevu wa mazingira ya vyanzo vya maji ni miongoni mwa mambo yanayosukuma dhana ya usimamizi wa rasilimali za maji. Kwa msingi huo, mapendekezo yoyote ya Sheria katika sekta ya maji yanapaswa kuzingatiwa kwa muono wa dhana ya usimamizi wa rasilimali za maji.

**Mheshimiwa Spika,** uelewa huo uliisukuma Kamati kuchanganua mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Matokeo ya kufanya hivyo, yamebainisha mambo mbalimbali yanayoguswa na Muswada huu. Naomba kulibainishia Bunge kwa kutaja baadhi ya mambo hayo na kuyaeleza kwa kifupi kama ifuatavyo:-

(k) Cheo cha Ofisa Bonde la Maji (*Water Basin Officer*) kinabadilishwa kuwa Mkurugenzi wa Bonde la Maji (*Water Basin Director*). Itambulike kuwa kwa sasa uendeshaji wa sekta ya maji unahitaji maofisa hao waendelee kuwa na mamlaka na madaraka yanayoendana na cheo kinachopendekezwa kwenye Sheria;

(l) Tafsiri ya neno mahakama "*court*" inaongezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Bila kufanya hivyo, sheria itaendelea kuacha utata ambao si jambo la kuendelea nalo. Utata huo katika kushughulikia makosa yanayohusu ukiukaji wa masharti ya usimamizi wa rasilimali za maji unahitaji kutatuliwa na mfumo wa kisheria;

(m) Wigo wa masharti ya miradi ya maji kufanyiwa tathmini ya kimkakati ya athari ya mazingira unaongezwa. Ongezeko hilo ni jambo linalopaswa kuzingatiwa inavyostahili;

(n) Ufafanuzi wa majukumu ya Bodi ya kushauri kuhusu uratibu na uainishaji wa vipaumbele katika uwekezaji wa fedha kwenye masuala ya rasilimali za maji unawekwa bayana zaidi. Jambo hilo linahitaji kupimwa inavyostahili;

(o) Wadau wanawezeshwa zaidi kupata Taarifa kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika usimamizi wa rasilimali za maji. Lengo la kuwashirikisha wadau katika uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za maji linapaswa kuangaliwa kama limewekewa masharti stahiki;

(p) Adhabu kwa kosa la ufanyaji wa shughuli za kibinaadamu kwenye maeneo tengefu (*protected zones*) inabainishiwa msingi katika Sheria. Mantiki na busara za adhabu inahitaji mtazamo wa Bunge;

(q) Uzuiaji wa maji kwenye mkondo wake (*impoundment* of *water*) unawekewa masharti ili kusimamia na kudhibiti jambo hilo. Ni vema Bunge lioanishe jambo hilo na matarajio ya wananchi;

(r) Usimamizi wa uchunguzi na uhakiki wa ubora wa maji kwa kumruhusu Waziri anayehusika kuunda maabara za ubora unawekewa masharti katika Sheria. Dhima ya Bunge katika jambo hilo inapaswa kuwa kipimo;

(s) Changamoto ya gharama za usajili wa mabwawa na haja ya kuongeza kazi ya usajili wa mabwawa yenye usalama inawekewa misingi ya kutatuliwa. Dhamana ya Bunge kwa mahitaji ya wananchi kuhusu usajili wa mabwawa ya maji inapaswa kuwa kigezo cha uchambuzi; na

(t) Masharti yanayohakikisha kuwa kuna uwiano stahiki wa kijinsia katika usimamizi wa rasilimali za maji yanaongezwa na kuimarishwa katika Sheria. Bunge linapaswa kujiridhisha na masharti hayo muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho hayo yanayopendekezwa katika mfumo wa kitaasisi na kisheria wa usimamizi wa rasilimali za maji, yanaweza kuhakikiwa kwa kufanya mapitio ya machapisho na miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za umma nchini. Lengo ni kuzingatia mtazamo mpana kuhusu marekebisho yanayopendekezwa pamoja na kuoanisha mambo hayo na mwelekeo wa nchi kwa muktadha wa matarajio ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** mtazamo wa Kamati wakati wa uchambuzi ulijengwa kwenye Sera ya Maji ya Mwaka 2002, ahadi waliyopewa wananchi katika Ilani ya CCM ya mwaka 2020, bila kuacha mwelekeo uliobainishwa katika dira ya taifa ya 2025. Kwa faida ya mjadala kuhusu hoja iliyo mbele ya Bunge, naomba kutoa muhtasari wa matokeo ya mapitio kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Mtazamo wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, mtazamo wa jumla kuhusu usimamizi wa Rasilimali za Maji unajengeka kwa mapitio ya machapisho mbalimbali ikiwemo Taarifa za Kimataifa na Kikanda. Kamati ilijiridhisha kwa kuzingatia Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo ya Sekta ya Maji na Dira ya Afrika kuhusu Maji. Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo ya Maji ya mwaka 2021 (UN – World, 2022) inatambulisha dunia haja ya kuboresha usimamizi wa rasilimali

za maji. Ripoti hiyo imesisitiza mambo matatu kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji.[1]

Mambo hayo yaliyosisitizwa ni kutambua, kupima na kuendeleza rasilimali za maji pamoja na kufungamanisha mambo hayo katika michakato mbalimbali ya uamuzi. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kufanya hivyo ni muhimu ili kufanikisha ufuatiliaji wa usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na kufanikisha malengo endelevu (Sustainable Development Goals - SDGs). Mtazamo huu ulizingatiwa katika uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Kwa mfano, katika uchambuzi wa ibara kwa ibara, Kamati ilibaini kwamba, Ibara ya 8 inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kidogo cha (4) katika Kifungu cha 37 cha Sheria Mama kwa lengo la kubainisha kosa la kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ambayo yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu (*protected zones*) ya vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, Kamati ilizingatia Dira ya Maji - Afrika kwa mwaka 2025 (*The Africa Water Vision for 2025*) ambayo inajenga msingi wa mipango ya muda mrefu kuhusu maji katika Kanda ya Afrika na Jumuiya za Kikanda ndani ya Afrika. Kwa ujumla Dira hiyo inahimiza utawala bora katika usimamizi wa Rasilimali za Maji na kujenga uwezo wa kukusanya na kutoa taarifa kuhusu rasilimali za maji.

Dira ya Maji - Afrika inatambua kwamba bara hili limebeba vyanzo vingi vya maji na kwamba linakabiliwa na upotevu mkubwa wa maji ya mvua. Dira hiyo imefafanua zaidi kuwa uhaba wa maji katika baadhi ya nchi unatokana na kutolinganishwa kwa suala la rasilimali za maji zilizopo na mahitaji ya maji.

**Mheshimiwa Spika**, rasilimali za maji zinahitaji kulindwa na kuhifadhiwa ili ziwe za kudumu na endelevu, lakini pia zinapaswa kutumika kukidhi mahitaji ya maji yanayoongezeka. Uhusiano huo umeliingiza suala la usimamizi wa rasilimali za maji katika dhana ya usalama wa maji wa Taifa (*national water security*). Dhana ya Usalama wa Maji imefasiriwa na Kikosi kazi cha Usalama wa Maji cha Umoja wa Matiafa. Fasiri hiyo ilielezwa kama ifuatavyo:-

"*Water Security is the Capacity of a population to safeguard sustainable access to adequate quantities of and acceptable qualities of water for sustaining livelihoods, human well - being, and socio-economic development for ensuring protection against waterborne pollution and water related disasters and for preserving ecosystems in a climate of peace and political stability*."

[1] (Angalia unwater-org/publications/un-word-development –report iliyopitiwa tarehe 4 Agosti, 2022).

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji unaokidhi mahitaji ya Umma ni ule unaotengenezwa kwa sheria zinazosaidia usalama wa maji. Suala kubwa kutokana na ukweli huo ni kuona iwapo marekebisho ya Sheria yanayopendekezwa yatasaidia kuboresha usalama wa maji. Miongoni mwa viashiria muhimu vya kuzingatiwa kwa dhana ya usalama wa maji, ni masharti ya sheria inayopendekezwa kuongeza uhakika endelevu wa maji kwa kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maji. Aidha, uzingatiaji wa ruhusa ya matumizi ya maji kwa uhai wa binadamu ni suala lingine lililopewa uzito wakati wa uchambuzi huu.

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Ibara ya 4 ya Muswada huu ya kufuta maneno "***a major water Project is planned***" na kuweka maneno "***Water Programmes and development plans are prepared***", yanaendana na dhana ya usalama wa maji.
Mwendano huo unatokana na mambo makubwa mawili ambayo ni:-

(c) Kutaka uendelevu kwa kuzingatia tathmini ya mazingira kwenye miradi yote ya maji; na

(d) Kuweka adhabu zinazoogofya ili kuendelea kuzilinda rasilimali za maji.

### 2.1.2 Mapitio ya miongozo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua Muswada huu kwa muktadha wa ahadi walizopewa wananchi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Sababu ya kufanya hivyo ni kupima kama matarajio ya Wananchi yanazingatiwa katika Muswada huu. Kamati ilibaini kwamba, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinachoongoza Serikali, kiliwaahidi wananchi kuwa Serikali itasimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji.

Nia ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria imeelezwa kuwa ni kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ya usimamizi wa Rasilimali za Maji. Nia hiyo, inaendana kabisa na ahadi waliopewa wananchi kama inavyotolewa katika aya ya 37, ukurasa wa 36 wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Sehemu ya aya hiyo inahusu kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji.

### 2.1.3 Mapitio ya Sera ya Maji

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali, Kamati iliona umuhimu wa kuoanisha mapendekezo yanayotolewa kwa upande mmoja na mtazamo wa nchi kisera kwa upande mwingine. Mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 yalisaidia kuhakiki maudhui ya Muswada wa Sheria unaojadiliwa na Bunge lako tukufu leo.

Ili kuweka mtazamo wa Kamati kuhusu Muswada huu katika muktadha stahiki, naomba kulibainishia Bunge kuhusu sera inayorejewa. Sera hiyo imegawanyika katika sehemu kuu tatu:-

(a) Menejimenti ya rasilimali za maji;

(b) Utoaji wa huduma za maji vijijini; na

(c) Utoaji wa huduma za maji safi na maji taka mijini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya hoja hii inayojadiliwa na Bunge kwa sasa, Kamati ilijielekeza kwenye sehemu ya sera inayohusu menejimenti ya rasilimali za maji kwa kuwa ndiyo inayohusika katika marekebisho ya sheria inayopendekezwa.

Lengo kuu la Sera hii ni kuendeleza mifumo kamilifu kwa ajili ya maendeleo na menejimenti ya rasilimali za maji. Mifumo hiyo inakusudiwa kuwa endelevu na shirikishi kwa wanufaika. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, azma ya Sera hii inatiliwa nguvu za kisheria katika mapendekezo ya Serikali. Jambo hili linadhihiri katika maudhui ya Muswada ikilinganishwa na Sheria inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho.

### 2.2 Uchambuzi wa Ibara za Muswada

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Muswada ibara kwa ibara ulifanyika kwa kusoma kila sentensi na kila neno katika Muswada. Utaratibu huo unazingatia ushauri aliowahi kuutoa Mwandishi Mtaalamu wa Sheria, John Aneurin Grey wa Chuo Kikuu cha Wales kwa kusema:-

*"The function of a Committee on a bill, says Erskine May, is to go through the text of the Bill clause by clause and, if necessary, to making such amendments in it as may seem generally acceptable".*

Kwa tafsiri ya Kiswaili isiyo rasmi tunaweza kusema:

*Kazi ya Kamati inayoshughulikia Muswada, anasema Erskine May, ni kupitia Matini (text) ya Muswada ibara kwa ibara na, ikilazimika neno kwa neno kwa mtazamo wa kufanya marekebisho ambayo yanaweza kuwa ya kukubalika.*[2]

---

[2] Taz. Uk. 37 JAG Griffith, Parliamentary Security of Government Bills, P.E.P. Study of Parliament Group, London

Katika kufanya hivyo, Kamati ilipitia Muswada wote kuanzia Namba ya Utambuzi wa Chapisho la Muswada (ISSN-International Standard Serial Number), Namba ya Muswada, Namba ya Toleo la Gazeti la Serikali lililoutangaza Muswada, Tarehe, Mpangilio, Sababu na Madhumuni hadi jina na saini ya mdhamini wa hoja. Lengo la kufanya hivyo ni kujiridhisha na masharti yote ya utungaji wa Sheria na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kulishauri Bunge inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi Kamati ilitambua kazi kuu ya kuzingatia mapendekezo kwa kutathmini maelezo ya mtoa hoja, mapendekezo ya wadau na maoni yaliyokuwa yakitolewa kwa kila Ibara wakati wa kuujadili Muswada huu. Vigezo vilivyotumika kufikia makubaliano katika Kamati vilijumuisha kujiridhisha:-

(a) Iwapo kuna mahitaji ya marekebisho ya Sheria yaliyopendekezwa;

(b) Iwapo marekebisho yanayopendekezwa yanaendana na ahadi zilizotolewa kwa wananchi; na

(c) Iwapo marekebisho ya Sheria yapo ndani ya misingi ya Uandishi.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwa ili Bunge likidhi mahitaji hali ya sasa:

(a) Jumla ya Ibara Kumi na Mbili (12) katika Muswada huu zinastahili kupitishwa na Bunge kama zilivyo;

(b) Jumla ya Ibara Saba (7) zinahitaji kurekebishwa kidogo kwa kurekebisha uandishi, maneno au sehemu yake;

(c) Aya moja ya Ibara inahitaji kutokuwepo kabisa katika Muswada huu; na

(d) Aya moja inahitaji kuongezewa sehemu.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo hayo, mtoa hoja, Waziri wa Maji, Mhe. Juma Aweso, Mb aliafikiana na Kamati na kuja na Jedwali la marekebisho. Kamati inapongeza hatua hiyo ambayo iliwezesha kufikiwa mwafaka katika mambo yanayohusu maslahi ya wananchi katika shughuli za Umma.

## 3.0 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu Kamati inayo maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

i. Serikali iweke juhudi katika kutoa elimu mara kwa mara kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza, kulinda na kuhifadhi raslimali za maji. Wananchi wakielewa umuhimu huo, ulinzi, utunzaji, na uhifadhi wa raslimali za maji utakuwa wa kiwango cha kuridhisha; na

ii. Kwa kuzingatia kwamba, Sera ya Maji ya Taifa ya Mwaka 2002 ni nyenzo muhimu inayoweka dira ya usimamizi wa raslimali za maji nchini, hivyo ni vyema ikahuishwa ili iendane na hali halisi iliyopo sasa.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena nakushukuru kwa uamuzi wako wa kuuleta Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwenye Kamati ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji. Kwa kweli uzoefu wa Wajumbe katika Sekta ya Maji umekuwa na mchango wa kutosha wakati wa uchambuzi, Aidha, utayari wa Wajumbe kupokea na kusikiliza maoni ya Wadau umesaidia kupata mawazo yenye tija katika uzingatiaji wa maslahi ya Umma wakati wa kujadili Muswada huu. Kwa hatua hii niwashukuru tena Wadau mbalimbali waliotoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Wadau hao ni:-

(a) Mtandao wa Maji na Usafi wa Mazingira Tanzania (Tanzania Water and Sanitation Network) - TAWASANET ambao unajumuisha Mashirika yasiyo ya Kiserikali sita (6): Shahidi wa Maji; TAFEs, IECA, SNV, MAMADO na SAWA TANZANIA; pamoja na

(b) Africa Rural Development Support Initiative (ARUDESI)

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Muswada. Weledi walionao na umahiri waliouonesha wakati wa uchambuzi umesaidia kufanikisha ukamilifu wa taarifa hii. Naamini kwa taarifa hii, Bunge litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi ya Umma, taifa na uhai endelevu wa Tanzania. Aidha, kwa kutambua mchango wa Wajumbe, naomba kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Athuman Almas Maige, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb
4. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
5. Mhe. Charles John Mwijage, Mb
6. Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb
7. Mhe. Mohamed Suleiman Omar, Mb
8. Mhe. Furaha Ntengo Matondo, Mb

9. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb
10. Mhe. Asya Sharifu Omary, Mb
11. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb
12. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb
13. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb
14. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb
15. Mhe. Michael Mwita Kembaki, Mb
16. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb
17. Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mb
18. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb
19. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb
20. Mhe. Rita Enespher Kabati, Mb
21. Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb
22. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
23. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb
24. Mhe. Yahya Ali Khamis, Mb
25. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb
26. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb; na
27. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia kuwa baadhi ya Wabunge ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji wakati wa uchambuzi wa Muswada huu, sasa ni Wajumbe wa Kamati nyingine, sina budi kuwashukuru sana kwa mchango wao ambao ni sehemu ya Taarifa hii. Wajumbe hao ni

i. Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb; na
ii. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb

Aidha, nichukue fursa hii kuwakaribisha Wabunge walioteuliwa hivi karibuni kuwa Wajumbe wapya wa Kamati hii ambao ni:-

i. Mhe. Asya Sharifu Omary, Mb; na
ii. Mhe. Tauhida Cassian Gallos, Mb

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kumshukuru Waziri wa Maji na Wataalamu mbalimbali kutoka Serikalini kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Muswada. Maelezo yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Muswada huu kwa wakati.

Namshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* kwa kuongoza kikamilifu shughuli za Sekretarieti katika kuratibu uchambuzi wa Muswada huu. Mwisho lakini si kwa umuhimu, namshukuru Ndg. Michael Chikokoto, ndc, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Fedha na Uchumi, Makatibu wa Kamati Ndg. Eunike Shirima na Chacha Nyakega,

pamoja na Ndg. Waziri Kizingiti, Msaidizi wa Shughuli za Uratibu kwa kufanikisha kazi za Kamati kama ilivyostahili.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

15 Septemba, 2022

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Kifugo na Maji. Ahsante kwa uwasilishaji.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni muda wa mjadala wa pamoja. Tutaanza na Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Ana Richard Lupembe na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, wajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Muswada huu muhimu wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Maji. Nami kama Mjumbe wa Kamati ya Maji, kwanza naunga mkono marekebisho ya sheria ambayo yanakwenda kufanywa na pia naunga mkono taarifa ya Kamati ambayo imemaliza kuwasilishwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza pia kwa kumnukuu Ismail Serageldin huyu mimi namwita ni Balozi wa masuala ya maji duniani. Amekuwa ni sauti kubwa sana kuzungumzia masuala ya maji na namna gani tunaweza tukatunza maji kwa ajili ya vizazi vijavyo. Yeye katika moja wa mkutano wake mwaka 1995 alisema "*if the wars of this century were fought over oil, the wars of the next century will be fought over the water.*" Anasema kwamba kama vita vya dunia vya karne hii ambayo inamalizika vilipiganwa kwa sababu ya mafuta, pengine na dhahabu na mali nyingine za thamani duniani, anasema kwamba karne inayokuja, vita kubwa duniani itahusisha masuala ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa kwamba kuna watu wapatao milioni kama 400 walio Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao wana changamoto kubwa ya kukosa maji. Sababu zimeelezwa zinaeleweka kwamba dunia imeongezeka sana watu, shughuli za kibinadamu zimeongezeka sana, kwa hiyo, inakuwa sasa suala hili ni la lazima hasa kwa

nchi yetu kama Tanzania ambayo bado haijapata majanga makubwa kama ambayo yanapatikana katika nchi nyingine ambazo tayari zimeanza kuwa kame kwa sababu zilishindwa kutunza hivi vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Watanzani ni lazima tuchukue hatua sasa kuhakikisha kwamba tunatunga sheria ambazo zitatoa mamlaka kubwa kwa hawa wasimamizi wa mabonde kuweza kusimamia rasilimali za maji kwa ajili yetu sisi wenyewe na kwa ajili ya vizazi vijavyo. Kwa hiyo, ni muhimu sana hili jambo tukaweza kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inaipatia mamlaka za mabonde ya maji; kwanza, kuwa na udhibiti kwenye matumizi ya maji, kwa maana ya kwamba, hata kama mtu anahitaji kuchimba kisima mahali popote, anahitaji apewe kibali. Hiki kibali kitamwelekeza kitaalamu ni nini afanye. Kwa sababu tumeona sehemu nyingi kwamba watu wanachimba maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu kinyume na sheria; na maji haya wakati mwingine wanachimba pengine hawafikii kile kiwango kinachotakiwa na hivyo kusababisha yale maji yawe machafu, yawe na wadudu na kuathiri pia afya za watumiaji. Kwa hiyo, sheria hii ambayo tunaileta sasa itakwenda kuzipa mamlaka za mabonde ya maji, kusimamia hata wale ambao wanachimba visima vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kushauri kwamba kwa kuwa sasa haya mabonde tunaenda kuyapatia nguvu ya kisheria, ni lazima pia wafanye mapitio ya visima vyote ambavyo vimechimbwa katika nchi hii na vinavyotumika, kama vimechimbwa kwa viwango ambavyo vitamsaidia Mtanzania kuwa na afya anapotumia hayo maji. Kwa hiyo, wasimamie hata kule ambako tayari visima vilishachimbwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapokwenda kutunga sheria hii na kuongeza usimamizi mkali kwenye vyanzo vyetu na maeneo tengefu, maana yake, kuna watu ambao wanakwenda kuathirika. Wengi ambao walikuwa wanalima katika maeneo ya mabonde, wataathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hizi sheria zinapokuja kuna mmoja atafaidika na mmoja ataumia. Wale ambao wanalima kwenye maeneo ya mabonde, wanakwenda kuumia kidogo. Sasa mapendekezo yangu ni kwamba pamoja na kusimamia hizi rasilimali za maji, ni lazima pia Wizara ijikite sana katika kuendeleza na kuanzisha maeneo mapya. Kwa mfano, kama tutakwenda kutengeneza mabwawa ambayo yanatokana na kudaka yale maji yanayotokana na mvua; kwa mfano sasa Wizara ya Maji imeshaanza kutengeneza mabwawa, yale maeneo ya mabonde ambayo ni njia kubwa za maji, tukienda kujenga yale maeneo tukatengeneza hivi vidakio, tukatengeneza mabwawa, tutasaidia wananchi wengi ambao tutaweza sasa kuwatoa kwenye mabonde kwa sababu sheria hii itawabana,

maana yake tunawapa jambo lingine ambalo ni mbadala. Kwa hiyo, hilo nalo ni jambo la kulizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni namna gani pia sheria hii itakwenda kutekelezwa kwa wepesi? Ni muhimu sana tukaunda jumuiya kwenye vijiji na maeneo haya yenye vyanzo vya maji na maeneo tengefu. Tuwe na jumuiya za wasimamizi wa mabonde kwenye haya maeneo ili sasa kiwe ndiyo chombo ambacho kitakwenda kusaidia kutoa elimu kwa wananchi. Maana kama mamlaka yenyewe ina watu wachache, sasa kama tutatengeneza hizi jumuiya kwenye vijiji, kwenye hivi vyanzo vya maji na kwenye maeneo haya tengefu, itasaidia hii elimu ifike kwa haraka. Kwa hiyo Wizara na mamlaka hizi za mabonde ya maji zijikite sana katika kutoa elimu kwa kutumia hizi jumuiya ambazo tutaenda kuziunda kwenye haya maeneo ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuangalie pia, kumekuwa na uharibifu wa maji kwa ujumla, kwa sababu sheria hii pia inazungumzia uchafuzi wa maji. Tuangalie ni namna gani tunaweza kushirikiana na Wizara nyingine na mamlaka nyingine. Tumeona hivi karibuni kwamba kwenye maeneo ya maziwa na bahari, ni kwamba watu wamekuwa wakijenga, yaani pembezoni kabisa, wengine wanaingia mpaka ndani ya maji. Sasa hii sheria sijui itafanyaje kwa sababu naliona hili pia ni aidha ni uchavuzi wa maji na pia inaweza ikaleta *diversion* kwenye haya maji na baadaye inaweza kuleta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona huko duniani, iko bahari moja ilishawahi kukauka. Profesa Muhongo alishatuambia, miaka 400 iliyopita kuna bahari moja ilishawahi kukauka kwa sababu ya matumizi mabaya ya maji. Sasa tunafanyaje kushirikisha hizi mamlaka nyingine? Watu wanaojenga mpaka kwenye haya maziwa ndani, hilo nalo tuangalie namna gani tutashirikisha mamlaka nyingine kuhakikisha kwamba hata haya maji yanatunzwa kwa ajili ya vizazi vingine vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye sheria hii nilitaka tu kuweka muhuri kwamba ninaunga mkono mabadiliko ya sheria hii na kwamba Bunge zima tuiunge mkono kwa sababu tutakwenda kuilinda nchi; na nchi hii itakuwa ni ya kutamaniwa na itaweza kuwa endelevu, hata vizazi vingine vitakavyokuja baadaye vitakuta mazingira yametunzwa na tutaendelea kupata uchumi unaotokana na vyanzo vya maji. Kama tutakuwa na vyazo vya maji ambavyo vimeendelezwa, itakuwa ni *source* nyingine ya uchumi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeki, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii kwa mikono yote miwili kwamba ipite ili nchi hii tuitunze kwa ajili yetu na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga. Tunaendelea na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe halafu Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje wajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Muswada wetu huu wa leo, wenye manufaa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa nafasi hii ya uzima na uhai. Naomba nimshukuru sana Waziri ambaye ametuletea Muswada huu kwa ajili ya manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kuona sasa ni kipindi cha kulinda rasilimali zetu za maji, kwa sababu maji ni uhai na bila maji hakuna kitu chochote kinachofanyika katika maisha ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangali kupitia maji katika maeneo mbalimbali ya mabonde na kupitia mabwawa, bila kuweka udhibiti hakuna kitu chochote kinaweza kufanyika. Sasa tunaona jitihada za Wizara kutuletea huu Muswada, ambao utatuwezesha kudhibiti maji, kwa sababu katika maeneo mengi kupitia vyanzo vya maji, kupitia hifadhi mbalimbali tumeona uharibifu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nilpongeze Serikali kwa kuona sasa ni kipindi cha kulinda rasilimali zetu za maji kwa sababu maji ndio uhai na bila maji hakuna kitu chochote kinachofanyika katika maisha ya binadamu. Ukiangalia kupitia maji katika maeneo mbalimbali ya mabonde na kupitia mabwawa na nini, bila kuweka udhibiti hakuna kitu chochote kinaweza kufanyika. Sasa tunaona jitihada za Wizara kutuletea huu Muswada sasa tunaweza kudhibiti maji, rasilimali ile maji kwa ajili ya manufaa kwa sababu katika maeneo mengi kupitia vyanzo vya maji, kupitia hifadhi mbalimbali tumeona uharibifu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kuna watu wengine wanathubutu kuingia katika maeneo ya vyanzo vya maji ambavyo vile vyanzo vya maji ambavyo tukivitunza na tukaviweka katika mazingira mazuri ambayo sisi wenyewe tunakuja kuvitumia na kupata manufaa na faida kwa ajili ya mahitaji ya binadamu. Tumeona kwenye mabwawa mbalimbali watu wanaingiza mifugo, watu wanafanya wanavyotaka wao, watu wanavuta maji kiholela, ina maana udhibiti haukuwepo, lakini leo tunaona Serikali imeleta Muswada huu ambao utasaidia sasa kuhakikisha mazingira yetu yatakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa katika hali halisia, uoto wa asili katika nchi yetu unaanza kupotea na uoto wa asili ni kitu muhimu sana. Vile vyanzo ambavyo zamani sisi wakati tunakua kulikuwa kuna chemchem, maji tu yanatoka chini, lakini zile sehemu zote zimepotea kutokana na uharibifu mkubwa ambao uliofanyika. Hata hivyo, kupitia Muswada huu utaweza kudhibiti sasa vile vyanzo vyote vya maji na mazingira yatakuwa mazuri. Tunajionea katika nchi yetu hata mvua sasa imekuwa ni ya kusuasua, mazingira yamekuwa si rafiki sana, unakuta tunapata tabu kwa sababu tumeshaharibu mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunatunza miti, sasa ile miti yote tumeshaiharibu, matokeo yake sasa hata mvua zimekuwa za kusuasua. Ingawa tunasema tumwombe Mungu atuletee mvua lakini mazingira tumeshayaharibu, lakini kupitia Muswada huu uliokuwa mbele yetu sasa tutaweza kupata mvua nzuri na vile vyanzo vyote vinaweza kudhibitiwa, kulindwa na tukaweza kupata manufaa makubwa kupitia miradi mikubwa mikubwa. Hii ni kwa sababu tukitunza vyanzo vya maji vizuri, tukitunza rasilimali zetu za maji, mazingira yetu yatakuwa mazuri, uoto wetu utarudi kama kawaida, tunaweza sasa tukatengeneza miradi mikubwa mikubwa kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa kuona sasa kupitia rasilimali hizi za maji, kuhakikisha kwenye maeneo yetu sasa udhibiti na usimamizi na wanawake nao wamekumbukwa kwa ajili ya kuwa katika vile vikao, upande wa jinsia wanawake wawili wapo. Tunajua akinamama ndiyo wahusika wakubwa wa tatizo na wanawake ndiyo wahangaikaji wakubwa kupitia maeneo yetu katika vijiji na vitongoji. Naomba niipongeze sana Serikali kwa kukumbuka uwiano wa kijinsia katika uongozi mbalimbali kwa maslahi yetu katika maeneo yetu katika masuala ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua watu wengi wanapenda kuchangia kwa sababu Muswada huu uliokuwa mbele yetu ni mzuri na ni jambo muhimu sana. Naomba niishukuru Wizara kwa kuwa itaweka maabara maalum kwa ajili ya kuhakikisha sasa ubora wa maji unapatikana katika kila eneo. Maana yake zamani maabara ilikuwa iko moja tu na Wizara kama Wizara ilikuwa haina maabara kila wilaya au kila mkoa, lakini sasa hivi tunaona Serikali inaamua sasa kuanza kuweka maabara kwa ajili ya usafi wa maji yetu na kuhakikisha tunapata maji safi na salama kupitia maji taka na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze sana Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. Anafanya kazi tunaona jitihada zake na watu wa mabonde wapo katika maeneo yetu wakiendelea kutafuta mazingira ya maji ili wananchi waweze kupata maji, naomba nimpongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Richard Lupembe. Tunaendelea na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje na Mheshimiwa Tumaini Bryson Magesa wajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia Muswada ulioko mbele yetu, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2022. Pia kama sehemu ya Wajumbe wa Kamati tunaunga mkono mapendekezo ya Serikali yaliyoletwa na tungetamani kuona kwamba yale ambayo wanayapendekeza katika Muswada huu, waende kuyasimamia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani tunaunga mkono mapendekezo ya Serikali na pia nitumie nafasi hii kuliomba Bunge lako Tukufu yaani Wabunge waweze kuunga mkono hoja iliyoletwa na Waziri, ni kwa sababu moja mapendekezo haya yanabeba maudhui ya kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la msingi sana kama tusipolinda vyanzo vya maji vya asili vilivyopo gharama za kupata maji kwa ajili ya *domestic use,* lakini pia tunakwenda kupanua mahitaji ya maji katika nchi hii katika kilimo na umwagiliaji, itakuwa shida sana kama vyanzo vya maji havitalindwa. Kwa hiyo ni hoja ya kwanza kwa nini tunaunga hoja mkono, kwa sababu inaenda kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, Wizara iendelee kuongeza jitihada za kuwafikishia maji Watanzania, wakishakuwa wamepata maji kwa ajili ya matumizi, maana yake kuvilinda vyanzo vya maji inakuwa ni rahisi, lakini kama mtu hana maji ya kutumia kwa vyovyote atayatafuta kwa njia anayoiona. Kwa hiyo kuwafikishia wananchi maji ili wapate maji ya kutumia itakuwa pia ni ulinzi kwa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa nini tuunge hoja mkono? Hoja hii imebeba maudhui ambayo pia wadau wametia maoni yao kwa maana kwamba wadau muhimu katika sekta ya maji pia wamekubaliana na mapendekezo haya na kuweka maboresho yao ambayo Serikali imeyapokea. Vile vile kwa nini tuunge hoja mkono? Ni kwa sababu inapendekeza adhabu na faini kwa mtu au taasisi ambayo itajihusisha na uharibu wa vyanzo vya maji pamoja na kuharibu mfumo wote wa udhibiti wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika Kamati msisitizo wetu ulikuwa kuwa, elimu na ushirikishwaji wa wananchi katika ulinzi na usimamizi ndiyo iwe nyenzo kubwa ya ulinzi. Kwa sababu gani tunasema hivi? Kama

unapendekeza adhabu na faini lakini mtu hajui kwamba hata anakosa, siyo sawa. Kwa hiyo Serikali yaani Wizara itumie muda wa kutosha kwa vyombo vya habari kwa namna yoyote inayoweza kupeleka elimu na kuwashirikisha wananchi. Huo ndiyo utakuwa ni ulinzi unaojitosheleza, lakini ukienda na nguvu ya adhabu na faini zilizopendekezwa, watu watatoa faini lakini hutakuwa umelinda vyanzo vya maji, kwa hiyo ndiyo maana tukasema kwamba Wizara itoe elimu na iwashirikishe sana wananchi ili wao wenyewe baada ya kupata elimu waweze kuwa ni walinzi wazuri wa vyanzo vya maji na usimamizi utakuwa ni bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, watu wengi sana nchini Tanzania tumechimba visima vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, lakini hatukujua kwamba tunahitaji vibali na kwamba kuna faini katika hilo. Ni ukweli usiopingika kwamba katika sasa sijui Kiswahili cha *aquifer* ni nini, lakini katika *aquifer* moja ukitoboa mashimo mengi sana ya visima, utaharibu kabisa mfumo wa maji, lakini hatujui. Sasa ndiyo maana kwamba lazima hiyo elimu wananchi waipate, kwamba jamani nyinyi katika mkondo huu hapa mko katika *aquifer* moja, *geological formation* ya *aquifer* moja hatuhitaji visima 20 hapa, la sivyo tutaharibu, elimu hiyo hatuijui, ni lazima tuipate ili tuweze kulinda hivyo vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine watu huchimba visima akipata maji katika yale maji ya juu juu ambayo siyo *aquifer* anaamini amepata maji, baadaye kisima kinakauka elimu hiyo hatuijui. Kwa hiyo ndiyo maana Wizara hii inahitaji kufanya sana uhamasishaji na ushirikishwaji ili hata visima vilivyochimbwa vionekane kwamba vina ubora wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu pia wamekuwa wakitumia chemchem yao siku zote, Waziri hajawapelekea maji ya bomba, wanaitumia kwa jinsi wanavyoweza, wakati mwingine anamwagilia ili apate kabichi ya kula. Mheshimiwa Waziri asiende akampiga faini mtu yule amweleweshe kwanza na amsaidie namna ya ambavyo atapata maji kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake, kwa sababu maji ni hitaji la msingi. Sasa Waziri akifika akampiga faini kwa sababu anatumia maji ya chemchem hajampa maji, nadhani Waziri anaelewa kabisa kwamba maji ni haki ya msingi, anayahitaji kwa matumizi, kwa hiyo tusitangulize faini kabla ya kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 13 inapendekezwa Waziri aweze kuanzisha maabara kwa ajili ya ubora wa maji. Hili jambo ni la kupongezwa na Mheshimiwa Waziri atafute vyanzo vya fedha kokote anakoweza kupata aanzishe maabara za kupima ubora wa maji. Kwa nini nadhani kwamba hili ni jambo la msingi? Watanzania wanaotoka baadhi ya maeneo sasa siyo kwamba na-*abuse* lakini tunaona kwamba wana meno ambayo yana rangi ya kahawia kwa sababu ya *fluorine*. Mara nyingi tunadhani kwamba hiyo ndiyo athari peke yake ya *fluorine* nyingi katika maji, lakini *florine* ikizidi inaleteleza hadi *osteoporosis,* ugonjwa wa kukonda mifupa

inakwenda mpaka kukuharibu *joints,* inazi-*damage fluorine* nyingi, lakini watu wengi katika maeneo ambayo tunatoka wanatumia maji, tunaona tu meno yao yamekuwa kahawia tunasema anatoka Singida, huyu anatoka Moshi huyu. Kwa hiyo lazima Waziri aweke maabara ili zipime ubora wa maji kabla ya kutumiwa kwa sababu athari za *elements* nyingi katika maji ni kubwa zaidi ya zinazoonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa uchafuzi wa maji ambao ni mbaya zaidi na huwa hatuiongelei ni *nitrate*. *Nitrate* inaingia katika maji kutoka kwenye vyoo na maji ya viwandani mara nyingi visima vile vilivyochimbwa vifupi wanatumia yale maji kukiwa na *nitrate* nyingi sana. Sasa unashangaa kwa nini tuna saratani nyingi na kuna *birth defects* yaani kizazi kinaharibika kwa sababu ya *too much nitrate* katika maji. Kwa hiyo *water quality laboratories* ni za msingi sana ili Watanzania watumie maji ambayo yako *quality,* tutamsaidia sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu kutojadili kwamba vyanzo vya kansa vinatoka wapi kumbe vingine ni kwa sababu ya *too much nitrate*. Kwa hiyo *Water Quality Laboratories* ni za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, sera tunajadili Sera ya mwaka 2002 ambapo *population* ya Watanzania ilikuwa ni 34,000,000 sensa itatwambia lakini tuko *almost doubled,* sasa una sera ya *population* ya watu ambao wame-*double,* yawezekana ikawa haikidhi mahitaji ya sasa. Kwa hiyo tunaomba Wizara iharakishe mchakato wa kuwa na sera mpya ambayo ita-*take on both,* Dira ya Maendeleo ya miaka 25 mingine, lakini pia kuangalia maendeleo ya kisasa, miji yetu imekua na kila maendeleo mengi yamefanyika Tanzania baada ya miaka hii 20, tupate Sera mpya ya Maji ambayo itakuwa inakidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango huo, naunga mkono hoja na tumwombe sana Waziri akayasimamie haya na atafanikiwa sana katika Wizara ambayo amepewa dhamana kuisimamia. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, tunashukuru kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mheshimiwa Tumaini Bryson Magesa na Mheshimiwa Dkt Charles Kimei wajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kama ambavyo wenzangu wameshaanza kuchangia. Kwanza nipongeze *flexibility* ya Serikali, sasa neno *flexibility* hapo utasema tuongee Kiswahili moja kwa moja tutasaidiana. Nipongeze utayari na hiyo *flexibility* ya Serikali namna ambavyo wameweza kuingiza mawazo ya Wajumbe wa Kamati lakini pia na wadau mbalimbali ambao wametoa maoni yao kwa maana ya watumiaji wa maji, lakini pia taasisi ambazo zinashughulika na usimamizi wa masuala ya maji. Kimsingi ndiyo jukumu la Serikali la msingi

kusikiliza na pamoja na kufanyia kazi ushauri wa wataalam, lakini pia na watu ambao wako kwenye hiyo sekta ya matumizi ya maji tukiwemo sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sasa ndiyo kazi ya Bunge tunayoizungumza, kwamba hapa sasa ndiyo tunatunga sheria na naona jukumu langu la msingi kuhakikisha kwamba tunashauri Serikali kwenye namna bora tunaweza tukatumikia watu waliotupa majukumu ya kuja humu ndani kwa ajili ya kuwawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nisaidiane na Mheshimiwa Waziri kama na yeye huu Muswada ambao tunaufanyia marekebisho unasomeka kwamba ile sheria mmei-*quote* kwenye Muswada kwamba ni *Water Resources Management Act*. Kwenye *bill* imeandikwa 2019 na sijui kama kwa Waziri pia iko hivyo, nafikiri ni tatizo la uandishi kwa sababu katika Sheria zote za Maji, Sheria ya mwaka 2019 ni *Water Supply and Sanitation Act* ndiyo ya mwaka 2019, kwa hiyo naomba hapo irekebishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi ambayo Wizara imejaribu kuyagusa katika kufanya marekebisho ya hii sheria, kuna sehemu moja ambayo wameitaja na nawapongeza sana kwa sababu wanajaribu kuingiza dunia inapokwenda mabadiliko ya tabia ya nchi na athari za kimazingira. Kifungu cha 37 kwenye sheria mama ambacho kinaeleza maeneo tengefu ya maji wameingiza na kwa kweli ni jambo zuri ambalo kwenye *bill* ni namba nane, ni jambo zuri kwa kweli nalipongeza. Kwenye Muswada ni namba nane lakini kwenye sheria mama ni namba 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo zuri na kwa kweli sisi linatuonyesha utayari wa Serikali kwenye kulinda vyanzo vya maji, kwa sababu watu wote katika sisi wananchi wote duniani humu kinachotutambulisha ambacho kinatuunganisha, kwa sababu maji yako dunia nzima, kwa hiyo jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba wanalinda vyanzo vya maji na maeneo tengefu ni jambo la kupigia mfano na tuwapongeze pia Kamati kwa kuishauri Serikali na Serikali kupokea na wamefanyia kazi, kwa hiyo yapo mazuri mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo tunataka tujenge, kuna mambo mengine wameyaweka ambayo nafikiri katika uandishi bora wa sheria kwa kipindi ambacho tunacho kuna kifungu cha 24 cha sheria mama ambacho kwenye Muswada ni kifungu cha 7 ambako wameweka sifa za Mkurugenzi wa Bonde la Maji kwa kuandika kabisa sifa:

(a) Atatakiwa awe na Shahada ya kwanza katika masuala ya maji;

(b) Anatakiwa awe na uzoefu wa miaka mitano katika nafasi za uongozi na utawala;

(c) Awe ana uelewa na uzoefu kwenye sekta ya maji; na

(d) Ama sifa nyingine zinazofanana na hizo

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitu kizuri kwa sababu hatuna uhaba wa wataalam, tuna Chuo cha Maji na wanatoa wataalam ambao ni *the best* na masuala ya uzoefu kwa sababu pia tunahitaji watu ambao *at least* wameshafanya hivyo vitu, wanajua, kwa sababu nchi hii bado inaendelea kwenda mbele na kwa sababu tunao hao watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri badala ya kuweka kwenye sheria kama ilivyo sasa hivi kwa sababu tuna kanuni, kuna *regulations,* bila kutoa chochote inaweza ikawekwa kwenye *regulation* badala ya kuwekwa kwenye sheria kama ilivyo. *The best way* ya kutunga sheria kwa sababu hata kama zipo sheria kwenye nchi yetu nyingine ambazo wameweka sifa za wataalam kwenye sheria, lakini kwa sababu hili Bunge ndiyo kazi yetu kutunga sheria, nashauri tuweke kwenye kanuni badala ya kuweka kwenye sheria, vingine vilivyobaki sina shida navyo kwenye kipengele hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 44 kwenye *Principal Act* ambapo kwenye *bill* ni kifungu cha 11 kinafutwa na kuandikwa upya na lengo lake lilikuwa ni kuweka masharti ya adhabu na kuyatambulisha makosa ya masuala ya matumizi ya maji. Najua hapa lengo lilikuwa zuri, lakini kuna maneno nitayanukuu:

"*Kwamba mtu yeyote anayetumia maji zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa kwenye kibali chake cha matumizi ya maji au anatumia maji kwa dhumuni tofauti na lile lililoidhinishwa katika kibali chake cha matumizi ya maji anatenda kosa na akipatikana na hatia, faini ni kuanzia laki tatu mpaka milioni tano au kifungo cha miezi mitatu ama miezi sita.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sawa, najua wanajaribu kubana kwa sababu hata mimi ningekuwa Waziri, huwezi kuwa wewe kazi yako kwenda kukagua tu, kwenda kuzindua mabomba ya maji sijui na nini na kuna watu wanaharibu vyanzo vya maji. Kwa hiyo najua lengo ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira ya watu kuheshimu vyanzo vya maji, lakini kuhakikisha kwamba Serikali inatimiza jukumu lake la kuhakikisha kwamba watu wanapata maji safi na salama *which is very good.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwamba mtu amezidisha matumizi ya maji tofauti na kibali alichoomba, tunajua watu wanaoshughulika na masuala ya maji huwezi kufanya *approximation* mtu akatumia maji 100 *percent* kama walivyofanya makadirio. Kwa hiyo, nilifikiri ni busara mtu ambaye ameomba kibali cha matumizi ya maji asihesabike kama amefanya kosa endapo atazidisha ila alipe kutokana na kiwango kilichozidi katika matumizi yake, kwa sababu tunaishi kwenye nchi ambayo uchumi wetu pia maji ni sehemu ya mikakati au vyanzo vya uchumi kwenye nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanafuga, watu wanalima sasa wakati mwingine huwezi kukadiria asilimia 100 ndiyo maana tunasema mtu asionekane kama ametenda kosa badala yake alipie kwa sababu tuna chagiza na tunasisimua uchumi tunaita baadae *of course* nimeleta *schedule of amendment* tunaweza tukaona namna gani ambavyo tunaweza tukashauri kiandikwe katika namna bora sana ambayo bado utaendelea kuweka mikakati, kwamba unaendelea kulinda vyanzo vya maji na matumizi ya maji lakini unatoa pia nafasi kwa Watanzania kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa sababu hata Serikali inategemea kupata mapato kutokana na shughuli za kiuchumi kwenye nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye Kifungu hicho kuna kipengele kingine ambacho kinazungumzia kutumia maji tofauti na kibali mtu alichoomba, hapa imeonekana kwamba ni kosa kama mtu ataomba kibali hiki baadaye mtu ukabadilisha matumizi. Nafikiri ilikuwa ni bora sana kama tutatafuta namna bora tusifanye kama kosa la jinai hichi kitu kwamba analazimika mtu a-*notify* Bodi ya Maji, a-*notify* kwamba amebadilisha matumizi, nafikiri Serikali ijikite kwenye umetumia kwenye kiwango ambacho uliomba utatumia na ikizidi ulipie palipozidi kuliko kwamba leo niliomba kibali cha kufanya umwagiliaji lakini nimepata fedha sehemu nataka niongeze na ufugaji nionekane kwamba nimebadilisha matumizi ya maji, nafikiri siyo sahihi ni kwenye namna tu ya uandishi mtaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema ninakubaliana na kwamba tunajaribu kutafuta namna ambapo Serikali inaweza ikafanya jukumu lake la kulinda vyanzo vya maji na matumizi sahihi ya maji. *Otherwise* niwapongeze sana Serikali na niseme tu kwamba tupo pamoja kwenye hili na nikutakie kila la kheri katika usimamiaji kwa sababu tunakufahamu ndugu yetu umekuwa ukifanya majukumu makubwa na watu wa Kamati pia tunawapongeza sana kwa sababu wameendelea kila siku bila kuchoka kutoa michango yao kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, tunaendelea na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi ya kuongea kwenye Bunge hili leo tena. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuja na Muswada huu ambao unakwenda kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji. Wote ni mashahidi kwamba maji yanahitajika kwa kila jamii, yanahitajika kwa ajili ya mifugo, kwa ajili ya kilimo na vitu vingine, kama yataondoka kama alivyochangia Mheshimiwa Kiswaga

kutatokea vurugu vita katika awamu hii katika karne inayokuja kwa sababu ya upungufu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili linalofanyika leo ni kitu muhimu sana kwa sababu tunakwenda kusimamia kuhakikisha kwamba rasilimali za maji zitaendelea kuwepo sasa na baadaye. Pia ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri katika Muswada huu nilikuwa najaribu kupitia katika *Section* Namba 23 mahali ambapo wameonesha wazi kwamba inatakiwa kupatikana elimu, imezungumziwa sana na wenzangu hapa, kama kuna mahali mara nyingi tunakosea ni mahali tunapokwenda kubadilisha, tunapokwenda kuwasimamia wananchi wetu bila kuwapatia elimu kwanza. Hawa wananchi wasipopatiwa elimu mwanzo wanashangaa kitu kipya kimekuja na bado elimu hawajapata, katika hili kwasababu kuna hoja ya *awareness,* kuna hoja ya elimu kwamba wananchi wanatakiwa wapewe kwenye *Section* No. 23 nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwasababu tunakwenda kuwaingia kitu ambacho kitawasaidia katika usimamizi wa rasilimali za maji lakini elimu itakuwa imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ninakupongeza kwenye *Section* Namba 24 ambayo imeingizwa hapo, inaonesha wazi kwamba kiwango cha elimu au elimu anayotakiwa kuwa nayo mtu ambaye ataajiriwa kuwa Kiongozi wa Bonde La Maji imebainishwa hapo, kuna watu wameonesha *Hydrology, Hydro-geology* kuna *Environmental Engineering* na *Civil Engineering.* Maana yake ni nini kama tunataka kwenda kuwapa watu waongoze mabonde haya na kusimamia maji ni lazima vilevile wayajue maji vizuri ili wanapotoa elimu iwe elimu wanayoijua, kwa hiyo nikupongeze sana kwa hili kwasababu kama unataka kutoa elimu na huyu anayekwenda kutoa elimu hana utaalam hana elimu hiyo atatoa kitu ambacho siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine niseme tu wazi nimekifurahia hapa tena ni kiwango cha uzoefu anaotakiwa kuwa nao huyu Meneja wa Bonde, huko tunapotoka na Waheshimiwa wenzangu wengi, viongozi wa mabonde wamekuwa wanaenda wanawaambia watu wahame kwenye maeneo waliyokuwa wanalima toka wanazaliwa, hii inaleta mkanganyiko maalum, kwa sababu ya uzoefu mtu hajajua anamwambia nini mtu ili aweze kuhama kwenye bonde hilo liendelee kuwa ni sehemu ya chanzo cha maji, sasa ninaamini kabisa kama hawa tunaowapeleka watakuwa wanauzoefu *at least* wa miaka mitano watakuwa wanajua nini wanakwenda kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Section No*. 44 (a) ambayo imeongezwa ambayo inaonesha kwamba kulikuwa sasa inaongezwa *Section* ambayo inahusiana na watu wanaotumia maji bila vibali, *using water without permit.* Ni sahihi kwamba Watanzania wengi hapa tulipo tunatumia maji vyovyote vile hata huko tulipo, tunapozaliwa, tunapoishi mimi nikiinuka tu Mheshimiwa Waziri natafuta maji mahali fulani naanza kutumia. Lakini sasa inaonekana kabisa kipengele Namba 44 (a) kimewekwa kwa ajili ya utumiaji wa maji bila

kibali. Maana yake sasa maji haya yatadhibitiwa kwamba tunapotaka kuyatumia tunakuwa tunajua kabisa tumetoa kibali hiki kwa ajili ya shughuli fulani na shughuli Fulani, hivyo tunaweza tukawa tume-*protect* utumiaji wa maji usio sahihi. Lakini Kifungu Namba 44 ambacho kimsingi ndiyo kimetengeneza faini kwamba kuna faini ya mtu ambaye hana kibali lakini kuna faini ya mtu ambaye ametumia maji nje ya utaratibu wa kibali alichopewa, hapa ni mahali muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kupingana na wenzangu waliosema kwamba ukishakuwa na miradi mitatu, ulipewa kibali kwamba haya maji utayatumia kwa ajili ya kunywesha ng'ombe baadaye unasema nitayatumia kwa ajili ya kumwagilia shamba, ni lazima tupate kibali ili tujue usahihi wa utumiaji wa maji haya unajulikana, isionekane kwamba mtu anaibuka tu anasema nimeongeza miradi mitano sasa maji ninatumia hivi hapana. Aombe kibali kingine cha matumizi hayo na hii sheria imeonesha bayana kwenye *Section* No. 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tu mahali ambapo naweza nikashauri ni hapa ambapo mtu anaonekana amepewa faini lakini analirudia kosa katika *section* hiyo na inaonekana huyu anapewa adhabu ya Shilingi 100,000 kila anaporudia. Hii Shilingi 100,000 kama ni mfanyabiashara mkubwa anaweza kufanya *analysis* akagundua kwamba akifanya makosa yale makosa anayoyafanya gharama ya maji ni kubwa kuliko Shilingi 100,000 atarudia tena, kwa hiyo hapa iangaliwe upya ni faini ya aina gani kwa kosa linalojirudia isiendelee kuwa hii Shilingi 100,000 inayofikiriwa, iangaliwe nini kinaweza kufanyika hapo ili kosa hilo lisijirudie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana sheria hii imezungumzia habari ya maabara, watu wetu wengi wanaugua utakuwa mtu anaugua vibarango kichwani, ukimuuliza anatatizo gani anasema watoto wangu walikuwa wanaoga tu maji kutoka kwenye kisima chetu hiki ameugua, maana yake hayo maji hayajatibiwa. Tukiwa na maabara zetu zitaonesha wazi kwamba kuna kasoro ndani ya maji haya, nini kinachokosekana nini kilichozidi, nini ambacho kinaweza kuleta athari kwa mwanadamu na tutakuwa na uhakika kwamba matibabu ya watu wetu kutokana tu na *protection* yataanza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi wakati tunayafanya haya yote kama Mwenyekiti wangu wa Kamati alivyosema, ni lazima tuhakikishe kwamba Sera yetu ya mwaka 2022 ya Maji imerekebishwa, kwa sababu lazima tuhakikishe kwamba sera inasema nini na sasa tunakwenda kufanya nini, vikipingana maana yake tutakwenda kuleta *commotion* kwenye mazingira tuliyopo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inathibitisha kwamba tunatakiwa tuwapatie watu maji ya kutosha, kwa hiyo

niseme tu Mheshimiwa Waziri kama alivyochangia Profesa Manya hapo tuhakikishe kwamba wananchi wanapata maji ili upatikanaji wa maji utupe nafasi ya kusimamia vyanzo vya maji bora na maji yaweze kupatikana hata kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa machache haya, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Festo Richard Sanga jiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nichukue pia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu anayeongoza Serikali na Wizara hii husika ambayo ameona umuhimu wa kuleta marekebisho haya ya kuboresha usimamizi wa rasilimali ya maji katika nchi yetu. Ninaamini ni jambo muhimu na ninamshukuru sana na kumpongeza Waziri wetu, Kijana wetu Mheshimiwa Jumaa Aweso, Mheshimiwa Maryprisca ambaye ni Naibu wake pamoja na Viongozi wa Wizara hii kwa umakini wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia kwamba wameshirikisha, wamepokea maoni ya wadau kuhusiana na masuala haya ambayo yanakwenda kurekebishwa na ninaamini kwamba ukiangalia utaona kwamba siyo masuala ambayo kama wangekuwa sio watu makini sana wangeweza kuyaibua lakini wameweza kuyaibua kwa sababu kweli wanataka ufanisi katika suala hili zima, ambalo mimi nimejiona kama ni sheria ambayo inapaswa kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali ya maji kwa kukabiliana na vitendo vinavyosababisha uharibifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni shughuli ambayo inaenda kudhibiti au kuhakikisha kwamba wanadamu ambao sisi tunahitaji maendeleo tunatumia vyanzo vya maji kwa namna ambayo itakuwa endelevu na ndiyo sababu kwenye hifadhi nyingine, mimi ninafikiri kwamba kwenye mabonde ni kama hifadhi tu hakuna tofauti na hifadhi nyingine wameenda mkondo ule wa kuunda hata majeshi kabisa kule ambako ni hifadhi watu wasitumie ile ardhi kwa namna ambayo itaharibu au kupoteza kabisa utajiri huu ambao Mungu ametupa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba hawa hawajaenda kwa kufuata nadharia ya kuunda majeshi kuhifadhi maji, lakini wanataka kutumia naona nadharia inayotumika na msingi wake ni ushirikishwaji wa wananchi katika kusimamia vyanzo na matumizi ya maji haya tuliyopewa. Tofauti kidogo pia ambayo ninaiona na ninashukuru kwamba Profesa Manya amezungumza mambo mazuri sana sitaki kuyarudia, nayaona kwamba kuna

umuhimu wa kufungamanisha usimamizi wa maji kwenye mabonde lakini pia tuangalie pia zile mamlaka ambazo zinasambaza maji, zile mamlaka ambazo zinasimamiwa na Mamlaka za Usambazaji Maji Mijini na Vijijini kwasababu zenyewe ndiyo zinaenda sasa kuona kwamba watu wale wanaoshirikishwa kwenye usimamizi wana motisha na wanajua namna gani na umuhimu gani wanaweza wakapata katika suala hili zima la kusimamia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia ieleweke kwamba maji yanapita kwenye mikondo, maji yanatokea kwenye chemchem mbalimbali na yanapita kwenye mashamba ya watu walikuwa wanazitumia zile chemchem kunywesha mashamba, kule kwetu ni kawaida kabisa chemchem zipo karibu hata kwenye shamba langu kuna chemchem ambayo ninaweza nikatumia, lakini ukweli ni kwamba lazima tuweze kulinda sasa haya maji yanatiririka namna gani yapelekwe kwenye maeneo ambayo yanahitajika na yatatumika kwa ufanisi zaidi katika shughuli za kibinadamu pamoja na ikiwa ni maji safi wa kunywa na pia maji ya kuendeshea shughuli mbalimbali kwenye sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaamini kuna umuhimu huo na ndiyo sababu ninaamini kuwa hii nadharia ya kushirikiana wale watu ambao wanaweza kwa urahisi sana kufikia hivi vyanzo na kuviharibu inakuwa ni jambo la msingi na ndiyo maana kwamba wenzangu waliozungumza suala zima la elimu, kutoa elimu sana kwa wananchi siyo tu wanaoishi kwenye maeneo ya vyanzo vya maji lakini pia wale ambao wanaweza wakachimba visima na wale wanoatumia. Watu wajue kwamba maji yana umuhimu, kuna maji ya kutumia kuoshea magari na kuna maji ambayo yanaweza yakatumika kunywesha mashamba, lakini siyo yale yale maji yanastahili kutumika kwa kunywa. Kwa hiyo watu wajue kwamba maji yale ambayo wanatumia kufanya shughuli zao siyo maji ambayo yangeweza kutumika kwa shughuli za watu kunywa ambayo ni msingi sana ni maji safi hayapo kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba kama nilivyosema hatuwezi kuzungumzia suala zima la usimamizi wa rasilimali maji bila kuzungumzia wale wanosambaza na maana yake ni kwamba lazima Kanuni zinazotungwa chini ya vifungu husika au huko baadae tutakapoangalia hii sera ya maji tuone kwamba namna gani wale wanaosambaza maji wanabanwa ili waweze kusambaza maji kwa namna ambayo ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hatuwezi kuondokana na ukweli kwamba, hatuwezi kutokuzungumzia gharama za kuwafikishia wananchi wetu maji kwenye nyumba zao na katika maeneo yao ya kufanyia shughuli mbalimbali, hizi gharama zimekuwa ni kero na jambo ambalo mimi ninaamini kwamba watu wanaanza sasa kukiuka kutumia yale maji kupitia mikondo husika

ambayo tunafikiri kwamba inahifadhi na badala yake wanaanza sasa kutoboa toba ili wapate maji kwa gharama ambayo ni nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naamini kwamba suala la motisha la kuhifadhi kama nilivyosema haliji endapo utasema kwamba mtu ambaye anaweza akafikia maji kwa urahisi pale alipo unaenda kumtoza Shilingi 800 kwa *unit* ambayo ni fedha kubwa kwao, wanaona kwamba pengine afadhali wapindishe yale maji yaende kwenye nyumba zao bila kulipa chochote. Kwa hiyo masuala ya gharama lazima yaangaliwe, ninaamini kwamba Naibu Waziri husika atachukua hili suala zima la kusema kwamba atafanyaje, atatumia Kanuni gani ili wale wanaosambaza wasambaze maji kwa gharama ambazo ni muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nitoe maoni yafuatayo ya kuzingatia pia, kwamba mabonde haya tumeona hayana vyanzo ambavyo vinatosheleza kwa fedha, kwa hiyo naomba kwamba ili haya mabonde yaweze kutoa elimu kama tunavyosema basi ni lazima yawezeshwe kupata rasilimali ya kutosha ya kuweza kuelimisha kutoa elimu kwenye ngazi zote kuanzia kwenye Vijiji hata kwenye Kata na kwenye Wilaya. Mabonde haya pia yapewe uwezo wa kufanya doria pengine kwa kushirikiana na Kamati za Usalama na Ulinzi kwenye maeneo yetu ili waweze kukagua vyanzo hivi vya maji na kuhakikisha kwamba hivi vyanzo vipo vinatunzwa na vinatumika kwa namna ambayo ni sahihi na maji hayachafuliwi na watu wengine wakawa wakakunywa maji chini ya bonde, maji ambayo yamechafuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya za Watumia Maji pia nafikiri kwamba watumiaji maji hususani wale wanaomwagilia wasaidiwe kuboresha miundombinu yao ya mifereji ili kuepuka matope kujaa kwenye vyanzo vile na kuhakikisha maji yale hayaendi kwenye mkondo na kwenda kwenye maeneo mengine ambayo yanahitajika maji kufika kwenye bonde hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kwamba Bonde la Mto Pangani kwa mfano, lina matatizo na wanahitaji kweli kuweza kuwawezesha wale wanotumia waweze kuboresha mifereji yao ili maji yaendelee kwenye mikondo inayostahili hata kufika kwenye Bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara ifanye maboresho kwenye bei za maji kama nilivyosema kwenye maeneo mbalimbali ili maji yawafikie watu kwa njia ambayo ni sahihi na gharama ambayo inakubalika lakini natumaini kwamba pia kwa sababu suala hili lote ni mtambuka Wizara ya Mifugo ninaamini kwamba na wao wamepitia Muswada huu. Wizara ya Mifugo wasaidie kujenga mabwawa na mabirika ya mifugo kuweza kupata maji katika nyakati zote za mwaka ili mifugo sasa isiwe inafunguliwa kwenda kuharibu vyanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayefuga akiona ng'ombe wake anakufa kwasababu ya maji anapeleka yule ng'ombe mahali popote, kwa hiyo naomba Wizara ya Maji sasa ijikite na iwezeshwe kutengeneza mabirika ya mabwawa ambayo yanaweza kusaidia sasa ng'ombe na mifugo mingine kupata maji. Pia naamini kwamba Kamati zile ambazo mnasema zitaundwa kwenye vidaka maji, zile kamati ninaomba Wizara ifikirie kuweka vigezo vya wanakamati, kwa sababu tumeona kwenye jumuiya wameweka watu kwenye jumuiya za maji za *RUWASA* ambao hawana uwezo, hawaelewi hata ni kitu gani kinafanyika, hawafanyi hesabu na hamna vitabu vinavyojitosheleza kutoa hesabu yam aji, bili zile wanazokusanya zimekuwa Shilingi ngapi, mapato na matumizi kiasi gani hela zimepelekwa kwenye Serikali Kuu kusaidia uendelevu wa miradi ya maji ambayo inatekelezwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Wizara ifikirie pia kuweka vigezo vya wanakamati, kwa sababu tumeona wameweka watu kwenye jumuiya za maji za *RUWASA* watu ambao hawana uwezo, hawaelewi hata ni kitu gani kinafanyika. Hawafanyi hesabu na hamna vitabu vinavyojitolesheleza kutoa hesabu ya kwamba maji, *bill* zile walizokusanya zimekuwa shilingi ngapi mapato na matumizi na kiasi gani hela zimepelekwa kwenye Serikali kuu kusaidia uendelevu wa miradi ya maji ambayo inatekelezwa hapa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi wajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote napenda kuipongeza Wizara ya Maji kwa kutuletea Muswada huu kwa mustakabali wa maisha ya sisi wenyewe na vizazi vyetu vijavyo na mustakabali mzima wa taifa letu katika sekta hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo yote yaliyowasilishwa kwetu na Serikali kuhusu Muswada huu wa rasilimali za maji. Nakubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kusaidia na kushiriki kwao katika kutoa maoni ya kuhakikisha kwamba Muswada huu unafanikiwa na kuleta tija kwa mustakabali wetu sisi wananchi na vizazi vyetu vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Muswada huu wa rasilimali za maji ni kwa faida yetu sisi na vizazi vijavyo. Kwasababu kumekuwa na uharibifu mkubwa katika vyanzo vya maji, lakini pia kuna upotevu mkubwa wa rasilimali za maji ambazo bado hazijawekewa sheria. Kwa muktadha huo sasa, sheria hii itasaidia utunzaji, uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za maji. Kwa sababu, kwanza niuhifadhi, pili ni kutunza na la tatu ni kulinda. Kwa hiyo, Muswada huu umekuja kwa wakati mwafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 44, kuandikwa upya naungana nacho kwa sababu ya kutenganisha kosa la mtumiaji maji ambaye ana kibali na mtumiaji wa maji ambaye hana kibali. Hapa kumekuwa na changamoto. Kwa wanaokuwa na vibali, wanakuwa na vibali lakini kwasababu anakibali anatumia zaidi ya kibali, kibali kinamruhusu afanye jambo kadhaa na kadhaa lakini yeye anaongeza mara tatu, mara nne na kupelekea uharibifu wa vyanzo vya maji. Na kwa hawa ambao hawana vibali wanatumia mwanya wa kusema kwamba wao hawaelewi, kwamba kuna sheria zinazohusu udhibiti wa vyanzo vya maji na rasilimali za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana kabisa na huu Muswada kwa kurekebisha hiki kipengele ili kuwafanya hao wenye vibali wanatumia mwanya wa kupata kibali kujinufaisha zaidi na utumiaji wa rasilimali za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 37 cha sheria mama kuongeza Kifungu Kidogo cha 4. Kifungu hiki kinahusu udhibiti wa maeneo tengefu. Tuna maeneo yetu tengefu, lakini katika maeneo haya tengefu kuna shughuli za kibinadamu bado zinaendelea kufanyika. Sasa katika kudhibiti haya maeneo tengefu sheria hii itatoa ufafanuzi wa namna ya kulinda na kudhibiti maeneo tengefu. Kwa mfano maeneo tengefu ya visiwa, visiwa vinatumika na wavuvi, wavuvi wale wanapotumia visiwa hivi ambavyo ni maeneo tengefu wengine hawajui, wengine wanajua lakini kwa kujifanya hawajui.

Kwa hivyo, elimu kuhusiana na maeneo tengefu itolewe zaidi. Kwamba wananchi wanatakiwa wajue ni sheria gani zinambana mtumiaji huyo na uharibifu gani akiufanya na adhabu gani atapata. Imewekwa adhabu kwenye Muswada huu, ni vizuri. Walichofanya ni kuongeza baadhi ya adhabu kwasababu adhabu za nyuma zilikuwa hazilingani na makosa. Makosa mengine ya uharibifu wa maji adhabu zake zinakuwa kama robo tu ya hasara. Serikali inaingia hasara kubwa kurejesha ule uharibu alioufanya yule mtumiaji wa vyanzo vya maji. Serikali inaingia hasara kubwa kuliko kile ambacho anatakiwa alipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana, kwa mfano amefanya uharibu wa gharama ya milioni 50. Serikali inataka kuingia gharama ya kurejesha ile kwa milioni 50, lakini nyuma adhabu ilikuwa; kwa mfano, kama analipa milioni moja au laki tano hapo utalinganisha uharibifu alioufanya na hasara. Sasa kwa adhabu zile ilikuwa uharibifu unaendelea kwasababu yule anayefanya uharibifu hapati madhara yoyote isipokuwa kapata faida kubwa kwa kufanya ule uharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuzungumzia kuhusu utunzaji wa rasilimali za maji. Hii ni kwa faida yetu sisi wananchi, binadamu, wanyama, miti na viumbe vingine; pia sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo, mifugo na mambo mengine ya kimaendeleo katika nchi yetu vinatumia maji. Hivyo, ni vyema sasa uhifadhi wa mazingira, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, liwe ni suala la mkazo. Katika sekta zote za Wizara zote kuwe na kifungu na fungu maalum litakalohusika na uhifadhi wa mazingira yetu ili yatusaidie kutunza nchi yetu, kutunza mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, uhifadhi wa vyanzo vyetu vya maji ambavyo ni rasilimali tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, rasilimali hii ni kwa faida yetu sote na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu utajenga mustakabali mwema wa taifa letu katika kuhifadhi vyanzo vya maji na uhifadhi wa maji kwa ujumla. Kama leo tukiupitisha Muswada huu, nashauri Serikali itoe elimu katika maeneo husika kwa njia husika, nyepesi ambazo zitawafikia walengwa huko waliko, na si tu kutumia radio na magazeti bali kuwafuata wahusika huko waliko, kujumuisha wananchi na uongozi wa pale. vilevile kutoa elimu kwa eneo lililowazunguka, ikiwa ni eneo la vyanzo vya maji ama ni eneo tengefu au ikiwa ni eneo la bonde; waelewe maana ya kutunza bonde lao, kutunza vyanzo vyao vya maji na kutunza maeneo tengefu ili kudhibiti hasara itakayotokea hapo mbele. Pia na wao wasipate adhabu ambazo hazistahiki kwa kutojua maana ya uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza taasisi isiyo ya kiserikali ya *TAWASANET,* mtandao wa maji na usafi wa mazingira Tanzania kwa juhudi zao za dhati kwa wanavyoisaidia Serikali katika shughuli mbalimbali ikiwemo kutoa elimu, kuhifadhi mazingira ya vyanzo vya maji. Mtandao huu umefanya kazi kubwa sana maeneo mbalimbali ya Tanzania. Nawapongeza sana, nawataka na wengine waendelee kusaidia nchi katika uhifadhi wa mazingira, vyanzo vya maji na utunzaji kwa ujumla wake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; nimalizie mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwekeza fedha nyingi katika sekta ya maji. Dhamira yake ya kuwekeza fedha nyingi katika sekta ya maji kumsaidia mwananchi, akiwemo

mwanamke, kupata fursa ya kupata maji katika sekta za uzalishaji, matumizi ya kibinadamu lakini kuongeza uchumi na Pato la Taifa letu kwa kupitia sekta hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuunge mkono juhudi hizo kwasababu kama ilivyosemekana, maji ni uhai, maji ni kila kitu; na kama ilivyoelezwa hapa, kwamba vita nyingine itakayokuja duniani uwezekano mkubwa ikawa vita ya maji na sisi tumepakana na mabonde, tumepakana na mito ambayo inaruunganisha na nchi nyingine jirani. Kwa hivyo, uhakiki na utumiaji sahihi wa maji ni muhimu kwa nchi yetu. Sheria zifuatwe ili kuona usawa unapatikana katika kutumia rasilimali hizi zote za maji, ikiwemo maziwa na mito kwa nchi zote ambazo tunaungana katika kutumia maji hayo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; nakushukuru kwa nafasi hii, naipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji wa majukumu mbalimbali na kusimamia rasilimali za maji pamoja na kusimamia miundombinu ya maji inayoharibiwa na kutoa adhabu inayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Tunaendelea na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Matumizi ya Rasilimali Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye marekebisho ya Kifungu Namba 37 Kipengele Namba 4, kinachozungumzia ulinzi wa maeneo ya uhifadhi wa maji *(protected zones)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme naunga mkono kazi nzuri ambayo imefanywa na Kamati pamoja na haya mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri. Kuna mwandishi mmoja ameandika, anasema *no matter how rich you are or poor you are, you can't live without water.* Kwa hiyo, ninaamini dunia nzima inategemea sana maji ili iweze kuishi. Vilevile, wanasema *no water no life, no blue no green.* Kwa hiyo tunaamini kabisa maji yanahitajika kwa wingi na yanahitajika kutunzwa zaidi katika Taifa letu na kwenye dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye marekebisho haya namba 37 kwenye kutunza vyanzo vya maji mimi niseme kwamba tuna wajibu wa kutunza maji kama Taifa. Katika marekebisho ya Sheria hii, mapendekezo yangu ilikuwa ni kuangalia maeneo tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani, kwenye marekebisho ya sheria, kwa mfano watu kama wa Makete na maeneo mengine ya milimani, Njombe maeneo kama Ludewa, sheria kama hii kuna maeneo haiwezi kufanya kazi. Hii ni kwa sababu, kwa mfano, Makete ni sehemu ya milima na kuna vijito na mito. Ndani ya mita 30 unakuta kuna makazi na mashamba ya watu. Sasa, sheria hizi zinakuja kuwabana wananchi, kwamba wahame maeneo yale kwa sababu wako ndani ya mita 60 ya maeneo ambako kuna vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa mimi, kama hii sheria ikifanya hivyo Jimbo langu la Makete lote linatakiwa liondoke. Hii ni kwa sababu wananchi wote wanaishi kwenye maeneo ya mito na kwenye vijito. vilevile wanalima kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninaomba sana, tunapotunga sheria hizi ni lazima tuangalie na kuzingatia kuwa hizi sheria haziwezi kuwa *applied* kwenye maeneo yote. Kwa sisi watu wa Makete, kwa mfano maeneo ya Ujuni, hii ni kata yenye vijiji takriban viwili, na hili eneo limezungukwa na maji, na ndiko kwenye wakulima wakubwa wanaobeba uchumi wa Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye vyanzo vya maji, ndani ya mita 30, 60, sehemu kubwa wamejenga nyumba na ndimo wanamolima. Sasa, watu wa bonde la maji wamekuja pale, na bahati mbaya, nashukuru kwamba wamekupa nafasi ya kuteua watu ambao wana uelewa; wanakuja watu wa bonde la maji wanawaambia wananchi, nyie mnatakiwa muhame na hamtalipwa chochote. Lugha kama hizo zinaumiza wananchi na zinawachonganisha na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo niombe, kwamba, lazima tuwe na sheria rafiki ambazo zinaendana na wananchi wetu na maeneo husika. Sisi hatukatai kutunza vyanzo vya maji kwa sababu sisi Makete ndio tuna *provide* maji kwenye bwawa la Mwalimu Nyerere, tunatoa kwenye Kituro, tunatoa Matamba, haya yote yanaenda kwenye bwawa la Mwalimu Nyerere. Na tumefanya hivi kwa miaka yote maji yanaelekea kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli lazima tutunze vyanzo vya maji, lakini sheria lazima iendane na wananchi wetu wanaoishi maeneo yale. Sasa hivi mimi na *DC* wangu, Mkuu wangu wa Wilaya na Mkurugenzi tunahangaikia namna ya kuweza kutuliza ghasia iliyoko kule kwa wananchi kwa sababu watu wa bonde la maji wamekwenda na lugha iliyowaumiza wananchi wangu. Wananchi wa Kijiji cha Ilolo kule nao wana changamoto hiyo. Kwa hiyo lazima tuwe na sheria ambazo ni rafiki na maeneo husika haziwezi kuwa na *applied* na maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie, kwa mfano pia marekebisho kwenye kipengele namba 44 (a), hapa inazungumzia kuhusu kosa la matumizi ya maji bila kibali. Waziri ni vyema hata hizi jumuiya za maji zikapewa uwezo wa kuelimisha wananchi. Nakupa mfano mmoja.

Nimekwenda sehemu moja inaitwa Matamba, watu wa jumuiya ya maji na wataalamu wa maji, watu wa *RUWASA,* wanawaambia wananchi kwamba haya maji sheria inasema ni kwa matumizi ya nyumbani. Sasa, mwananchi anatakiwa amwagilie nyanya na bustani zake, lakini anazuia asimwagilie kwa sababu yale maji sheria inasema ni ya matumizi ya nyumbani, akitumia anapigwa faini. Sasa, ni vema tukajikita kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taifa ambalo umwangiliaji bado haujawa katika *level* kubwa kwenye kilimo wananchi waruhusiwe kutumia maji haya kwaajili ya umwangiliaji. Kama kuna changamoto ya kwamba watatumia maji mengi ni vema Wizara sasa ikajikita kwenye kufunga mita kwa wananchi hawa ili mtu atumie kulingana na kiwango kile ambacho mita itasoma ili aweze kulipia, kuliko mwananchi anatumia kwenye umwangiliaji, anatumia kwenye kufyatua tofali, ambazo zinaleta tija kwenye ukuwaji wa uchumi wa Wilaya yangu ya Makete lakini anaenda kuzuiwa kwamba huwezi kutumia maji haya kwa sababu maji haya siyo kwa ajili ya umwangiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata hizi faini ambazo mnaweza ku-*introduce* tunaomba ziwe ni faini rafiki, lakini tusijikite kwenye kuzuia watu kutumia maji tujikite kwenye kuelimisha. Kwa hii sheria namba 44 mtu asiadhibiwe kwa kosa la kutumia maji, mtu aadhibiwe kwa kwamba alipie kile kiwango kilichozidi kwenye matumizi ya maji, siyo aadhibiwe kwanini ametumia maji mengi au kwanini ametumia maji kwa ajili ya umwagiliaji au kwanini ametumia maji kwa ajili ya kufyatua tofali, *that is not are mistake,* mtu anafanya shughuli zake za kiuchumi ili ajikwamue lakini sisi tunaenda ku-*block* kwa sheria ambazo siyo rafiki kwa taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri, ni vyema akatusaidia sana sana kujikita kwenye kuelimisha wananchi wetu kuliko kuanza kuzuia wananchi kwamba msitumie maji kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sina mambo mengi, yangu yalikuwa ni hayo, mambo mawili; mita 30, hizo mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji lazima ziwe rafiki, sisi kule Makete *his not applied.* Mtafanya jimbo langu lote liondoke Makete kwa sababu ya hizi mita 30 kwa sababu mimi niko kwenye maeneo ya milima. Ninaamini kwamba Wizara yetu ni sikivu na inachapa kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina jambo lingine na Mungu akubariki sana, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga tunaendelea na Mheshimiwa Yustina Rahhi baadaye Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatia kwa dakika tano na baadaye mtoa hoja ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hoja hii ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana Wizara ya Maji kwa kuja na Muswada huu wa kufanya marekebisho katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Ninasema hivyo kwa sababu maji ni rasilimali muhimu sana. Tunasema maji *scarce resource,* lakini maji ni muhimu sana katika maisha yetu, maji ni uhai kwa binadamu, maji ni uhai kwa Wanyama, maji ni ustawi wa mimea pamoja na mazao. Kwa hiyo, tunaweza tukasema hapa bila maji sasa kumbe hakuna uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja wakati mzuri sana. Tunaona kwamba rasilimali maji imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka. Kama tunakumbuka, kwamba kipindi nchi yetu inapata uhuru kulikuwa na wastani wa maji wa lita za ujazo takribani 10,000 kwa mwaka kwa kila Mtanzania. Lakini kwa sasa na kwa takwimu iliyopita wastani wa upatikanaji wa maji kwa Mtanzania ni mita za ujazo 2,250. Sasa nategemea kwamba hata tukipata takwimu ya sensa ya mwaka huu bado inaweza ikaonesha upatikanaji wa maji unazidi kupungua. Sababu ni nyingi tu, kwamba moja wapo ni hilo la ongezeko la binadamu lakini la rasilimalimaji ipo pale pale, wanyama rasilimalimaji ipo pale pale, shughuli za kilimo, lakini uharibifu wa vyanzo vya maji na hasa maeneo tengefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea usimamizi wa rasilimali za maji tunaongelea muundo wa kitaasisi pia na mamlaka na wajibu katika kusimamia rasilimali za maji pamoja na kudhibiti uharibifu. Sasa tumeona kwamba tuna mabonde tisa, na mabonde haya yalikuwa yakisimamiwa na maafisa mabonde. Sasa katika usimamizi mzuri tunafikiria tu kwamba tupate muundo mzuri wa taasisi wa kuweza kusimamia haya mabonde; na ndiyo maana tukasema mabonde haya sasa yasimamiwe na wakurugenzi kabisa wenye mamlaka. Sifa za kuteua hawa wakurugenzi zimeainishwa kwenye muundo huu. Kwamba, angalau basi wawe na *degree* za *hydrological, ideological degrees* na fani zinazosimamiwa na hapa. Muundo wa kazi pamoja na majukumu yanayotakiwa kufanya yameelekezwa pale ili kuwe na usimamizi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini taasisi hizi zikishuka mpaka huku chini kwenye jumuiya ya watumiaji wa maji *(water uses associations)* zilizoko vijijini na kwingine, tulikuwa tunaona kwamba nyingi zinaundwa na wanaume, au nyingine wanasema *at least* kuwe na wanawake wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sasa ninapendekeza kwamba muundo huu uletwe sheria inayotaja kwamba uwakilishi wa wanawake katika taasisi hizi unakaaje. Napendekeza angalau isiwe chini ya asilimia 30, na hata ikiwezekana wawekwe wanawake wote kwenye kamati hizi za usimamizi wa

maji. Hii ingependeza kwasababu ni watumiaji wazuri wa maji, lakini pia wapo makini katika kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nakubaliana na faini mbalimbali zilizotajwa. Ninasema hivyo kwa sababu kuna makosa kwa kweli yameelekezwa hapo. Kwa mfano, kuvamia maeneo tengefu, ndiyo tunayotegemea kulinda vyanzo vya maji, lakini watu wanavamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wakulima wetu wanaenda kulima mpaka kwenye vyanzo vya maji au wanapitisha mifugo huko. Sasa maana ya faini siyo kuwakomoa Watanzania. Tukiacha mambo haya yakaenda holela, tena hasa kwa ndugu zangu wafugaji, watavamia haya maeneo, ukimpiga faini ndogo, atalipa na kesho bado atapeleka mifugo. Anayelima anajua atalima mazao yake, ukimpiga faini ndogo, atalipa, ataendelea kulima. Kwa hiyo, nafikiri faini katika Muswada huu ni sahihi, lakini tuangalie faini ambazo zinaweza zisiwaumize sana Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faini hizo zimetajwa katika vifungu mbalimbali vya sheria hii inayorekebishwa kuanzia kifungu 44, 55, 64 na kuendelea. Ni faini inayoanzia kwenye Shilingi 300,000/= mpaka Shilingi milioni tano, maana kwa kila kosa kuna faini yake; au kifungo cha miezi mitatu mpaka miezi sita. Sasa kwa kweli imeelezwa katika makosa mbalimbali; ukichungia mifugo kuna adhabu yake, pia kuna wanaochepusha tu maji; kuna mto au bwawa anaamua kuchepusha, anamwagilia labda eneo lake anavyotaka au kuchimba visima bila kupata kibali cha mabonde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa faini hii pia imeangalia mambo mengi. Faini hii inatofautisha kati ya taasisi, hawa tunaosema *legal person,* anapaswa kuwa na faini kubwa kuliko watu wa kawaida ambao huku wanasema *natural person;* au mtu anayerudiarudia makosa, basi atakuwa na faini kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana kabisa kwamba faini hizi ziwepo kwa ajili ya ustawi wa nchi yetu, kwa ajili ya hifadhi ya mabonde haya ya maji, kwa sababu maji tunayahitaji. Pamoja na faini hizi, jambo kubwa la muhimu ni kuwaelimisha wananchi, elimu ya kuhifadhi mabonde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwenye Sera ya Maji wamesema kila kwenye mradi wa maji lazima miti ipandwe. Hata kwenye Wizara ya Ardhi nimesikia ukipewa hati ya ardhi ya nyumbani kwako, sharti mojawapo ni kupanda miti. Kwa hiyo, nafikiri tutoe wito kwa Watanzania na elimu itolewe, tuhifadhi vyanzo vya maji lakini pia tuhifadhi mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi. Tunamalizia na mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Salome Makamba kwa dakika tano, baadaye mtoa hoja atahitimisha hoja yake.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba nitofautiane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuhusiana na mapendekezo yaliyoletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni kijana na nilikuwa nategemea kwa ujana wake angeisaidia Serikali kuwafikia wananchi kwa kuwapelekea maji ya kutosha; pia angeisaidia Serikali kufanya maji kuwa sehemu ya mchango mkubwa wa kuingizia Serikali kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Ibara ya 10 anasema, mtu akitumia maji kupita kiasi alichoruhusiwa kutumia anatenda kosa na unampa adhabu takribani mpaka Shilingi milioni 10 au kifungo cha miezi sita. Mheshimiwa Waziri usiturudishe huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kutupimia kiasi cha maji cha kutumia yalikuwa ni mwaka 1980 huko ndiyo mtu alikuwa anaenda kuchukua sukari kwenye duka la Ushirika; anapimiwa sukari kilo mbili kwa sababu ana watoto wawili. Acha watu watumie maji. Unachotakiwa kufanya ni kupima *units* za mtu anazozitumia na kum-*charge* kwa *unit* kama wanavyofanya watu wa umeme. Usimwambie mtu eti katumia maji mengi, hivyo anatenda kosa, unataka umfunge jela miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaosema eti kuna vita, sidhani kama kutakuwa na vita kubwa kama kumfunga jela mtu ambaye anatumia maji kwa ajili ya familia, anatumia maji kwa ajili ya kukuza uchumi na ustawi wa familia yake, eti unamfunga jela kwa sababu kazidisha kile kiwango ulichomruhusu kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema hapa eti ni kosa mtu kubadili matumizi ya maji kutoka kwenye kile kibali alichopewa. Hivi mimi nimeomba kibali kwa ajili ya kulima, nimeona kilimo hakinilipi, nikaamua niende nikafyatue matofali, nachangia nchi, najiongezea uchumi wangu, naongeza ustawi wa Taifa. Kosa liko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane, kubadili matumizi ya maji siyo kosa na huwezi kufungwa jela kwa sababu umebadili matumizi, tunarudi nyuma balada ya kwenda mbele. Unasema ni kosa mtu kutumia maji bila kibali; amesema vizuri kaka yangu pale Mheshimiwa Sanga, hivi mtu aliyeko kijijini kule Mwamalili, anachukua mifugo yake anapeleka mtoni kwa ajili ya kwenda kunywesha mifugo yake. Anajuaje hizi habari za kibali anazoziweka

Waziri hapa? Ukiacha hivyo, aende akanyweshee wapi mifugo yake? Mheshimiwa Waziri, tengeneza miundombinu, weka mabwawa ya kunyweshea mifugo, weka mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, weka *center,* husisha sekta binafsi wakusaidie. Kama mzigo ni mkubwa kwa ajili ya kuwahudumia watu, kuwapelekea maji na maji yenyewe yapo, hivi Serikali mngepewa kazi ya kutengeneza maji! Maji ni ya Mungu, maji yapo, kazi yenu ninyi ni kuyapeleka kwa wananchi. Mngepewa kazi ya kutengeneza haya maji jamani tungekuwa tunalipa shilingi ngapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji kama yapo, kazi ni ndogo tu. Kama unaona Serikali inatumia fedha nyingi kuwapelekea wananchi huduma ya maji, huduma bora, basi usiweke faini na vikwazo. Miaka zaidi ya 60 ya uhuru kweli tunaambiana hapa, "mtu akitumia maji kupita kiasi," hivi mimi nitajuaje ng'ombe wangu anahitaji kunywa maji lita 20 na siyo lita 15? Nitajuaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitunge sheria kama vile Tanzania nzima ni Dar es Salaam au kama vile Watanzania wote wanaishi mjini. Watu wanaishi vijijini. Umetanua hapa, umeweka hii sheria imeenda mpaka kwenye mabonde ya maji, sijui maji yanayoporomoka; hivi kweli wale watu wa kule watajua haya mambo yako unayosema hapa sijui kibali, ubadilishe matumizi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akumbuke asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania wanaishi vijijini.

**MHE. ESTER BULAYA:** Eeh!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maji haya ni ya Mungu, usiwawekee watu masharti ya kutumia maji. Ndiyo maana mwingine anaoga maji ndogo ya lita 20, mwingine anaoga maji ndoo ya lita 10.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Usiweke vikwazo vya matumizi ya maji...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome subiri, kuna taarifa huku.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Alah!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eng. Mwanaisha.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, maji ni ya Mungu lakini namna ya ku-*utilize* maji ni lazima yatengenezewe utaratibu, kwa sababu *underground water resources* ni mkondo ambao una-*channels.* Kama *channel* haitakuwa *limited,* ndiyo yanayotokea, visima vinachimbwa na maji yanakauka. Serikali inaingiza fedha nyingi humo, lakini matumizi yetu mabaya yanapelekea visima kukauka. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na utaratibu wa kuzuia maji yale hata kama ni ya Mungu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba, unaipokea hiyo taarifa!

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru na bahati nzuri Bunge liko *live,* ndiyo bahati nzuri yake. Yaani ninyi mmeenda kwa wananchi kuomba kura, mkawaambia mtawapelekea maji, mkawaambia mtahikikisha wanapata maji ya kutosha, mnamtua mama ndoo kichwani, sasa hivi tunaweka sheria kwamba mtu atakayetumia maji kupita kiasi atatozwa faini ya Shilingi milioni 10 au atafungwa jela miezi sita.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi? Mheshimiwa Salome subiri kidogo. Taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu sana naomba nimpe taarifa dada yangu Mheshimiwa Salome. Kwanza sheria tunayoifanyia mabadiliko siyo ya usambazaji wa huduma za maji, tunafanya mabadiliko ya sheria ya inayo-*manage* vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, asijikite kwenye sheria ya usambazaji, hii ni sheria ya *management* ya vyanzo vya maji na ndiyo maana tunasema, kubadilisha matumizi ya maji ni lazima upewe kibali. Kile kibali maana yake ni nini? Tunakuwa tumefanya tathmini kuona kwa shughuli yako unahitaji maji kiasi gani? Ya namna gani? Unapotaka kubadilisha matumizi, utaomba kibali na sheria iko vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome naomba umalizie kwa nusu dakika.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri huyo pia ni Mbunge wa Jimbo. Kwa hiyo, watu wakiwa kwenye jimbo lake, wakitaka kutumia maji kunyweshea mifugo, yale maji ya mabondeni, yale maji ya mtoni, wanatakiwa wakaombe kibali cha kutumia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ihakikishe watu wanapata maji, itengeneze miundombinu ya watu kupata maji, ihakikishe inatengeneza mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji, kwa ajili ya kilimo, kwa ajili ya mifugo. Ihakikishe inawapelekea watu maji kwenye maeneo yao. Hakuna mtu anayependa kutoka kwake ateremshe bondeni kwenda kunywesha mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Sheria ya Maji naikubali. Changamoto yake ni kwamba inalenga kwenda kudhibiti badala ya kuboresha miundombinu ya maji kwa watu wetu. Kwa hiyo, ombi langu na rai kubwa kwa Serikali na nimeleta *schedule of amendment*. Kwanza, hizi faini ziondolewe. Ni mapema sana kuweka hizi faini kwa wananchi. Watu wataumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamesema hapa, hata haya yanayoandikwa humu hawayajui. Sisi tunajifanya tuna busara kubwa tunapochangia, lakini ukweli ni kwamba wanaoenda kutekeleza hii sheria watasimamia mkono wa chuma na watu wetu wataumia. Tufute haya masharti, watu waboreshewe miundombinu, na *automatically* tukiboresha miundombinu maji yatatumika vizuri, *automatically* tukiboresha miundombinu hakuna mtu ataenda mtoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mimi nalima, kiangazi kimekuja ghafla, nahitaji kumwagilia eneo langu kwa maji kutoka mtoni, unaniambia lazima nikaombe kibali, mazao hayasubiri kibali. Nami sikujua kama mvua itakata ghafla. Kwa hiyo, ombi langu, kwa heshima na taadhima, hii sheria imekuja mapema sana. Hivyo vyanzo vya maji tunavyotaka kuvilinda, ni kweli, lakini hawa wananchi wanapata hiyo huduma ya maji? Ofisi ya Waziri wa Maji inatekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu tu ku-*post* picha hapa niko Bungeni nikasema leo tuna Muswada wa Maji, zimekuja *comments* kibao. Watu wanasema, hata hayo maji yenyewe ukienda kuomba uvutiwe nyumbani kwako ni shughuli. Watu wanaovuta maji wamekuwa mabosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome. Naomba sasa mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake. Karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru wewe binafsi kwa mwongozo wako katika Bunge letu hili Tukufu. Pia nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Tumepata hapa michango zaidi ya Wabunge 11; Mheshimiwa Kiswaga, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Profesa Shukrani, Mheshimiwa Kimei, Mheshimiwa Festo Sanga, Mheshimiwa Khadija Aboud na Waheshimiwa wengine kama

dada yangu Mheshimiwa Salome, Mheshimiwa Nusrat na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia. Niseme tu maoni yao tumeyapokea na tunayafanyia kazi na mengine tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango, ushauri na maoni yao waliyoyatoa, yamelenga siyo kuboresha Muswada pekee, bali pia yanaonesha umuhimu mkubwa unaochukuliwa katika suala la usimamizi wa rasilimali za maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru tena Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji, ambapo kupitia mjadala huu wa leo inaonesha Serikali na Kamati ya Bunge ilivyopata muda wa kutosha kupitia na kuchambua kwa kina Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2022 *(The Water Resources Management Amendment Act, 2022)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imepokea michango, ushauri na maoni yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na yatazingatiwa katika utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiufupi naomba niseme kwamba nakubaliana na michango ya Waheshimiwa Wabunge lakini kuna jambo kubwa ambalo nimejifunza kama Waziri wa Maji. Unapokuwa kiongozi kwa maana ya Waziri wa Maji, faraja yako na hata Waheshimiwa Wabunge ni kuona unazindua mradi wa maji. Unatamani uone tu vituo vya kuchotea maji, unatamani uone matenki ya maji, lakini lazima tukubali ndugu zangu Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, kwani tuna maji kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kutoa historia fupi. Rasilimali za maji tulizokuwanazo juu ya ardhi na maji yaliyokuwa chini ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 126. Bilioni 105 ni maji yaliyokuwa juu ya ardhi na bilioni 21 ni maji yaliyokuwa chini ya ardhi. Lazima tukubali kujiuliza, mwaka 1961 tulikuwa na Watanzania takribani milioni 10. Je, leo hii tuna Watanzania wangapi? Tuna Watanzania takribani zaidi ya milioni 60 na sensa bado haijatoa majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiufupi mwaka 1961 Watanzania wale milioni 10 rasilimali tulizokuwanazo, kwa maana ya maji yaliyokuwa juu ya ardhi, mito, maziwa na maji ambayo yalikuwa chini ya ardhi ukimgawia Mtanzania aliyekuwepo kipindi kile ambao ni milioni 10 alikuwa akipata 12,600 mita za ujazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakadiria Watanzania zaidi ya milioni 60 bado sensa haijatoa takwimu, maana yake watu wameongezeka, tukiwagawia maji rasilimali ile ile tuliyokuwanayo, sasa hivi Mtanzania

anapata 2,250. Nini maana yake? Tumetoka kumgawia maji 12,600, leo ni 2,200 na kitu. Tunatambua maji yakienda zaidi ya 1,500 na kitu, nchi yetu inaingia katika *water crisis.* Nini maana yake? Ambacho ninakisema na ninachokubali, rasilimali hii ya maji imeumbwa na Mwenyezi Mungu, lakini jukumu la kulinda, kutunza na kuendeleza ni letu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pale Mara imeandika: "*Ukinipamba nitapendeza.*" Hata mke usipompamba, hata kama ni mzuri namna gani, atakongoroka tu. Kwa hiyo, tunatambua kabisa rasilimali zimeumbwa na Mungu lakini tusiache wajibu wa kulinda na kutunza rasilimali zetu za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano dhahiri kabisa. Leo Dar es Salaam tumeona kabisa tulivyoingia katika *crisis* ya maji. Mto Ruvu umekauka, umepotea, watu wanateseka, lawama imebaki kwa Serikali. Sisi kama viongozi tuna wajibu: Je, tuendelee kuumia katika maeneo kama haya? Kwa hiyo, lazima tuchukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane. Tunaweka sheria hizi siyo kwa ajili ya kuwaumiza watu. Tunaweka sheria hizi ili ku-*control* tu. Nataka niwaambie Wakurugenzi ambao wanasimamia mabonde ya maji, pamoja na sheria hizi ambazo tumezitunga, lakini tusiende kupeleka taharuki kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote tunayoyafanya, yapo mambo ambayo tumejifunza. Kabla ya haya, nilifanya ziara katika maeneo yote ya mabonde. Katika Wizara yetu tuna mabonde tisa, lakini katika kuyazungukia na kujifunza, nimejifunza mengi tu. Moja ni changamoto katika Wizara yetu na hata baadhi ya watendaji. Unaweza ukasema bonde la maji; nini maana ya bonde la maji? Bonde la maji jukumu lake ni kulinda na kutunza vyanzo vya maji. Je, mwananchi anajua hilo bonde? Mwingine anajua hilo bonde labda ni kilima kidogodogo. Kwa hiyo, kuna wajibu wa kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kubwa ambalo nakubaliana nanyi Waheshimiwa Wabunge, jamii ipo tu siku zote. Ukiishirikisha utafanikiwa, usipoishirikisha utakwama. Nikiwa mwenye dhamana katika Wizara hii ya Maji, tutashirikisha jamii na tutawashirikisha Waheshimiwa Wabunge kama tulivyoishirikisha Kamati yetu na tumekubaliana na maoni yao ambayo tumeona yana maslahi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mheshimiwa Festo Sanga pamoja na sheria hii. Hatutakuwa kikwazo kwa Wana-Makete kuhakikisha kwamba wanafanya shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa, lazima tukubali kwamba maji ni rasilimali ya Taifa. Lazima tukubali Waheshimiwa Wabunge kwamba maji ni usalama wa Taifa. Ukiwa na maji toshelevu, una uhakika wa nishati ya umeme; ukiwa na maji toshelevu una uhakika na kilimo cha umwagiliaji; unapokuwa na maji toshelevu una uhakika wa afya ya Watanzania; unapokuwa na maji toshelevu una uhakika katika shughuli za kiuchumi na hata ukiwa na maji toshelevu una uhakika wa kulinda ndoa za mama zetu. Kwa hiyo, hatuwezi kama Wizara ya Maji kupoteza ndoa za mama zetu katika kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambacho tumepata, tutaenda kukizingatia pamoja na hii sheria, na nioneshe *commitment* katika Bunge letu Tukufu ni suala la elimu. Hili tutalipa kipaumbele sana na kuwashirikisha wananchi. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tumeliona ni kweli unaweza ukawa na mifugo na unawaambia kwamba wasinywe kwenye rasilimali za maji, ataipeleka wapi mifugo? Tumekubaliana kufanya kazi pamoja na Wizara ya Mifugo kwa maana ya uchimbaji wa mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, ninyi nyote ni mashahidi. Wizara yetu ya Maji tumepata fedha nyingi na tumenunua mitambo kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa na tumeshaanza kupokea. Kwa hiyo, maeneo ambayo tunaona haya ni ya ufugaji tutachimba mabwawa, siyo kwa ajili tu ya maji ya kunywa, ni kwa ajili ya mifugo na kilimo. Kwa hiyo, hakuna sababu ya mfugaji leo kupeleka ng'ombe wake katika vyanzo vyetu vya maji. Kwa hiyo, kwa mwenendo huu tutaweza kuwasaidia wafugaji wetu na tutakuwa pia na kilimo cha uhakika katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inaenda katika uchumi ambao tunautaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tulilitolea ufafanuzi ni juu ya sifa za Wakurugenzi ambao wanateuliwa wanatakiwa wawekwe katika sheria kama dada yangu Mheshimiwa Nusrat anavyolizungumza. Sifa za msingi kwa mtu kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Bonde la Maji ni muhimu zikaainishwa kwenye sheria ili kuhakikisha kuwa sifa hizo zinaakisi malengo ya sheria na majukumu kama yalivyoainishwa kwenye sheria hiyo. Hivyo kifungu cha 24 kibaki kama kilivyo kwenye Muswada ili sifa zilizoainishwa kupewa uzito unaostahili katika utekelezaji wake kuliko kuweka katika kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimeeleza awali michango ya Wabunge tumeipokea na mingine tutawajibu kwa maandishi naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI*:*** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Aweso hoja imeungwa mkono.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hajatoa hoja.

**MWENYEKITI**: Kweli, Mheshimiwa Waziri hujatoa hoja. (*Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwie radhi, naomba kutoa hoja sasa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji hoja imeungwa mkono. Katibu tunaweza kuendelea.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Bunge Zima.

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. ZAINABU ISSA - KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022**

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 7

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 7, kina marekebisho ya Mheshimiwa Nusrat Hanje. Mheshimiwa Nusrat!

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho yangu kwenye kifungu cha 7 nayasoma hapa kama nilivyoyaandika, *by deleting the whole subclose two and rewrite it as follows; "A person a legible to be appointed as the Basin Water Director shall have to posses such academic qualification and other job-related criteria as specified in the regulations.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kutaka kufanya marekebisho haya, ni kurejea kama mwanzo nilivyozungumza wakati nachangia kwamba, hakukuwa na ulazima wa kuandika sifa za Mkurugenzi wa *Water Basins* kwa sababu tukiandika kwenye *regulations* Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kufanya marekebisho kwenye kanuni badala ya kuja kuita

tena Bunge kwa ajili ya kurekebisha upya vifungu hivi kwa sababu elimu yetu inabadilika na sheria tukitunga inaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa elimu inabadilika na leo tunaandika tunataka mtu wa shahada, kesho tutataka mtu wa *masters,* kwa sababu kila siku elimu inakuwa na tumeshasema tutatengeneza elimu yetu vizuri. Kwa hiyo nashauri tungeiweka kwenye *regulation* ili iwe rahisi kufanya *amendment*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naona anataka kukusaidia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa *schedule of amendment* ambayo imeletwa na dada yangu Nusrat, lakini nikirejea maelezo ya Mheshimiwa Waziri wakati ana-*respond* katika hoja na tukiangalia utamaduni wa sheria nyingi ambazo tumezitunga humu, suala la mtendaji kuainishwa kwa mujibu wa sheria ni jambo la msingi sana. Ukiliweka katika kanuni maana yake unafanya *discretion* ya kutengeneza kanuni, lakini ukiona *minimum qualification in degree holder* hili jambo linaleta afya zaidi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria zote zilizotungwa humu ndani kwa uelewa wangu jambo hili nadhani kwa jinsi Muswada ulivyokuja ninaomba libaki kama lilivyo kama Waziri alivyolileta**.**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje**.**

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti *too longs don't make it right.* Bunge hili ni jukumu letu kutunga sheria na tuna sheria inabadilika na inakua kila siku, nashauri *the better way* hata kama zipo sheria natambua ziko baadhi ya sheria ambazo wameweka *criteria* na sifa za watu kama Wakurugenzi na watu wengine ambao ni watendaji kwenye eneo mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pendekezo langu ni zuri wala sina nia mbaya, ninachojaribu kutunga *the best laws* kutoka hapa kwenda mbele. Nashauri, wachukue pendekezo langu, sababu litatusaidia pia hata kuokoa gharama za kuja kuleta tena Muswada kujadili wakati Waziri anaweza akarekebisha kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje kifungu chako kinasema *shall have to posses such academic qualification* sio *qualifications,* moja maana yake halafu, *and other job-related criteria,* hii kazi unampa nani ya kuweka *hizi other job -related criteria,* yaani Waziri akakae, akaweke kwenye kanuni kila anachotaka yeye bila kumpa mwongozo. Maana sisi ndio tunatunga sheria, kwa nini tunataka Waziri ndio tumpe haya mamlaka ya kwenda kuamua hizo *other job criteria* yaani yeye akatafute *criteria* mahali, wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Hanje si ndio tunatunga sheria hapa. Hizi *other* yeye ataenda kuzipata wapi yaani tunamtuma yeye akazitazame wapi ambako zipo akazichukue azilete hapa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ana bodi ambayo anafanya nayo kazi na inaweza kumshauri.

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, sawa yeye ameshaeleza na akizungumza mara ya pili hajakusudia kwamba jambo lake lijadiliwe.

Waheshimiwa Wabunge, hiki kifungu hakina mabadiliko ya Serikali, kina mabadiliko ya Mheshimiwa Nusrat Hanje, kwa hiyo nitawahoji kuhusiana na hayo mabadiliko ya Mheshimiwa Hanje.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu changu ni cha 11 ambacho kwenye sheria mama ni cha 44.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje karatasi ambayo ninayo hapa ya marekebisho imeandikwa *in* clause *10 by deleting the content of* clause *44 and subsisting for them with the following,* nasoma hii ya kwako niliyonayo hapa.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yes.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo haikuwa hapa, umekosea?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni cha 10 hicho.

**MWENYEKITI:** Si ndio tuko hapa?

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio naomba niendelee, nikisome.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema by deleting *the content of close 44 ya Principle Act* ambayo ni clause 10 kwenye *bill and subsisting for them with the following; "(i) Any person who uses water in excess of amount authorized in the water permit, shall have to pay the excess amount of water used in such rate of money as such out in the regulations."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni ile ambayo mwanzo nilizungumza kwamba isiwe kosa mtu kutumia zaidi ya *amount* ambayo ipo kwenye *water permit* na lengo likiwa ni kwamba watu walipe ile kiasi cha ziada iwe ni sehemu pia kama Serikali kuona namna gani ambavyo wanaweza wakachochomoa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *aim* ni kutojinaisha matumizi ya ziada ya maji badala yake tuyaweke kwenye upande wa *finance,* watu waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili yake isomeke:

*"(ii) Any person who intends to use water for a purpose other than the other specified in the water use permit, shall have to notify the Basin Water Director except that, the amount of water to be use in the other project shall not exceed the one authorized in the water use permit."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ijikite kwenye kuangalia je, huyu mtumizi, isijikite kwenye kuangalia kwamba amebadilisha matumizi, hapana, tuna shughuli nyingi za kufanya, lakini Serikali ijikite kwenye tulichosema utatumia ndio umetumia hicho na kama kilizidi ulipe, kwa hiyo tunasomeka kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kifungu cha 44(i), matumizi ya maji zaidi ya kiasi kilichoruhusiwa kwenye kibali sio tu ni ukiukwaji wa sheria, bali pia kunaathiri kwa kiasi kikubwa watumiaji wengine, hivyo kuleta changamoto kubwa katika ugawaji wa maji kwenye vyanzo, mtu aliyekiuka sheria hutakiwa kulipia kiasi cha maji aliyotumia peke yake hakutaleta hamasa na tija katika usimamizi wa rasilimali za maji na uzingatiaji wa sheria. Hivyo kifungu cha 44 kibaki kama kilivyo kwenye Muswada.

Mheshimwa Mwenyekiti, pia suala la maombi ya kibali cha matumizi ya maji ikiwa ni pamoja na kubadilisha matumizi imeshaelezwa kwenye masharti mengine ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura 331, kifungu cha 71 na kanuni zake. Kwa kuwa mapendekezo yaliyotolewa na yameshazingatiwa kwenye sheria kifungu cha 44 kibaki kama kilivyo kwenye Muswada ili adhabu ziweze kutolewa kwa mtu ambaye hatazingatia utaratibu wa sheria kwa kubadilisha matumizi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *in the name of* watumizi wengine wa maji kutokuathirika na-*drop* ya kwanza, lakini ya pili nafikiri Serikali iendelee kuangalia namna gani ambavyo tunaweza kufanya hapa, lakini kwa sababu ya watumizi wengine, naomba ni-*drop* hii kwa sababu maelezo ya Mheshimiwa Waziri nimeyaelewa kwamba *aim* ni kwamba kuna wengine walikuwa wanapata, wengine wanakosa kwa sababu wengine wamebadilisha matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vingine wakielezea kama hivi ndio tunaweza tukaelewa na tuka-*move on.*

**MWENYEKITI:** Vizuri. Nadhani Waheshimiwa Wabunge, mmemsikia Mheshimiwa Nusrat Hanje lakini wale wa Kamati nadhani wao huwa wanapata fursa ya kwenda huko na huko kuna watu wanapewa vibali vya kumwagilia na yeye anakuwa mbele ya mto ulikoanzia. Sasa yeye akichukua maji yote halafu akasema analipa wenzie kule chini watatumia nini na akasema shida si ni kulipa, nimetumia maji na nina utayari wa kulipa, kwa hiyo namshukuru Mheshimiwa Nusrat ameelewa maelezo ya ziada yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri.

Marekebisho mengine, Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye kifungu hiki cha 10 mapendekezo yangu niliomba kifutwe, kisiwepo kabisa na sababu zangu ni hizi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kifungu hiki cha 10 kinaongelea habari ya kutumia maji zaidi ya kibali kama alivyokuwa anaeleza Mheshimiwa Nusrat. Kwa Tanzania ya leo miaka 60 ya uhuru, mtu kutumia maji kupita kiasi sidhani kama ni jambo tunatakiwa tulijadili, kazi ya Serikali inatakiwa ipeleke maji *as much as possible* kama ambavyo iliyo kwenye

umeme sababu hii ni huduma kama ilivyo kwenye madawa yaani mtu akiumwa huwezi kusema unakunywa dawa nyingi kupita kiasi wenzako watakosa. Hapana, hiyo ifutwe. Hiyo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja, anasema eti wana mpango wa kutengeza mabwawa, wameshirikiana na Wizara ya Mifugo. Sasa kama wana mpango na hawajatengeneza mabwawa kwa nini wanaweka hizi faini kubwa namna hii, hii ni hatari, kwa sababu hiki kifungu kidogo (a) kinasema mtu aliyetumia maji kupita kiasi hatatozwa fani kuanzia laki tatu mpaka milioni tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kinachofuata kinasema atatozwa kama ni *legal person* kwa makampuni au taasisi atatozwa faini si chini ya milioni tano. Kama hoja maji hayatoshi, sisi ndio kazi yetu kulishauri Bunge lifanye nini wa-*involve private sector,* lakini kusema tunaweka hizi faini eti kwa sababu hazitatumika vibaya sio kweli. Wanaokwenda kutekeleza kusimamia ni watumishi, watatekeleza kama tunavyowaelekeza na hili litawaumiza wananchi wetu, ni *very premature* kuweka adhabu kubwa namna hii eti kwa mtu ambaye na Waziri amekubali, asilimia zaidi ya 80…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome hebu tusaidie ni matumizi gani ya maji unayozungumzia ambayo unaona hayana athari mtu akitumia zaidi kile kibali yaani ni matumizi gani, ni matumizi ya nyumbani badala ya ndoo 40 katumia 60 au ni matumizi ya aina gani unayoyazungumza, yaani kwamba mtu ametumia maji kufanya nini ili nielewe vizuri hoja yako.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kumwagilia kuna watu wako wanalima mabondeni na nimetoa mfano kwenye mchango wangu.

**MWENYEKITI:** Sasa ngoja nikusaidie hiyo ya kumwagilia umeenda vizuri kabisa. Kwenye umwagiliaji kuna mtu ana shamba kubwa, mwingine ana shamba dogo, mwenye shamba dogo yuko mbele ya yule mwenye shamba kubwa, amepewa kibali cha maji yanayotosheleza shamba lake kubwa, ameamua kuongeza ukubwa wa shamba, yule mwenye shamba dogo kule nyuma maji hayaendi kwa sababu huyu katumia zaidi ya yale anayoruhusiwa. *(Makofi)*

Yule unayemtetea wewe kati ya hawa wawili unamtetea yupi, kwamba huyu mwenye kubwa kwa sababu anao uwezo wa kulipia kibali, alipie kibali chake yaani aje alipe ile adhabu, halafu yule wa kule mwingine hata asipopata ni sawa, kwa sababu yeye anaweza akaenda kuomba sijui sasa msaada kwa huyu mwingine, hebu tueleweshe vizuri maana umetaja kumwagilia. Tuseme wanatumia mto labda, twende hapo kwenye kumwagilia.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umetuongoza vizuri sana. Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha alijibu hoja yangu ya hao watu wa kilimo na watu wa mifugo ambao mtu wa mifugo hawezi kujua leo ng'ombe wangu atakunywa lita 15 au lita 30 hajui mtu wa kilimo hawezi kujua kwamba mvua zitakatika ghafla natakiwa nimwagilie kutoka mtoni akajibu hivi, yeye na Wizara ya Mifugo watashirikiana kutengeneza mabwawa na miundombinu ya kutosha kwa ajili ya kuwasadia wakulima na wafugaji, nami nimekubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo kwa nini sasa wasisitishe hizi adhabu mpaka watakapotekeleza mpango huo wa kuhakikisha kuna maji ya kutosha kwa ajili ya kilimo, kuna maji ya kutosha kwa ajili mifugo ili tusilete taharuki au tusifanye sheria hizi kandamizi kuwaumiza wananchi wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni uelewa tu hapa, kitu ambacho tunakizungumza katika sheria hii ni namna ya ku-*control* yale matumizi ya maji. Kwa mfano umwagiliaji maji yanatoka mashariki yanakwenda magharibi na watu wote wanatakiwa wapate kulingana na viwango vile walivyopangiwa na huyu mmoja atakapozidisha maana yake nje tu ya hiyo faini amenyima haki watu wengine kuendelea kuyatumia yale maji. Kwa hiyo, lengo kubwa la sheria hii ni kutoa katazo la kutotumia maji kwa sababu ya uwezo ulionao ili wote mpate kulingana na *request* yenu ambayo mliombea maji yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani hakuna athari ambayo inaweza ikasema basi mwenye haki ya fedha nyingi tumwache awabane wengine, bado tutakuja tena hapa tutakaa na kusema tuliunda sheria kandamizi kwa sababu inampa haki tajiri kuendelea kutumia maji yote yale. Kwa hivyo nadhani Mheshimiwa Makamba akubaliane na mawazo ya Serikali kwa sababu shida kubwa tunataka ku-*control* matumizi ya maji ili watu wote waweze kupata manufaa yanayolingana ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajenga nchi moja. Kwanza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameninukuu vibaya, mimi sijashauri anayeweza kulipa zaidi apate zaidi, hapana. Nimesema kifungu chote kifutwe kwa maana gani? Kwanza ni *premature,* hiyo miundombinu hamjaitengeneza bado, halafu hauwezi kuwapelekea watu adhabu kwa sababu nyinyi mmeshindwa kutengeneza miundombinu ya watu kupata maji, yaani mnaweka adhabu kwa sababu miundombinu iliyoko isiyofaa inasema kwamba mtu wa mwanzoni atapata maji mengi wa mwishoni hapati.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Ndio.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome tuko kwenye ngazi ya kutunga sheria, kifungu unachotaka kifutwe kinazungumzia matumizi ya ziada ya maji na ukishatumia ziada, adhabu imewekwa kama wewe ni kampuni au ni mtu binafsi. Kwa hivyo haya maelezo ya ziada yaani kwenye ngazi hii hayapo, yaani wewe hukitaki hiki kifungu kwa sababu kinampa adhabu mtu aliyetumia maji zaidi. Kwa hiyo maelezo yaliyotoka ni kama maelezo yako uliyoyatoa tu hayana tofauti. Sasa kwa ngazi hii kwa sababu hujakusudia kutoa hoja, ulikuwa umemaliza kuongea ama bado kwa sababu…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nilikuwa namalizia kuongea.

**SPIKA:** Haya dakika moja.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaniunga mkono? Mimi siwezi kutoa hoja nisije nikaonekana kilaza hapa. Mimi ushauri wangu Kifungu hiki yaani kujadili leo huduma ya maji, kwamba huyu mtu kazidisha huyu hajazidisha ni sawa nakusema mtu ametumia dawa nyingi wengine watakosa au ni sawa sawa na kusema mtu ametumia umeme mwingi wengine watakosa, kujadili siyo *issue*, *issue* iliyopo hiki Kifungu kimekuja mapema..

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli Mheshimiwa Makamba amesukuma kwa nguvu kubwa hii hoja, kama kuna mtu huko nje anasikiliza hivi anaweza akaona anaongea kitu kikubwa sana na sisi wengine wote tumenyamaza hapa hatuna wananchi wetu watakaoumia kutokana na sheria hii, ndiyo maana ana-*refer* sana toka tupate uhuru mmeshindwa kuwapa watu maji halafu muwapangie namna ya kutumia, ndiyo! Tulipopata uhuru tulikuwa wachache, leo hii tuko wengi na rasilimali za maji zimebaki kuwa zile zile, ndiyo tumetajiwa kiwango cha maji tulichonacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Makamba pale alipotoka babu yako Kijiji cha Kitati, Jimbo la Kibakwe na Kijiji cha Lumuma tukiweka huu utaratibu unaosema tufute hiki Kifungu, wanaendelea kugombana kila siku maji hayatoshi, watu wameongezeka shughuli za wakulima zimeongezeka lakini mto ni mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninautoa huu mfano kwa sababu Makamba ndiko anapotoka, yeye Kijiji chao Makamba kinaitwa Kitati kipo kwa chini, maji yanatokea Lumuma ule Mto unaitwa Lumuma, wale wakina Kibozi na wengine wakisema wachukue yale maji yote kwa sababu wanatumia maji toka tupate uhuru, sasa Mto ndiyo ule ule maji ndiyo yale yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo maji ya kuwapelekea, unajua tatizo hapa mmeshindwa kuelewa hoja, hoja ni kwamba tunazungumzia *water sources* hatuzungumzii *supply* ya maji. Mme-*miss* basi tu mnashindwa kuwa wakorofi wa kusema vibaya lakini *you have missed the point* kwamba hapa *we are talking of water sources* siyo *supply of water,* maji nyumbani kwako wewe tumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia huwezi ukawa nyumbani kwako umepata mita ya kutumia nyumbani kwako na familia yako halafu Aweso amekufungia maji, wewe kule ndani unawaza kiwanda cha kuzalisha maji ya kuuza! Sasa hapo lazima upate kibali na ile *access* tumesema hatukuzuii ila ubadilishe kile kibali upate kibali kingine cha kufanya hiyo shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukianza kusema toka tupate uhuru mmeshindwa kuwapa maji, unatusukumia jambo gumu. Kwa hiyo, nikueleze tu Mheshimiwa Salome Makamba tunakuomba uunge mkono hiki Kifungu Kibaki, kwa sababu ukifanya hivyo yale mashamba ya Babu yako Makamba yatakauka yote, maji kule Lumuma watu watamaliza huku hawatapata maji

na wewe kule Kijijini itabidi muhame sasa utaenda wapi na kule ndiyo kwenu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba kengele ilishagonga, nilikuwa nimekupa dakika moja, sekunde thelathini malizia.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya uhuru tulikuwa wachache, sasa hivi tumekuwa wengi na hata wakati wa uhuru Baraza la Mawaziri walikuwa wachache sasa hivi wamekuwa wengi, *assumption* ni kwamba uwezo wa ukuishauri Serikali namna ya kutatua changamoto ya maji umeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hiki Kifungu kifutwe kwa sababu adhabu tunazoziweka ni lazima zitaenda kuwaumiza wananchi hakuna mwananchi atakubali kuona mfugo wake unakufa kwa kiu, eti kwa sababu ameambiwa akienda kunyweshea kwenye chanzo cha maji atatumia maji yaliyopita kiasi. Kama mnapiga kura tupige lakini ukweli ni kwamba hiki Kifungu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome unacho hicho Kifungu hapo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ili tusitumie picha ambayo haina uhalisia huko nje.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Kifungu kinasema hivi: *any person who uses water in excess of amount authorize in the water use permit,* ni nani ambaye huwa anaomba *permit* ni mtumiaji wa maji wa aina gani. Ni mtumiaji wa aina gani, kwa hiyo tusitume picha huko nje kana kwamba yaani kuna kila mtu nchi hii kutumia maji anahitaji kibali hapana! haina huo uhalisia. Inaongelea mtumiaji wa maji ambaye kwa kawaida huwa ana kibali sasa ametumia zaidi ya kibali chake na sisi nchi hii tunawafahamu wanaohitaji vibali kutumia maji, siyo kila mtumiaji wa maji anahitaji kibali. Kwa hiyo, isitumwe hiyo picha huko nje kana kwamba sasa hiki Kifungu kimewekwa kila anayetumia maji anahitaji kibali au kwamba Serikali imetoa vibali huko basi sasa kila mtu sasa akapange foleni hapana! siyo matumizi yote ya maji yanayo vibali, wanaongelea mwenye kibali ambaye kaomba maji kiasi fulani na ametumia zaidi awe na kiwanda na nini, awe na chochote na shamba na kila mtu, hiyo ndiyo picha halisi ya hiki Kifungu na siyo nje ya hapo. Kwamba sasa mtu umesema hapo ng'ombe wake wawili watakufa huyo wa ng'ombe wawili hana kibali hajawahi kuomba kibali ataendelea na maisha yake kama yalivyo sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo picha halisi na ndivyo Kifungu kinachosema hapo. Sasa tusije tukatuma ujumbe huko nje ambao siyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salome ninakupongeza kwa maelezo ila sasa kidogo hapo kwenye ng'ombe wawili na maelezo mengine ni ya ziada.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha sekunde 30 umetumia kumjibu wa taarifa badala ya kujenga hoja yako. Ahsante sana.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 11

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba Kifungu cha 11.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo pale pale kwenye suala la faini, Kifungu hiki kinaongelea matumizi ya maji bila kibali. Kwenye Kifungu hiki cha matumizi ya maji bila kibali kwa *consideration* ile ile kwamba, kuna watumiaji wa maji Jimbo la Shinyanga Mjini Kata ya Mwamalili kuna watu wanalima kwenye bonde ambalo ni chanzo cha maji na wanalipa Laki Saba mpaka Laki Tisa kwa mwaka kupata kibali cha ku-*tap* maji kutoka kwenye bonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwafikiria watu wangu wale wa mamalili na watu wengine wa nchi nzima ambao wanafanya shughuli hizo kuwatoza faini kwamba alitumia maji bila kibali naomba nisome kwa kunukuu: "*in case the offender is a natural person be liable to a fine not less than Two Million Shillings but not exceeding Ten Million*" akaenda mbele zaidi kwa upande wa taasisi sina shida, shida yangu mtu wa kawaida hii faini ni kubwa. Kwa hiyo, mapendekezo yangu naomba tubadilishe kiwango kutoka Shilingi Milioni Mbili mpaka Shilingi Milioni 10 ije Shilingi 500,000 mpaka Shilingi Milioni Mbili, kwa ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kwa ajili ya maslahi ya Watanzania wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu maslahi wote tuko hapa kwa ajili ya maslahi ya Watanzania. Mimi nataka kuelewa jambo moja Mheshimiwa Salome Makamba, nadhani mwaka jana Waziri Mkuu alifanya ziara Pwani Mto Ruvu ulikuwa unataka kukauka na kimsingi Dar es Salaam ilikuwa uwe mgao wa hatari. Waziri Mkuu akaenda pale, Wataalam wakaenda huku na huku wakakuta watu wamejitengenezea Mito kwenda kwenye mashamba yao. Sasa hiki Kifungu kinasema: *A person who diverts* yaani mto ulikuwa unakwenda kushoto wewe umeamua kuupeleka kulia au karibu na kulia kidogo *impounds, store, abstracts or uses water without water use permit*

*commit an offence,* unataka mtu yule aliyeamisha mto, yaani hii Milioni Mbili iliyowekwa hapa awekewe 500,000 amehamisha mto, hichi kifungu sijui kama na wewe unacho hapo Mheshimiwa Salome, maana wewe umeenda moja kwa moja kwenye adhabu kabla hapo mwanzo hujasoma atakuwa amefanya kosa gani? Hapo mwanzo umepasoma kweli Mheshimiwa?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Umesoma na unaona mtu anaye-*divert* adaiwe Laki Tano? *(Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza kutoa maelezo ya ziada.

**MWENYEKITI:** Utoe maelezo ya ziada lakini ule mfano ulioutumia wa huko Jimboni ama Shinyanga Mjini hauna uhalisia kwenye Kifungu hiki kwa hiyo, wewe endelea na maelezo yako lakini hebu liweke jambo hili sawasawa tukuelewe kwa nini unataka tupunguze adhabu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Na mimi naheshimu sana mwongozo wako najua na ndiyo maana naendelea kukua kila siku. Mheshimiwa Mwenyekiti tunapotunga Sheria ya nchi tunatunga Sheria ya nchi kuangalia uwezo na hali za watu wenyewe. Kama kulikuwa kuna *concern* ya Ruvu tunayo *Local Government Authority* wangetunga Sheria ya Ruvu na watu wa Dar es Salaam. Hii Sheria ni Sheria ya nchi na ndiyo maana …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome ukishaitwa unasikiliza.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Sheria inasema *Water Resources Management Act, Water Resources* ni Sheria ya Bunge *Local Government* kila mtu ajitengenezee, kila mtu na maeneo yake, sasa jamani tutafika kweli. Hii ni *Water Resources Management Act,* ndiyo tunayo-*amend* sasa mtu nimeuliza tu swali jepesi mtu aliyehamisha Mto adaiwe Laki Tano? Na anataka kusababisha watu mamilioni wasipate maji.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nisikilize tu utanielewa. Mimi …

**MWENYEKITI:** Nataka nikusikilize umesema wewe mwenyewe vizuri kwamba Bunge lipo *live*. Nataka nikusikilize na watu kule nje wawe wanapata picha halisi.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani hamna shida.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, lazima tuelezane vizuri.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyotunga sheria tunatunga sheria ya nchi, mtu wa kawaida kwenda kumtoza faini ya Milioni Mbili mpaka Milioni Kumi, Mtanzania wa kawaida mimi kwangu naona ni hela nyingi.

**MWENYEKITI:** Huyo wa kawaida anakuwa anafanya shughuli gani? Ngoja tuende taratibu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa si ungenisikiliza nimalize.

**MWENYEKITI:** Subiri, subiri! Huyo Mtanzania wa kawaida anayefanya shughuli yake itakayompelekea yeye ku-*divert* Mto wote ni nani? Na huyo ni Mtanzania wa kawaida kweli? Kwanza ana nguvu gani za kujenga miundombinu ya kuhamisha Mto? Huyu ni Mtanzania wa kawaida huyu, simenti kapata wapi, mawe kapeleka na *lory* gani ya kuzuia Mto?

Mheshimiwa Makamba. Nilikuona Mheshimiwa Kimei lakini ngoja kwanza nimemuuliza swali. Huyu Mtanzania wa kawaida anayemzungumzia anayeweza kuhamisha Mto.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza neno Mto wote umeliongeza wewe haliko kwenye Sheria, hawajaandika mto wote, wamesema na nitasoma. Wamesema …

**MWENYEKITI:** Ngoja.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** *Diverts* anaweza ku-*divert* nini? *(Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh hawajasema *divert the whole river.*

**MWENYEKITI:** Ngoja, unachoweza ku-*divert* ni kitu gani? Kisima.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes.* Hakuna sehemu iliyoandikwa mtu ana-*divert* kwanza huwezi ku-*divert* Mto wote, haiwezekani.

**MWENYEKITI:** Soma hapa juu Mheshimiwa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inavyosomeka hapa..

**MWENYEKITI:** Ngoja, ulifuatilia ile ziara ya Waziri Mkuu maana unasema huwezi ku-*divert* Mto wote, ulifuatilia?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatunga sheria umesema mwenyewe.

**MWENYEKITI:** Subiri ulifuatilia? Umeleta mwenyewe hoja ya watu wako Jimboni, ulifuatilia ile ziara Mheshimiwa Salome?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Hukufuatilia, ndiyo maana hujui kama mtu anao uwezo wa kuhamisha Mto wote. Kwa hiyo, kwa sababu sisi tunao…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huku hawajaandika Mto wote hiyo Mto wote ni ya kwako, humu wameandika tu ni *dam* ambao…

**MWENYEKITI:** Neno *diverts* maana yake nini?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haijaandikwa mto wote! Sasa ndiyo wote?

**MWENYEKITI:** Aah kwa hiyo, akihamisha sehemu ya mto ni Mtanzania wa kawaida na ni sawa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si ungeniacha nikajenga hoja kwa sababu najua mwisho wa siku hoja yangu mimi ndiyo inashawishi Bunge.

**MWENYEKITI:** Hoja yako unaijenga unapeleka picha siyo, tupo kwenye kutunga sheria soma Kifungu…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hata kama siyo, si tuna uhuru wa kutoa maoni.

**MWENYEKITI:** Soma Kifungu kinachosema, tupo kutunga sheria.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasoma.

**MWENYEKITI:** Tupo kutunga Sheria, soma Kifungu ndiyo tuelewane hapo ndiyo maana nilikwambia umeenda moja kwa moja kwenye adhabu bila kushughulika na sehemu ambayo inaanzisha adhabu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana mimi nimesoma Muswada wote na nitausoma tena.

**MWENYEKITI:** Soma tangu mwanzo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema nianze *the principal Act, is amended by adding immediately after section 44 the following; 44A (1) A person who diverts, dams, impounds, store, abstracts or uses…*

**MWENYEKITI:** Subiri, baada ya neno *diverts* kuna koma usiseme *diverts dams* kuna koma maana yake hayo ni maneno tofauti yanajitegemea.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. A *person who diverts,* naweka koma hamna shida. *A person who diverts, dams, impounds, store, abstracts or uses water without water use permit commits an offence and shall on conviction* niendelee … *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Endelea si ndiyo kwenye hoja yako?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ….*an offence and shall, on conviction: - (a) in case the offender is a natural person be liable to a fine not less than Two Million Shillings but not exceeding Ten Million Shillings or to imprisonment for a term of not less than Three Months but not exceeding Six Months.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoelewa mtu anaye-*diverts* au hayo mambo mengine yatakayofanyika kwenye chanzo cha maji ndiyo atapewa hiyo faini na huo ndiyo msingi wa hoja yangu. Kwamba ukisema mtu ambaye anatumia *water permit without ….*

**MWENYEKITI:** Sawa eeh! Ngoja ili twende vizuri, Mheshimiwa Salome ili tuende vizuri haya maneno nilikukumbusha kuhusu koma. Maana yake hiki Kifungu unaweza kusoma hivi: *A person who diverts water without water use permit commits an offence. What sort of water can you divert if it is not a river? Can you divert any other form of water, can you?*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamba malizia hoja yako sekunde thelathini.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia hoja yangu, mtu wa kawaida *a natural person* kumchaji Shilingi Milioni mpaka Kumi kwa sababu tu ame-*divert,* amefanya *dam,* ame- *impounds, ame-store,*kutunza ame-*abstract* au ametumia maji bila kibali ni adhabu kubwa na mapendekezo yangu badala ya …

**MWENYEKITI:** *Dam* ni nini Mheshimiwa Salome? W*hat is a dam*?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni *dam*.

**MWENYEKITI:** Aah *what is a dam?*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ili mpitishe. Badala ya kumchaji Milioni Mbili mpaka Milioni Kumi mtu yule adhabu iwe Laki Tano mpaka Milioni Mbili, hayo ni mapendekezo yangu unaweza kutuhoji inawezekana kuna wengine wananiunga mkono.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu cha 11kina marekebisho ya Serikali na kina marekebisho ya Mheshimiwa Salome Makamba. Anayeafiki marekebisho ya Mheshimiwa Salome Makamba ya kupunguza adhabu kwa mtu ambaye amefanya haya makosa yaliyotajwa hapa aseme ndiyo,

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Wasiyoafiki waseme siyo,

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani waliosema siyo wameshinda. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho ya Serikali)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 22 Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwenye Kifungu hiki cha 22 naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuhusisha wanawake kwenye Kamati hizi mbalimbali za maji. Mapendekezo yangu ni madogo tu kwa sababu wamehusisha wanawake ambao naona *it's a valid reason,* kwanza wanawake na watoto na nini hivyo, ushauri wangu ningependa waongeze watu ambao wanaishi na ulemavu, wapate uwakilishi kwenye hizo Kamati za Maji. Kwenye mabadiliko yangu nimeandika maneno yafuatayo: … *in paragraph 5 (1) by adding the words at least two members shall be women and one member a person with disability immediately after the word members.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nitoe ufafanuzi Kamati za Usimamizi ni vyombo vya usimamizi wa jumuiya za maji ambazo zipo katika vyanzo vya maji ambapo baadhi ya maeneo ya vyanzo vya maji anaweza asipatikane mtu mwenye ulemavu ili kuwa sehemu ya Wajumbe ni vema suala hili likaachwa kwa mamlaka za uteuzi ili waweze kuzingatia uwakilishi huo pale panapokuwa na mtu mwenye ulemavu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri, na ndiyo maana likawekwa neno *at least, not shall, its not compulsory,* lakini *at least.* Kwamba *consideration* ya walemavu iwepo, wawekwe, lakini kama wasipokuwepo basi kuwe kuna *justification.* Hii itamsaidia hata yeye kwenda kusimamia; kwamba jamani, mliambiwa

angalau muweke mtu anayeishi na ulemavu; mlishindwa kumtafuta? Watamwambia wao Njombe yote hakuna watu wa *design* hiyo. Basi sawa. Lakini asipoweka kwenye sheria hawezi kuhoji, watasema siyo takwa la kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi sioni; halafu mwisho wa siku chukua hii, haina shida yoyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome Makamba, wazo ni zuri sana, isipokuwa kwa maelezo aliyoyasema Waziri hapa na kwa kuangalia kwamba hizi *management committees* ambazo zinaelezwa hapa ni zile ambazo ni za maeneo husika. Sasa umesema vizuri, umeweka neno *at least,* maana yake *a minimum of, you can't go below that.* Kwa hiyo lazima atafutwe na lazima awepo. Lile neno *at least* maana yake unaanzia hapo na kupanda, yaani huwezi kupungua zaidi ya hapo, inabidi uongezeke.

Sasa kwa maneno haya uliyoyatumia pengine yangekuja kwa namna nyingine haya mabadiliko yangekuwa yanaashiria kwamba kama yupo basi awekwe. Lakini sasa kwa namna ilivyoandikwa hapa ikikubaliwa maana yake hii bodi haitakuwa imekamilika isipokuwa kwa kuwepo huyu mtu. Yaani yale maneno *at least* kisheria maana yake hiyo ndiyo *bare minimum.*

Kwa hiyo unakwenda juu ya hapo. Nadhani hilo umeelewa; matumizi ya neno *at least* ni kwamba hiyo ndiyo *minimum.*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, nimekubaliana nayo, hakuna shida.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri umetoa majibu hapa, umesema viachiwe vyombo vya uteuzi, hapa naona ni watu wanachagua. Hapa ni watu wanachagua kwenye mkutano. Sasa hii ya uteuzi siyo, lakini hawa sasa kule wanakochagua na kwa sababu umelisemea hapa Bungeni wao waangalie uwezekano wa huyo mtu kuwepo.

Kama hiki kifungu kingekuwa kimeeleza kuhusu uwezekano, maana kwa ngazi hii sasa hatuwezi kuongeza na kufanya hivi, kama kingekuwa kimeandikwa hivyo tungeenda nacho, lakini kwa yale uliyoyajibu hapa kwenye utekelezaji utapeleka sijui kama unaitwa waraka kwenye chaguzi zile, kule mahali ambapo inawezekana, kadri inavyowezekana, waweke huu uwakilishi, ni muhimu sana, hasa kwenye mambo ya maji.

Kwa sababu athari zake huyu atakwenda mwendo mrefu huyu maana yake atakwenda mwendo mrefu zaidi. Kwa hiyo changamoto za watu

wenye ulemavu anaweza yeye akazizungumza vizuri zaidi kuliko mtu mwingine kwenye hicho chombo ambacho kinasimamia.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa maelezo hayo, kifungu cha 22 kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa tarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2020, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *(The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 pamoja na marekebisho yake sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Nadhani wote wameafiki, hakuna aliyesema hapana ama siyo.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa ajili ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa lengo la

kufanya sheria hiyo kuendana na mabadiliko mbalimbali yaliyotokea katiika sekta ya maji. *A Bill for an Act to Amend The Water Resources Management Act in order to align the provisions of the Act with recent development that has taken place in the water sector.*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa Ajili ya Kufanya Marekebisho Katika Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa Lengo la Kufanya Sheria Hiyo Kuendana na Mabadiliko Mbalimbali Yaliyotokea Katika Sekta ya Maji. *A Bill for an Act to Amend The Water Resources Management Act in Order to Align the Provisions of the Act With Recent Development that has Taken Place in the Water Sector,* ulipitishwa na Bunge**.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeshasoma mara ya tatu, tumemaliza utaratibu wa kutunga sheria. Na kwa hivyo nitumie fursa hii kutangaza kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 *(The Water Resources Management Amendment Bill, 2022)* umepitishwa rasmi na Bunge.

Kwa hiyo Bunge tumeshamaliza sehemu yetu ya kutunga sheria, na kama ilivyo ada tutampelekea Mheshimiwa Rais ili na yeye afanye kwa sehemu yake kwa mujibu wa Katiba yetu.

Kwa hiyo nitumie fursa hii kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wa hiari aliowapata leo; Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mawazingira. Nawapongeza kwa kazi nzuri mliyoifanya. *(Makofi)*

Lakini hasa Mheshimiwa Waziri kwa usikivu wako kwa mawazo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa kwenye ngazi ya Kamati na humu ndani na majibu uliyoyatoa yanatoa matumaini kwamba utekelezaji wa sheria hii utafuata kile ambacho Bunge limepitisha. Na tunakutakia kila la heri katika utekelezaji Mheshimiwa Rais akishasaini muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie pia fursa hii kuwapongeza sana Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji; tunawapongeza sana kwa kazi nzuri mliyoifanya mpaka kufikia hatua hii. Ahsante kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge ambao mmepata fursa ya kuchangia, mmetoa mawazo mbalimbali hapa na pale. Basi yale ambayo yanahitaji pengine hata kuitazama sera yote Wizara wamechukua, watatazama namna gani ya kuboresha hapa na pale ili vyanzo vyetu viwe

salama, na maji yetu kwa sababu yanaongezeka mvua ikija, lakini kama haikuwepo ndiyo yaleyale na wakati mwingine yanapungua kwa ajili ya mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa hiyo ni kazi yetu sisi sote kusaidia kuweka mazingira ambayo tutahakikisha vyanzo vyetu vya maji viko salama na watumiaji wetu wa maji wanalindwa na haki zao; hiyo ni kazi yetu. Pale panapotokea changamoto Mheshimiwa Waziri tuko naye hapa Bungeni, watatusikiliza.

Na ni dhahiri kwa michango mliyotoa Waheshimiwa Wabunge ziko changamoto sehemu mbalimbali, wakati mwingine za watendaji, na kama zilikuwepo za mapungufu ya kisheria basi ni hizi ambazo tumezifanyia kazi hapa ili kutoa fursa kwa watendaji wetu kufanya vizuri zaidi, na pengine kuwajibika kila mtu kwa nafasi yake.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, tunakutakia kila la heri katika utekelezaji. Na watendaji wako wote pia tunawapongeza, nao tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.33 mchana, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 16 Septemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*